ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Mhe. Pandu Ameir Kificho	-	SPIKA
1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi		- MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini		- MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed		-MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary		-MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad		-MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban		-MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji		-MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	-MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	-MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	-MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	-MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	-MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	-MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	-MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	-MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	-MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	- Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	-Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	- Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	-Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	-Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	-Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	- Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	- Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	- Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	- Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	- Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	- Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	- Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	- Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	- Nafasi za Wanawake

37.Mhe. Ashura Sharif Ali - Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Farida Amour Mohammed - Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Fatma Mbarouk Said - Jimbo la Amani

41.Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Kwamtipura

42.Mhe. Hassan Hamad Omar - Jimbo la Kojani

43.Mhe. Hija Hassan Hija - Jimbo la Kiwani

44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Jimbo la Mji Mkongwe

45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Muyuni

46.Mhe. Kazija Khamis Kona - Nafasi za Wanawake

47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Jimbo la Kikwajuni

48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Jimbo la Kitope

49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Jimbo la Mkwajuni

50.Mhe. Mgeni Hassan Juma - Nafasi za Wanawake

51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma - Jimbo la Bumbwini

52.Mhe. Mohammed Haji Khalid - Jimbo la Mtambile

53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi - Jimbo la Chambani

54.Mhe. Mohammed Said Mohammed - Jimbo la Mpendae

55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Nafasi za Wanawake

56.Mhe. Mussa Ali Hassan - Jimbo la Koani

57. Mhe. Mussa Khamis Silima - Jimbo la Uzini

58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Rahaleo

61.Mhe. Omar Ali Shehe - Jimbo la Chake-Chake

62.Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

63.Mhe. Rashid Seif Suleiman - Jimbo la Ziwani

64.Mhe. Raya Suleiman Hamad - Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rufai Said Rufai - Jimbo la Tumbe

66.Mhe. Saleh Nassor Juma - Jimbo la Wawi

67.Mhe. Salim Abdalla Hamad - Jimbo la Mtambwe

68.Mhe. Salma Mohammed Ali - Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Salma Mussa Bilali - Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salmin Awadh Salmin - Jimbo la Magomeni

71.Mhe. Salum Amour Mtondoo - Jimbo la Bububu

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman - Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha - Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki - Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai - Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim - KATIBU

Kikao cha Nane - Tarehe 28 Juni, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Makadirio ya Mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka 2011/2012.

Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Titaifa, Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha, ahsante.

MASWALI NA MAJIBU:

Nam. 196
Rais wa Tanzania Kuongea na Viongozi wa Nchi:

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Mnamo mwezi wa Mei, 2011 alipokuwa anafunga semina elekezi ya viongozi wakuu wa Mawizara, Rais wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete aliwaasa na kuwahimiza Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Manaibu wao pamoja na viongozi wengine waandamizi kujenga umoja na mashirikiano katika utelekezaji wa majukumu yao. Aidha aliwakumbusha kuwa siri kubwa ya mafanikio yao, Serikali na wananchi kwa ujumla itatokana na juhudi zao za kujenga umoja, uwazi na moyo wa mashirikiano na kuwaambia kuwa kinyume chake ni hasara kwa Taifa.

(a) Kwa kuwa Zanzibar chini ya Awamu ya Saba inayoongozwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa (GNU), dhamira yake ya dhati ni sawa na misingi aliyoieleza Mhe. Rais wa Tanzania katika semina hiyo, Je, kwa Zanzibar maelezo hayo ya Rais wa SMT yanachukuliwa kwa uzito gani.

(b) Zipo taarifa kuwa baadhi ya Viongozi wakiwemo Mawaziri na Wasaidizi wao na Makatibu Wakuu na Wasaidizi wao hawana mashirikiano ndani ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Je, jambo hilo ni kweli.

(c) Iwapo malengo ya GNU ni kuondosha ubaguzi na kujenga umoja kama yalivyo malengo ya Mapinduzi Matukufu ya 1964 na kwa kuwa zipo taarifa kuwa badhi ya watendaji wa Serikali wanahudumia wananchi kwa misingi ya ubaguzi, Je, watu hawa bado wanasifa ya kuwa watumishi wa umma.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 196 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, naamini Mhe. Mwakilishi atakubaliana nami kwamba msingi mkuu wa kuwa na Serikali yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa ni kuondoa siasa za hasama, chuki na kutoaminiana na badala yake kujenga nchi yenye umoja, amani, utulivu maelewano na mshikamano wa wananchi wote bila ya kujali jinsia zao, dini zao au eneo analotoka mtu.

   Mhe. Spika, dhamira kubwa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa ni kuhakikisha kuwa viongozi na viongozi na watendaji wote wa serikali wanajenga mazingira ya kujenga moyo wa mashirikiano, uwazi, umoja na tunaamini kinyume chake ni hasara kubwa kwa taifa. Mhe. Spika, kwa mnasaba huu ni dhahiri Serikali ya Zanzibar inayachukulia kwa uzito mkubwa maneno ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete ya kuwa mafanikio ya kweli yatatokana na mashirikiano, umoja, uwazi na mshikamano.

b) Mhe. Spika, hadi sasa hatuna taarifa za kuwepo baadhi ya Viongozi wakiwemo Mawaziri na Wasaidizi wao na Makatibu Wakuu na wasaidizi wao, kukosa ushirikiano ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa umoja wa Kitaifa. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu na wananchi wote wa Zanzibar kuwa yapo maelewano makubwa kati ya Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, Mawaziri na Manaibu Mawaziri na tufanya kazi tikiwa timu moja,
   tunasaidiana na kuna upendo miongoni mwetu. Nathubutu kusema umoja wetu ni wa mfano mkubwa katika Afrika na Ulimwengu mzima.

Mhe. Spika, tuna mifano mingi hapa Barazani tunamuona Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Waziri wa Katiba na Sheria anavyojibu masuala kwa niaba ya Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Mhe. Spika, Rais Mstaafu Mhe. Amani Abeid Karume hivi sasa anatoa mihadhara mbali mbali katika nchi kubwa Duniani namna tulivyofanikiwa katika muundo wetu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

c) Mhe. Spika, ni kweli malengo ya Mapinduzi Matukufu ya 1964 ni kuondoa ubaguzi wa aina zote, dhamira ambayo imeendelezwa na Awamu zilizopita za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na zitaendelezwa na Awamu ya saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa. Dhamira ya Serikali hii ni kuwahudumia wananchi bila ya ubaguzi wa aina yoyote. Serikali haitomvumilia Kiongozi au mtendaji yeyote wa Serikali ambaye atafanyakazi kinyume na dhamira hiyo. Hivyo, nataka niwahakikishie wananchi wote kwamba Serikali yao inawatumikia wananchi wote kwa misingi ya usawa na haki.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru na namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu mazuri na fasaha ambayo nimeridhika nayo. Pamoja na majibu yake mazuri sana naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba malengo ya Mapinduzi na Malengo ya Serikali hii ya Awamu ya saba ni kuwaunganisha Wazanzibari wote. Na kwa kuwe lengo hili la serikali ndio malengo hasa ya dunia na utawala bora. Je, iwapo itatokezea mwanamchi akahisi anabaguliwa ama kwa misingi ya kidini, kisiasa au mkoa au kisiwa, aende wapi kuleleka malalamiko hayo, ili serikali iyajue na iyafanyie kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba serikali yetu siku zote itahakikisha inapambana na ubaguzi wa aina yoyote, bila ya kujali dini, eneo analotoka, au vyengine vyovyote vile. Nia na dhamira ya serikali hii ni kuhakikisha kwamba inatenda haki ya wananchi wake wote na inawatumikia kwa uwadilifu mkubwa.

Mhe. Spika, pale ambapo pametokea kubaguliwa yeyote yule basi serikali yetu ina ngazi mbali mbali za kiutendaji kuanzia kwenye shehia, Wilaya, Mkoa, taifa. Sisi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais saa zote milango yetu ipo wazi kwa yeyote yule atakayeleta malalamiko yake yatashughulikiwa kikamilifu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa fursa kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kujibu majibu yake kwa ufasaha na kwa dhati ya nafsi yake. Na mimi nikiri kwamba nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye sura ya Umoja wa Kitaifa ni kuondoa ubaguzi na kuwaunganisha watu ili wafanye kazi kwa pamoja.

Mhe. Spika, lakini atakubaliana na mimi Mhe. Waziri kwamba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ni viongozi wa Serikali na wao hawapaswi kujiingiza sana kwenye mambo ya siasa.

Lakini wakati viongozi wale watakapofanya kazi zao kwa ubaguzi na kupendelea mambo ya siasa je, Mhe. Waziri yupo tayari kuwachukulia hatua viongozi kama hao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama nilivyokwisha kusema awali kwamba serikali hii haitovumilia mtendaji yeyote kumbagua mwananchi yeyote katika kupata haki zake.

Hivyo hivyo haitegemewi kwa Mkuu wa Wilaya ama Mkuu wa Mkoa kufanya ubaguzi wowote ukiwa wa kisiasa ama wa aina nyengine yoyote, wanachotakiwa ni kutenda kazi zao kwa uwadilifu mkubwa. Na yeyote yule atakayefanya kinyume na hayo atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi.

Nam. 171

Fungu la Miradi ya Wananchi

Mhe. Hamza Hassan Juma - Aliuliza:-

Katika Bajeti iliyopita ya mwaka 2010-2011 Baraza letu tukufu lilipitisha fungu la miradi ya wananchi kiasi cha 500 millioni ili kusaidia juhudi za wananchi kujiletea maendeleo katika majimbo yao.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimeshatolewa hadi hivi sasa kwa ajili ya kusaidia miradi hiyo.

(b) Je, ni miradi mingapi imeshapatiwa fedha hizo Unguja na Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Aliuliza:

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kujibu suali la Mhe. Mwakilishi lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, jumla ya shilingi milioni mia tatu na sitini, laki saba na hamsini zimeshatolewa na Serikali katika mwaka wa fedha 2010/2011 kwa ajili ya kusaidia miradi ya wananchi Unguja na Pemba, hii ni sawa na asilimia 72 ya fedha yote.

(b) Mhe. Spika, idadi ya miradi iliyopatiwa fedha hizo kwa Unguja ni 46 ambayo imegharimu jumla ya shilingi milioni mia moja na thamanini na nane lakini mili na hamsini. Kwa Pemba ni miradi 38 iliyogharimu jumla ya shilingi milioni mia moja na sabini na mbili na laki tano.

Nam. 139

Malipo kwa Wasimamizi wa Mitihani ya Taifa ya Zanzibar

Mhe. Rufai Said Rufai – Aliuliza:-

Suala zima la usimamizi wa Mitihani ya Taifa ya Zanzibar (Std. VII – Form II) ni suala linalohitaji uaminifu na uadilifu mkubwa ili yapatikane matokeo yenye kuaminika na kwa mustakabali mwema kwa Taifa letu.

(a) Je, kuna malipo yeyote yanayolipwa kwa Walimu kutokana na kazi hii adhimu.
(b) Je, kama yanalipwa, hulipwa kwa muda gani na ni kiasi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake namba 139 lenye sehemu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli kuwa kazi ya usimamizi wa Mitihani ya Taifa za Zanzibar (Darasa la saba na kidato cha Pili) inahitaji uaminifu na uadilifu mkubwa ili yapatikane matokeo halali, yenye kuaminika na kwa kujenga mustakabali mwema kwa taifa letu. Baada ya maelezo hayo naomba kujibu kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, walimu wanaoshiriki shughuli za usimamizi wa mitihani wanalipwa posho la usimamizi wa mitihani kwa mujibu wa siku walizosimamia.

b) Wasimamizi Wakuu wa mitihani wanalipwa posho la Shs.15,000/= kwa siku na wasimamizi wa kawaida wanalipwa posho la shs.10,000/=.Kwa mfano kwa mitihani ya Taifa iliyofanyika mwezi Novemba na Disemba 2010, wasimamizi wa mitihani hawajalipwa hadi hii leo kutokana na ukosefu wa fedha. Wasimamizi hawa wanadai jumla ya shs.177,700,000/= . Wasimamizi wa Unguja wanadai shs.101,000,000/= na wasimamizi wa Pemba wanadai shs.76,000,000/=. Kuchelewa kwa malipo ya wasimamizi wa mitihani kunatokana na uchache wa fedha zinazopatikana. Kwa mwaka 2010/2011 jumla ya Shs.1,000,000,000/= zilitengwa kwa ajili ya mitihani na hadi sasa shs.1,050,000,000/= zimetumika kwa kazi mbali mbali za mitihani na bado Wizara ina madeni ya wasimamizi na deni la shs.153,497,000/= zinadaiwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza suali la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri, pamoja na majibu mazuri uliyokwisha kujibu sasa hivi, lakini huoni kama wizara yako inaweza kusababisha walimu wakapoteza *morariti* ya kuweza kufanya kazi zao vizuri ipasavyo kutokana na kuchelewa kulipwa posho zao ambazo ni haki yao ya msingi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli kama binaadamu wanaweza wakapoteza *morali*, lakini mjenga nchi ni mwananchi. Na wao walimu ndio wasimamizi wakuu ndio walimu wakuu wa kutulelea watoto wetu, naamini madhali nia ya Wizara ni kuwalipa walimu hawa basi hawawezi kuhadalika na kitu chochote kile na wataitumikia nchi yao. Kwa sababu wanajua kwamba tunashona nguo tuliyonayo kwa mujibu wa kitambaa ambacho tunacho.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii asubuhi ya leo kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na uwazi aliyoueleza Mhe. Waziri na namshukuru kuwa alikuwa wazi kwa kiango kikubwa.

(a) Napenda nimuulize kwamba kwa kuwa walimu hawa hawa wanachangishwa michango mengine na Wizara haikuwalipa mpaka hivi leo na Bajeti inayosomwa ni ya 2011/2012. Wizara imejiwekea mfumo gani wa kuwambia inawapenda walimu.

(b) Kwa kuwa Wizara ya Fedha katika bajeti ya Serikali iliripoti kurejeshwa kwenye mfuko wa Serikali bilioni 4 inasemekana Wizara ya Elimu ni moja kati ya iliyorejesha pesa. Je, hii ni kweli na kama ni kweli kwa nini mkaiwachia Wizara ya Fedha irejeshe fedha katika fungu la mwaka huo wakati nyinyi hamjawalipa walimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika,

(a) Uwalimu ni wito kwa hivyo walimu wanajua kama sisi Wizara ya elimu tunawapenda na tunawathamini na ndio maana bado wapo na wanaendelea kufanya kazi zao. Nchi zote Mheshimiwa unasikia walimu wanagoma, wanafunzi wanagoma, lakini Zanzibar haijawahi kutokea kwa sababu wanajua licha ya kuwa hatuna lakini tunao bega kwa bega na tunafanya namo mazungumzo tunawaeleza hali halisi ambayo tunayo.

(b) Suala la Wizara ya Fedha kuwa Wizara ya Elimu imerejesha fedha hilo suala si kweli. Hakuna fedha ya Wizara ya Elimu ambayo imerudishwa Wizara ya Fedha. Nakushukuru.

Mhe. Asha Bakar Makame: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza suali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Kwa kuwa walimu nchi yeyote ile ni watu muhimu sana. Nichukue fursa hii kuwapongeza walimu hawa ambao kwa kweli wametumia uzalendo wa hali ya juu kabisa kwa ustahamilivu. Je, atakubaliana na mimi Mhe. Naibu Waziri ni malimbikizo ambayo Wizara yake imeyalimbikiza kutokuwalipa walimu hawa haki yao ya msingi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo Mhe. Naibu Waziri amekuwa akijibu nataka kuongeza majibu pamoja na kumjibu Mhe. Asha Bakari Makame suala lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli katika ule mwaka tunaoufanyia mtihani tunakuwa tunadaiwa, lakini ukifatia mwaka wa pili tukipata pesa tunalipa madeni kwanza, kinachobakia ndio tunaendelea kutumia katika mtihani wa mwaka ule, kwa hivyo tunabakia na deni jengine. Utaratibu huu sio kwamba tunawavunja morali wale. *Infact* wanajua kwamba midamu tunadai, lazima tutalipwa. Huu ndio utaratibu wetu tunaoendelea nao. Kwa hiyo na mimi nawashukuru sana walimu kwa kuwa wastahamilivu na wanajua kwamba wanasimamia mitihani lakini mwaka unaofuatia wanajua kwamba watalipwa pesa zao na hivi ndivyo tunavyofanya. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 100

Kukosekana kwa Uzio Katika Hospitali ya Kivunge

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Aliuliza:-

Kumekuwa na wimbi kubwa la wanyama wanaofungwa ndani ya eneo la Hospitali ya Kivunge, jambo ambalo husababisha hasara zisizo za lazima Hospitalini hapo. Hii ni kutokana na kukosekana kwa uzio katika Hospitali hiyo,

(a) Je, ni lini uzio wa hospitali hiyo utajengwa.

(b) Je, Wizara inachukuwa jitihada gani za kuhakikisha kuwa Hospiltali ya Kivunge inakuwa na hadhi inayotakiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 100 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba hospitali ya Kivunge imekuwa na tatizo la muda mrefu la kufungwa wanyama ndani ya eneo la hospitali.

Naomba nichukue fursa hii kuwajuilisha wananchi kwamba kuanzia leo si ruhusa kufunga wanyama ndani ya maeneo ya hospitali yoyote na sio kivunge tu. Wanyama watakaoonekana wamefungwa au kuzurura ovyo ndani ya eneo la hospitali, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mmiliki wa wanyama hao.

(a) Mhe. Spika, katika kukabiliana na tatizo hilo, Wizara ya Afya imepanga kujenga uzio kwenye hospitali za Kivunge na Makunduchi katika kipindi cha fedha cha mwaka 2011/2012. Ujenzi wa uzio huo utategemea na upatikanaji wa fedha kutoka Serikali Kuu.

(c) Mhe. Spika, kupitia miradi ya maendeleo *(Development Project)* hospitali ya Kivunge ni miongoni mwa hospitali zinazotarajiwa kupandishwa daraja kuwa hospitali ya Wilaya.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nauliza swali dogo tu la nyongeza, amezitaja hospitali za Makunduchi na Kivunge. Atakubaliana na mimi hali

kama hiyo ipo pia na katika Hospitali za Pemba, ikiwemo hospitali ya Micheweni na Chakechake.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, suala hilo lipo katika hospitali zote lakini kwa mwaka huu wa Fedha tutaanza na Makunduchi na Kivunge baadaye tutaendelea na hospitali zinazofuata.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba kwa mwaka huu wa fedha nakusudia kujenga uzio katika Hospitali ya Kivunge na Makunduchi, kwa msingi huo itakuwa fedha imetengwa. Je, kwenye bajeti hii anaweza akatwambia ni shilingi ngapi zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, napenda nimjibu Mwakilishi kwamba fedha za maendeleo zilizomo katika kujenga hospitali hizi ni zile fedha ambazo zinatakiwa zitoke wa wahisani. Zinapofika pale Wizarani ndipo zinapogawiwa kwa mujibu wa kile kinachotakiwa kutengenezwa. Kwa hiyo zifike halafu tutazigawa kwa kujengea uzio.

Nam. 61

Kituo cha Kilimo Chambani

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad – Aliuliza:-

Kituo cha Kilimo kilichofunguliwa katika Jimbo la Chambani miaka mingi iliyopita, ambacho kilikuwa na manufaa makubwa kwa wakulima wa Jimbo hilo ikiwa ni pamoja na kufaidika na ushauri kutoka kwa wafanyakazi wa kiuto hicho, hivi sasa kimetelekezwa baada ya kuhamishwa kwa wafanyakazi wa kituo hicho na kuivunja nyumba waliyokuwa wakiishi baadhi ya Wakuu wa kituo hicho.

(a) Je, ni kwa nini Wizara ilishindwa kukiimarisha kituo hicho ambacho kilikuwa na umuhimu mkubwa katika maendeleo ya Kilimo ya Jimbo hilo na sehemu nyenginezo.

(b) Ni sababu zipi zilizoifanya Wizara kama kuivunja nyumba waliyokuwa wakiishi baadhi ya watendaji wa kituo hicho, ambayo ilikuwa katika hali nzuri.

(c) Wizara ina mpango gani madhubuti na ya haraka ya kukiimarisha kituo hicho ili kukirejeshea hadhi yake ya awali na hivyo kusaidia katika maendeleo ya kilimo hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 61 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara yangu haikushindwa kukiimarisha kituo hicho, isipokuwa palikuwa na uhaba wa wafanyakazi na fedha za matengenezo ya nyumba hiyo ambapo alibakia mfanyakazi mmoja tu baadaye wengine kustaafu. Aidha, nyumba ilivunjwa kwa sababu ilikuwa kongwe na haikuwa katika hali nzuri kwa kukaliwa na watu.

(c) Mhe. Spika, wafanyakazi waliokuwa wakiishi katika nyumba hiyo ya kituo walihamishwa kabla ya nyumba kuvunjwa alikuwa kabaki mfanyakazi mmoja ambae baadaye alihamishwa.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Nashukuru Mhe. Spika, napenda nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kweli kukidhoofisha au kukitelekeza kituo kile cha Chambani wakulima wengi wa jimbo la Chambani wanakuwa na msukosuko mkubwa wa kupata ushauri wa mabwana shamba katika kituo kile.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kukiimarisha kituo kile ili wananchi wapate kupata maelekezo ya ushauri wa kilimo.

b) Hivi sasa kuna rasimali kama michungwa na miembe ile iko katika huduma ya nani hivi sasa pakiwa hapana mfanyakazi hata mmoja.

c) Kwa kuwa ulisema kwamba nyumba ilivunjwa kwa sababu ilikuwa tayari imeshachakaa, kuifanyia matengenezo wakati huo na kujenga nyumba mpya hivi sasa gharama zingekuwa zipi kubwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, nakubaliana naye Mhe. Mwakilishi kwamba ushauri na huduma kwa wakulima ni suala la msingi na muhimu na dhamira ya wizara yangu na sio kwa jimbo lake tu bali kwa wakulima wote nchini kuimarisha upatikanaji wa huduma za ushauri. Kwa hivyo, hili la jimbo lake tutalitizama kwa upeo huo huo ambao tutatizama maeneo mengine.

Mhe. Spika, kituo cha Chambani kilikuwa kituo cha uzalishaji ambapo tulikuwa tunapata mbegu pale kituoni kutokana na hiyo miti ambayo rasilimali

aliyoizungumza yeye. Hivi sasa yuko mfanyakazi mmoja pale ambaye anahudumia miti ile na huwa bado shughuli za kutafuta mbegu kwa hicho hicho kiwango kidogo zinaendelea.

Mhe. Spika, mimi nataka nikubaliane nae kwamba bahati mbaya kituo hicho sijakishuhudia kwa maana hakipo tena, lakini ni dhahiri kwamba inawezekana kwa pande zote mbili pengine ingewezekana kufanya matengenezo ikawa gharama zake ni ndogo zaidi kushinda kujenga upya. Lakini kwa vile sina taarifa za kitaalamu juu ya hali halisi ya nyumba ile na mimi mwenyewe kushindwa kukishuhudia kwa maana hakipo tena nitashindwa kumpa jibu muafaka ambalo litamridhisha yeye.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri ni juzi tu wakati anajibu swali aliendelea kusisitiza kwamba kauli mbiu ya Zanzibar ni Mapinduzi ya Kilimo, na kwa kuwa kuvunjika kwa nyumba ile pale wakulima wanaendelea kulima kilimo cha kienyeji sana ikiwa ni pamoja na *mono culture*, kutia moto mashamba, kukosa ushauri wa maafisa ugani na kwa kuwa maafisa ugani hawana hata pikipiki. Je, kuendelea kuitekeleza nyumba ile na kutojenga nyumba nyengine na kuwakosesha vipando maafisa ugani kwa ajili ya kutoa ushauri kwa wakulima wa Jimbo la Chambani na hata Jimbo la Wawi kule Pemba ni kwenda kinyume na kauli mbiu ya Zanzibar ya Kilimo Kwanza.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, ni sahihi kabisa nimetamka, serikali imetamka nikizungumza serikali kwa maana ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba kauli mbiu ya mageuzi ya kilimo ndani ya nchi yetu ni mapinduzi ya kilimo. Mhe. Spika, nataka niwathibitishie na kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu pamoja na wananchi pamoja kuitaja mimi ni muumini wa mageuzi hayo.

Mhe. Spika, tunaamini kuwa ndani ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwamba tunaweza kusimamia na kutekeleza mageuzi hayo, lakini hatukupata kusema kwamba safari hiyo itakuwa nyepesi. Mhe. Spika, ujenzi wa nchi si shughuli ya lele mama inahitaji umoja na dhamira ya kweli kwa upande wa serikali na kwa upande wa wakulima. Kwa bahati nzuri wakulima wa nchi yetu hawataki kukumbushwa ni watu wenye bidii na dhamira ya kweli.

Mhe. Spika, tumeeleza kwamba tumejipanga vizuri kutekeleza mapinduzi ya kilimo, maelezo yake hapa yatakuwa marefu sana lakini kwa hapa niseme tu kwamba pamoja na mambo mengine uimarishaji wa huduma za ugani na vituo vya utoaji wa huduma vikiwemo vya utafiti na uzalishaji ni miongoni mwa mipango ya wizara yangu na serikali kwa jumla katika mageuzi hayo tunayoyazungumzia ya mapinduzi ya kilimo.

Nam. 13

Mbegu za Kupandishia Ng'ombe Zilizopitiwa na Muda Kupelekwa Pemba

Mhe. Salma Mohammed Ali – Aliuliza:-

Inasemekana hivi karibuni mbegu za kupandishia ng'ombe zilizokwishapitwa na muda wake wa matumizi (*expired*) zipatazo 1000 zilipelekwa Pemba.

(a) Je, Mhe. Waziri, kuna ukweli gani wa taarifa hii.

(b) Je, kama taarifa hizi zina ukweli, huoni kuwa kuruhusu kutumika kwa mbegu hizo ni kusababisha hasara na kuwarudisha nyuma wafugaji.

(c) Je, Serikali iko tayari vipi kuwawajibisha wahusika na kuwalipa fidia wakulima kwa hasara walizozipata.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 13 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, sio sahihi kwamba kuna mbegu za kupandisha ngo'mbe kwa sindano zipatazo mirija 1,000 zilizokwisha muda (*expired*) zilizopelekwa Pemba. Ukweli ni kwamba katika mirija ya mbegu 500 ilioagizwa kutoka Arusha kwa ajili ya kuwapatia wafugaji wa Pemba, mbegu katika mirija 200 zilionekana na ubora hafifu baada ya kuchunguzwa na wataalamu wa Idara ya Mifugo. Na kwa sababu mbegu hizo ziliagizwa kutoka Kituo cha *National Artificial Insemination Centre* (*NAIC*) cha Arusha, mbegu hizo katika mirija 200 zilirejeshwa kwao na kufidiwa mbegu nyengine mirija 200 zenye ubora mzuri tayari zimeshasambazwa kwa wafugaji.

(b) Mara baada ya kupokea mbegu na kabla hazijasambazwa kwa wafugaji, Idara ya Mifugo kwa kutumia Maabara zake hupima ubora wa mbegu hizo ili kukwepa kuwatia hasara wafugaji wetu. Mbegu zinazogundulikana na vipimo vyetu kwamba zina ubora mzuri huruhusiwa kusambazwa kwa wafugaji na mbegu zinazoonekana na vipimo vyetu vina ubora hafifu huzuiwa kusambazwa kwa wafugaji.

c) Mhe. Spika, wizara yangu ipo tayari kumchukulia hatua za kinidhamu mfanyakazi yeyote ikitokea kufanya uzembe na kuwapa hasara wafugaji wetu, na kwamba wizara ipo tayari kushauriana na wafugaji juu ya namna ya fidia au msaada katika kuendeleza mbele shughuli za mifugo nchini kama ambavyo imekuwa ikiwasaidia katika programu mbali mbali zinazoandaliwa na kusimamiwa na Serikali kupitia wizara yangu.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

a) Kwa nini Zanzibar iagize mbegu kutoka Arusha wakati wizara inacho kituo cha kupandishi kama kilichoko Arusha.
b) Mhe. Waziri haoni mbegu kutoka Arusha zinakuwa ghali kuweza kununuliwa na wafugaji.
c) Je, wizara yako ina mpango gani wa kuondokana na tatizo hili.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ni kweli kwamba wizara yangu inacho kituo cha AI pale Maruhubi na tulilazimika kuagizia mbegu Arusha hadi hii leo kwa sababu mtambo wa *liquid nitrogen* ambao ni muhimu sana katika kuhifadhi mbegu ilikuwa imeharibika. Ni mwaka jana tu ndipo ambapo serikali kupitia wizara yangu imenunua mtambo mpya kwa shilingi milioni mia sita na tayari umeshafungwa unafanya kazi.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba mbegu kutoka Arusha zinakuwa ghali kwa sababu hulazimika kumtoa mtu hapa kwenda Arusha kutoka Zanzibar hadi Arusha kunahitaji nauli hiyo ndio husababisha mbegu kutoka Arusha ziwe ghali.
Mhe. Spika, ili kuondokana na hilo ni kwamba wizara yangu imo katika mipango ya kuona kwamba kituo cha Maruhubi kinaimarishwa ili kiweze kutoa mbegu kwa ajili ya wafugaji wa Zanzibar na hatua zifuatazo ndio ambazo hivi sasa zinachukuliwa. Kwanza mtambo wa *liquid nitrogen* ni tayari upo na juzi mwezi wa Mei Mhe. Rais alikwenda pale akaukagua.

Pili, ni kwamba maabara ya kituo hicho hivi sasa yamemaliza kukarabatiwa na hatua ya tatu ni kwamba leo hii Mkurugenzi wa Idara ya Uzalishaji wa Mifugo anafanya safari ya kwenda Kenya kwa ajili ya kununua madume bure na kuyaleta pale. Na hatua ya mwisho ya nne ni kwamba wizara imo katika maandalizi ya kuliandaa shamba ambalo litatoa malisho kwa ajili ya kituo hicho.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, ahsante sana katika majibu yake Mhe. Waziri alisema kwamba mbegu zinaponunuliwa au pengine pale zitakapokuwa tayari zetu sisi zinapelekwa kwenye maabara ili kuchunguzwa uzima wake. Mimi napenda nimuulize kwamba je, baada ya kutizamwa uzima wake na zikaonekana kwamba zinafaa kupelekwa kwa wakulima. Mhe. Spika, huwa kunakuwa na ufuatiliaji wa asilimia ngapi zilizofanikiwa zile mbegu kwa wakulima ili kuonekana kweli ubora ulionekana katika maabara ni sahihi na ule unaonekana katika mashamba.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, mara baada ya kuonekana kwamba mbegu zina ubora mzuri kinachofuatilia ni kwamba wanaohusika na shughuli za kupandisha mbegu ndio ambao wanaoifanya hiyo kazi baada ya mfugaji mwenyewe kuomba kufanyiwa kazi hiyo.

Mhe. Spika, mara kwa mara Maafisa wa Idara ya Mifugo wanaoshughulika na suala hili huwa wanawapitia wafugaji wetu kuona kwamba mbegu ambazo tumewapelekea zimesadifu katika shughuli ambayo imekusudiwa au vipi. Kwa hivyo, kazi hiyo inafanyika mara kwa mara na watu wetu katika vituo mbali mbali katika Wilaya zetu Unguja na Pemba.

Nam. 22

Mpango wa Kukipanua Kiwanja cha Ndege cha Unguja

Mhe. Ali Salum Haji - Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kukipanua kiwanja cha ndege cha Unguja na tayari imeingia kwenye mkataba na mkandarasi kwa kazi hiyo. Na kwa kuwa tangu mkataba huo ufungwe, mkandarasi huyo bado hajaanza kazi kutokana na wananchi wa eneo la upanuzi wa kiwanja kutohama katika maeneo ya ujenzi kwa sababu ya kutolipwa fidia na Serikali ya bilioni 1.7.

(a) Sababu zipi zilizopelekea hadi sasa wananchi hao wasilipwe fedha zao.

(b) Je, lini Serikali inatarajia kuwalipa fedha zao wananchi hao.

(c) Je, ni lini mkandarasi ataanza kazi zake ambazo hazitokiuka mkataba na Serikali kuingia hasara.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inaendelea na mpango wa kukipanua Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar na tayari imeingia mkataba na Kampuni ya *Beijing Construction Engineering Group* ya China kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la abiria.

Mhe. Spika, katika eneo la ujenzi kulikuwepo na nyumba na miti ya wananchi wizara imeanza kulipa fidia kwa baadhi ya nyumba hizo na miti mpaka kufikia mwezi Disemba, 2010 jumla ya shilingi milioni 500 zilikuwa zimelipwa kati ya shilingi bilioni 1.6 zilizokadiriwa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika kama nilivyokwishakueleza katika maelezo yangu ya awali Serikali imeanza kulipa fidia katika eneo hilo kwa wakati muafaka kwa mujibu wa taratibu za ulipaji fidia na hapakuwepo na sababu yoyote iliyopelekea wananchi waliokuwepo katika eneo hilo kutolipwa fidia. Serikali itaendelea kulipa fidia wananchi waliobakia katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha kadri hali ya upatikanaji wa fedha itavyoruhusu na kwa kuzingatia program ya kazi za mradi huu ilivyopangwa.

(b) Mhe. Spika, hivi sasa Mkandarasi tayari ameanza kazi za ujenzi wa jengo hilo la abiria sambamba na ujenzi wa jengo la uwekaji mitambo (*machine room*) ambapo kazi za uwekaji msingi katika jengo hilo la mtambo imekamilika na kuendelea na kazi hiyo katika jengo la abiria kama programu ya ujenzi huo inavyoelekeza na hakuna ukiukwaji wa mkataba uliofanyika hadi hivi sasa ambao ungepelekea kuipa hasara Serikali.

(c) Mhe. Spika, kama mambo yatakwenda vizuri ujenzi huu unatarajiwa kukamilika katika wakati uliopangwa wa miezi 36 kuanzia Julai 2010.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, serikali ilifanya jitihada ya kujenga uzio katika uwanja wetu wa *Karume International* lakini kwa bahati mbaya au bahati nzuri uzio ule kwa muda mrefu umesimama na inapelekea wanyama wengi kuingia katika kiwanja kile tatizo ambalo

linaleta usumbufu kwa ndugu zetu wa uokozi baada ya kusubiri suala la majanga wanaanza kufukuza wanyama wale kwa kutumia magari yao na kupoteza gharama kubwa ya mafuta.

Je, ni lini wizara yake itatumalizia uzio ule ili kuja kuepusha usumbufu wa wanyama wanaoingia kwa hatarisho kwa ndege zinazotua katika uwanja ule.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwa kipindi takriban zaidi ya miezi mitatu ujenzi wa uzio ulikuwa umesimama sababu zilikuwepo nyingi lakini miongoni mwao ilikuwa ni maongezi ambayo yalikuwa yakiendelea kati ya wizara yetu na serikali kwa ujumla na wawekezaji.

Mhe. Spika, serikali baada ya kutafakari kwa kina imeamua ujenzi huo uendelee kujengwa na matarajio yetu kuanzia mwezi wa saba ujenzi wa uzio huo utaendelea chini ya mkandarasi wa kampuni ya SOJEA kama tulivyokubaliana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ahsante naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, ziko taarifa kwamba ujenzi huo unaofanyika wa jengo jipya la abiria litaweza kuchukua ndege tatu kwa wakati mmoja, sasa chini ya mipango mikubwa ambayo inasimamiwa na serikali hii yakuijenga Zanzibar mpya ambayo uchumi wake unategemewa utaimarika na kuongeza harakati kupitia katika viwanja vya ndege na bandari zetu. Mhe. Spika, hatuoni kwamba baada ya kazi kubwa ya kuteseka na kiwanja hiki muda mrefu kulikuwa na haja ya kujenga kiwanja ambacho kitaweza kweli kuifanya Zanzibar kuwa kituo cha biashara na kuweza kuhudumia abiria wengi zaidi katika eneo hili.

b) Mhe. Spika, ziko taarifa kwamba katika ujenzi huo kumesahauliwa suala zima la kuwepo kwa ghala ambayo ingeweza kushughulikia mizigio kwa ukubwa kulingana na mahitaji ya kiwanja hicho kipya. Lakini suala hili linasemekana liliachwa. Je, ni kwa nini liliachwa na kuna hatua gani za kurekebisha hali hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, matarajio ya serikali kutokana na kuboresha uwanja wetu wa *Karume Internationa Airport* haya yanayotarajiwa yakiwemo ukubwa wa run way, huduma za forodha, huduma za afya pamoja na jengo jipya la abiria ni dhahiri

kwamba hii huduma ya kukuza kiwanja cha ndege kwa ajili ya kutanua kwa huduma za kibiashara zitakuwa zimefikiwa.

Mhe. Spika, pia ni kwamba kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi unaoendelea tumekubaliana kwamba ujenzi unaokwenda ni kwa mfumo wa *design and constructor*. Mhe. Spika, kwa maana hiyo hakuna sehemu wala sio kweli kwamba sehemu ya ghala itakuwa imesahauliwa, mahitaji yote tuliyoyahitaji sisi kama wenye mradi tumewapatia na wao wanatujengea.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, tulipofanya ziara ya kukagua kiwanja chetu cha ndege tulipata maelezo kwamba ndani ya ule uzio kuna mali ya mtu ambayo hajalipwa fidia na kwa sababu hiyo ule uzio wenyewe umewekwa mlango wa bwana yule kuja akitizama zile mali zake ndani ya uwanja, hii ni sababu ya kupitisha ng'ombe wakija mle uwanjani. Je, habari hizi ni kweli na kama ni kweli wizara yake ina mpango gani wa kumlipa fidia yule bwana na ule mlango ufungwe ili ng'ombe wasiendelee kuingia.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, si kweli kwamba kuna mtu ambaye hajalipwa fidia na eneo lake limo ndani ya uwanja, na hiyo milango ambayo haijazibwa ilikuwa ni kutokana na mkataba wetu na hiyo kampuni ambayo ilikuwa ikijenga tulikubaliana nao namna ya milango ya kuweka tulikuwa hatujafikia muafaka. Mhe. Spika, baada ya kwishakukubaliana hayo maeneo ambayo unahisi yana milango yatawekwa milango hiyo ambayo tumekubaliana, maeneo ambayo kuna watu ambao hatujawalipa fidia ni maeneo yaliyoko kwenye makaburi ambapo ujenzi wa uzio bado haujafika.

Nam. 74

Viwango vya Wachezaji

Mhe. Shadya Moh'd Suleiman – Aliuliza:-

Zanzibar ina viwanja viwili vya michezo vya kisasa ambavyo ni Amani kwa Unguja na Gombani kwa Pemba. Lakini kuwa na viwanja hivyo bila ya kuwa na timu bora wananchi hawataona umhumimu wa viwanja hivyo zaidi ya kule kufanyika sherehe za kitaifa kama vile sherehe za Mapinduzi.

Je, Mhe Waziri wizara yako itafanya kitu gani katika kukuza viwango vya wachezaji wetu hasa katika mpira wa miguu, mpira wa pete, riadha na michezo mingine.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 74 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika kukuza viwango vya wachezaji wetu wa michezo mbali mbali hapa Zanzibar, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inakusudia kufanya yafuatayo kwa kuanzia na bajeti ya mwaka 2011/2012:-

1. Kutoa mafunzo kwa makocha na walimu wa michezo mbali mbali.

2. Kusaidia vifaa vya michezo kwa vyama na vilabu vya michezo Wilayani.

3. Kufanya matamasha na mabonanza ya michezo kwa lengo la kuinua vipaji na ushajiishaji wa wananchi washiriki katika michezo, mijini na vijijini.

4. Kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa lengo la kuendeleza michezo maskulini, kwa lengo la kuibua vipaji na kumjenga mwanafunzi kiafya na kiakili.

5. Kusimamia na kuvisaidia vyama vya michezo vya Taifa kuendeleza mashindano mbali mbali yaliyoandaliwa kwenye kalenda zao za kila mwaka.

6. Kuandaa semina za maelekezo kwa viongozi wa vyama vya michezo ili kuleta ufanisi katika vyama vyao.

7. Kuandaa mashindano kwa taasisi za Serikali na Mashirika ili kuleta mwamko zaidi wa kimichezo sehemu za kazi.

8. Kusimamia uanzishwaji wa viwanja vya michezo vya kudumu kwa kila Wilaya.

9. Kuimarisha utendaji kazi wa mabaraza ya michezo ya Wilaya kwa lengo la kuendesha vyema harakati za michezo Wilayani.

10. Kuvisaidia vyama vya michezo kupata uanachama wa kimataifa kwa mujibu wa taratibu za taasisi hizo.

11. Kuviimarisha viwanja vyetu viwili vikuu vya Amani na Gombani pamoja na kukiimarisha Kiwanja cha Mao-Tse-Tung kwa mashirikiano na wadau mbali mbali.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa kuna aina nyingi za michezo na kwa kuwa hivi sasa michezo ni ajira katika ulimwengu kwa vile tuna viwanja viwili vya michezo vyote ni vya mpira wa miguu. Je, ni lini serikali itajenga viwanja vya michezo vyengine katika nchi yetu Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Mwakilishi sasa hivi tuna viwanja vingi sana hivyo hatuwezi kujenga viwanja vyengine kwenye jibu langu mama nimesema tutajenga viwanja kila Wilaya.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Kiwanja cha Mao-Tse-Tung nacho ni kiwanja kimoja wapo hapa Zanzibar tunakitegemea kwa michezo. Je, ni lini tutakifanyia marekebisho kiwanja hiki.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kama nilivyojibu kwenye swali mama kuwa Kiwanja cha Mao-Tse-Tung kwa kushirikiana na wafadhili mbali mbali Mwenyezi Mungu akitujaalia tutakijenga kiwe na hadhi ya kitaifa.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa suala la soka sasa hivi ni ajira Zanzibar na ulimwengu wote kwa jumla. Je, haoni kuna haja ya kushauriana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili suala la michezo likawekwa kuwa ni somo katika maskuli yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kama nilivyojibu kwenye swali mama nimesema kuwa tutashirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na serikali ili kuibua vipaji vya wana michezo hasa wanafunzi.

Nam. 82

Uokoaji wa Mikarafuu

Mhe. Farida Amour Mohammed – Aliuliza:-
Zao la karafuu kwa muda mrefu limekuwa tegemeo kubwa katika kuimarisha uchumi hapa nchini. Hata hivyo huko Pemba mikarafuu inaonekana kupungua kwa kasi kwa kukosa matunzo.

Je, serikali kupitia wizara husika imeandaa mikakati gani kuokoa zao hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 82 kwa kuanza na utangulizi kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nataka nikubaliane na Mhe. Mjumbe kwamba zao la karafuu limekuwa ni tegemeo kubwa na muhimili muhimu wa uchumi na umaarufu wa Zanzibar Duniani. Pia karafuu za Zanzibar zimekuwa na ubora wa kipekee ikilinganishwa na zile zinazozalishwa na washindani wetu na kwamba sifa hiyo imezifanya karafuu za Zanzibar kuwa na nafasi ya pekee katika soko la karafuu duniani.

Hata hivyo, Mhe. Spika, cha kusikitisha ni kwamba, katika miaka ya hivi karibuni uzalishaji wa zao hili hapa Zanzibar umeonyesha kushuka tena kwa kasi kubwa. Katika kulitafutia ufumbuzi tatizo hili, serikali kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ilifanya utafiti wa jumla kuhusu uchumi wa zao hilo na wajibu wa *ZSTC* kwa lengo la kubainisha uwezo, udhaifu na pia kuangalia fursa zilizopo za kuliendeleza zao hilo la karafuu. Taafira za utafiti huo tayari zimewasilishwa na kuzingatiwa na serikali, taarifa ambayo inayotumika katika misingi wa kuandaa Mkakati wa Kuendeleza zao la Karafuu (*Zanzibar Clove Development Strategy*).

Mhe. Spika, wizara hivi sasa inatekeleza mapendekezo ya mkakati huo kwa kuangalia mambo yafuatayo:-

- Kufanyia Marekebisho ya Muundo wa Shirika la Biashara la Taifa – *ZSTC*
- Kuandaa sheria mpya ya *ZSTC*
- Kuandaa sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu utakaosimamia zao hilo moja kwa moja suala zima la karafuu pamoja na kuongeza uzalishaji wake.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri namuuliza wizara yake kupitia Shirika la *ZSTC* imewahi kufanya tathmini ya kujua ni mikarafuu mingapi ilikuweko miaka mitano au kumi ya nyuma na sasa iko mingapi, baada ya miaka mitano ijayo itabakia mingapi. Kama hakuna tathmini hiyo. Je, huoni kama si suala zuri kiuchumi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda: Mhe. Spika, nimesema katika jibu la swali lake mama kwamba, taarifa ya utafiti huo ndio inayotumiwa na katika taarifa hiyo Mhe. Spika, imeeleza kwamba mikarafuu ya zamani mingi sasa hivi uzalishaji wake umeshuka na ipo haja kubwa ya kupanda mikarafuu mipya. Tayari mkakati huo umeshaanza kufanyiwa kazi na kufuatia ziara tuliyokwenda na Mhe. Rais tumeona katika shamba lisilopungua ekari 3 tayari mikarafuu imepandwa na imeanza kuzaa katika kipindi kifupi tu cha miaka mitano. Kwa hivyo, mikarafuu ile mikongwe haizai vizuri lakini kuna uwezo mkubwa wa kupanda mikarafuu mipya na itazaa kwa muda mfupi.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri licha ya kuwaimarisha wapandaji wa mikarafuu. Je, kuna uwezekano gani wa kuwapatia mikopo wakulima hao ili zao hili lizidi kuimarika kisiwani Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda: Mhe. Spika, nimeeleza kwamba, katika mkakati mzima wa kulifufua zao hili katika kujiongezea karafuu kutakuwa na Mfuko maalum *(Clove Development Fund)*. Mfuko huu utawezesha kuwahamasisha wakulima katiak kuendeleza zao la karafuu kama ni kutoa mikopo au kuwanunulia mikarafuu wakapanda, au kuwapa pembejeo nyegine zozote zitakazohitajika katika kuendeleza zao hilo.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. kwa kuwa kila siku zikienda mbele zao la karafuu linaonekana kushuka thamani. Je, wizara haioni kwamba ipo haja ya kubadilisha mfumo wa kutegemea karafuu na kutafuta mfumo mwengine wa uchumi hasa kwa wananchi wa Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda: Mhe. Spika, tayari serikali imelitambua hilo, kwamba sio tu zao la karafuu katika soko la dunia bei yake inapanda ikishuka, lakini haja nzina ya kupanua wigo wa jinsi gani uchumi wa Zanzibar tutaweza kuuinua, na ndio maana utakuta serikali sasa hivi haitegemei zao la karafuu peke yake. Kuna suala zima la utaliio, lakini pia pamejitokeza zao la mwani na mazao mengine ya kilimo yako katika kuwekwa kwenye mkakati wa kuyawekea nguvu ili kuinua uchumi wa Zanzibar.

Nam. 56

Tatizo la Maji kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kabla ya kujibiwa swali langu Nam.56 nataka nimpongeze kwa dhati kabisa Waziri wa Afya, Mhe. Juma Duni Haji kwa muda mfupi tu toka kukalia kiti

hiki na mageuzi anayoendelea kuyafanya kwa muda huu, ikiwemo kupeleka madaktari Pemba na suala la maji katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na Hospitali ya Wazazi Mwembeladu. Sasa niko tayari kujibiwa swali langu Mhe. Spika.

Katika Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar bado kuna tatizo kubwa la maji kiasi
cha kuathiri huduma za afya zinazotolewa hospitalini hapo.

(a) Je, Mhe. Waziri, huoni kwamba Wizara inalo jukumu la kusaidia katika kulimaliza tatizo hilo kwa haraka.

(b) Je, wizara yako ndio yenye jukumu hilo, imeandaa mpango gani katika kuhakikisha kuwa tatizo maji la kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja linamalizika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 56 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, nakiri kwamba wizara yangu ina jukumu la awali la kuwapatia wateja wa majumbani, wafanyabiashara na taasisi ikiwemo Hospitali ya Mnazi Mmoja huduma ya maji safi na salama.

(b) Wizara yangu ipo karibu sana na Wizara ya Afya katika kuona tatizo la maji linaondoka, hii ni kutokana na hatua tulizozichukua ikiwemo kutafuta njia ya kuweka laini ya ziada itakayowezesha kupata huduma hii muhimu. Itakumbukwa kwamba, hivi karibuni Wizara ya Afya ilifanya uzinduzi wa kisima kitakachotumika kupeleka maji katika Hospitali hiyo ya Mnazi Mmoja na Mhe. Waziri aliahidi kushirikiana na wizara yangu katika kufanya uchunguzi wa maji yatakayopatikana katika kisima hicho na kuangalia kama yako safi na salama kwa ajili ya huduma mbali mbali ya matumizi ya wanaadamu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, wananchi au wagonjwa walioko katika Hospitali ya Mnazi Mmoja wategemee lini kupata huduma nafuu katika tatizo hilo sugu la maji.

Pili suala la kutafuta laini ya maji limeanza lini na lini litakamilika.

Tatu, jana Mhe. Naibu Waziri alitoa indhari kuhusu kuzungukwa na maji ya bahari, unaweza kunambia kisima hiki kilichochimbwa na Wizara ya Afya kiko katika maeneo gani.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa sababu suala lenyewe linagusa wizara yangu naona kutoa nyongeza ya maelezo. Kisima tulichokichimba kiko katika ile nyumba inayoitwa *Victoria Garden* na maji tuliyoyapata tumeshirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kutafuta na sijui kitaalamu kwamba itafahamika, maji yale ni sahihi hayana chumvi, *PH* yake ni 7.1 na maji yaliyo safi yanatakiwa yawe na *PH 7*. Kwa hivyo, mnaweza mkaona na waliotupa vipimo hivyo ni Idara ya Maji.

Hivi sasa Hospitali ya Mnazi Mmoja hakuna matatizo ya maji baada ya kisima kile kutumika siku 60 wakati maji ya idara hayapo na hayakupungua. Na katika Hospitali ya Mwembeladu ndio hivyo hivyo, nako tumeshirikiana nao na sasa nako hakuna matatizo ya maji.

Hospitali ya Wagonjwa wa Akili nayo ilikuwa na tatizo la maji nako tumeshirikiana na Idara ya Maji sasa hivi pia hakuna tatizo la maji. Kwa hivyo, kwa hospitali zetu kubwa hizi tatu suala la maji safi na salama kutumia pale ambapo mfumo wa maji wa serikali una matatizo, kama hauna matatizo tutaendelea kupata maji kwa wagonjwa wetu. Nashukuru Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na majibu ya nyongeza ya Mhe. Waziri wa Afya naomba kuuliza swali la nyongeza. jana alipokuwa akizungumza na viongozi wakuu Balozi wa Marekani aliishauri Zanzibar ili kuondokana na tatizo la maji basi tuangalie uwezekano wa kutumia bahari yetu kwa ajili ya maji kwa Wazanzibari. Mhe. Balozi aliamini kwamba maji ya bahari yanaweza yakamaliza kabisa tatizo la maji Zanzibar na kutokana na kulalamika kwa kila siku kesi ya maji. Je, ushauri huu Mhe. Waziri anauonaje.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba pia kusaidia maelezo kuhusu ushauri wa Balozi wa Kimarekani. Si jambo baya kutumia maji ya bahari kupata maji ya kawaida, na utaratibu unaotumiwa kitaalamu unaitwa *distillation*. Lakini unapotumia maji ya bahari kugeuza ya kawaida unapata chumvi nyingi sana, kwa sababu maji ya bahari yana chumvi inayoitwa *Sodium Chloride*. *Sodium Chloride* tunaitumia kwa shughuli nyengine za kawaida ikiwa pamoja na kula, lakini ikiwa nyingi inaweza ikatupa matatizo ya jinsi ya kuitumia. Kwa hivyo, kabla hatujafanya maamuzi hayo tunahitaji kuzingatia *secondary effect* zinazoweza kutokea kwa kukusanya chumvi nyingi itakayokuwa ina matatizo kutumika. Mhe. Spika, nakushukuru.

Nam. 197

Kongamano la Katiba

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu naomba swali (b) mstari wa tatu kwenye neno ‘mkataba’ tuongeze maneno ‘mkataba halisi kwenye saini ya viongozi wetu waanzilishi’. Baada ya marekebisho hayo Mhe. Spika, naomba sasa nijibiwe swali langu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tuongeze maneno hayo aliyotaja Mhe. Mjumbe.

Ndani ya mwezi wa Machi 2011 Wazanzibari kama walivyowenzao wa Tanzania Bara walipata fursa ya kushiriki Kongamano la Katiba Mpya ya Jamhuri Muungano wa Tanzania, Mswada ulodhamiria kuundwa kwa Tume ya kukusanya maoni yao kabla ya kupelekwa Bungeni. Kwa bahati mbaya wananchi waliopata nafasi ya kutoa maoni yao kwa Kongamano hilo kwa zaidi ya asilimia tisiini (90%) husasan pale walipoambiwa suala la Muungano lisizungumzwe.

(a) Kutokana na matukio yaliyotokea katika Kongamano hilo, Serikali ya Zanzibar imejifunza nini kutokana na hoja hii ya Katiba Mpya.

(b) Wazanzibari wengi kama si wote hususan vijana wenye umri sawa au chini ya umri wa Muungano wamekuwa wakidai kwa muda mrefu kuona Mkataba wa Muungano (*Article of Union*) ambao uliyataja mambo 11 ya msingi ya Mkataba huo, Je, Serikali ya Zanzibar ni lini itaotoa hadharani Mkataba huo.

(c) Miongoni mwa dosari zilizosababisha Wazanzibar kuukataa mswada ni pamoja na SMZ kutoshirikishwa ipasavyo wakati wa maandalizi. Zipo taarifa kuwa Mswada huo umerekebishwa na karibu utaletwa tena. Je, SMZ imeshirikishwa vipi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 197 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba rasimu ya awali ya Mswada wa Sheria wa kuunda Tume ya Katiba iliweka sharti kwa

baadhi ya maeneo kutojadiliwa na hivyo kufanya wananchi kuhoji kwa wingi.

Kwa kuwa msingi wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ni Muungano kati ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar haikuwa sahihi kukataza kuzungumza kuwepo kwa Muungano kama vile hilo ndilo jambo la msingi linahitaji kupatiwa ufumbuzi. Kwa kuzingatia suala hilo, rasimu mpya ya Mswada iliyotayarishwa na Wanasheria Wakuu wa Serikali ya Muuongano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na watendaji wao kwa pamoja walikubaliana kuonda sharti la kutojadiliwa kwa baadhi ya maeneo muhimu wakati wa mchakato wa Tume ya Katiba ya kukusanya maoni.

Kwa msingi huo Mhe. Spika, naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kuwa Serikali ya Mapinduzi imekuwa makini katika kuhakikisha rasimu mpya ya Mswada inatoa fursa kwa wananchi kuzungumza mambo yote muhimu yanayohusu Muungano bila ya vikwazo.

Serikali ya Mapinduzi imejifunza kwamba ni lazima kwa mambo ya Muungano serikali zote mbili zishirikiane tokea mwanzo wa maandalizi ya jambo hilo, vyenginevyo inaweza kusababisha kutokufahamiana baina ya serikali zetu mbili. Kitendo hiki hatukipendi kutokea.

(b) Mkataba wa Muungano wa 1964, uliorodhesha mambo 11 ya awali kama mambo ya Muungano ambayo ni:-

- Katiba ya Jamhuri ya Muungano
- Mambo ya Nje
- Ulinzi na usalama
- Polisi
- Mamlaka juu ya mambo yanayohusu hali ya hatari
- Uraia
- Uhamiaji
- Mikopo na Biashara za Nchi za Nje
- Utumishi katika Serikali ya Muungano
- Kodi ya Mapato na Ushuru wa Forodha
- Bandari, Usafiri wa Anga, Posta na Simu.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba watu wengi hawaujui mkataba wa Muungano wa asili ingawa nakala za mkataba huo zipo nyingi tu. Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 ya mwaka 1984, sheria yeyote au hati yeyote inakuwa halali kwa ajili ya matumizi ama baada ya kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali, au kwa hati hiyo au Sheria iliyoainisha tarehe ya kuanza kwake, au kuanzia tarehe ambayo hati hiyo imetiwa saini. Kuwepo kwa Hati au Sheria za asili ni suala la uwekaji wa kumbukumbu tu, lakini kutokuwepo kwake hakuathiri uhalali wa hati au sheria husika. Hata hivyo, wizara yangu imeanza kuchukuwa hatua za kuhakikisha kwamba Hati hii kwa sababu inaulizwa na watu wengi sana Wazanzibari basi hati hiyo tunaanza kuhakikisha kwamba hati hiyo ya asili inapatikana.

(c) Baada ya Wazanzibari kutoa maoni yao mazuri kuhusiana na mchakato wa rasimu ya mswada wa kuunda Tume ya Kuchunguza Katiba Mpya ya Tanzania, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais aliwasiliana na Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano kumuelezea mapungufu yote ambayo Wazanzibari waliyaeleza.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na watendaji wengine wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wamefanya vikao vinne na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na watendaji wake ambapo kati ya vikao hivyo vinne, vikao vitatu vilifanyika Zanzibar na kimoja kilifanyika Dar es Salaam.

Mhe. Spika, Wanasheria Wakuu walifanya vikao hivyo kwa pamoja na walikubaliana na rasimu mpya ya mswada ambao utapelekwa serikalini na hatimae kuwasilishwa tena Bungeni.

Baadhi ya maeneo muhimu ambayo wamekubaliana ni:-

- Muundo wa Tume ya kukusanya maoni ya wananchi juu ya Katiba Mpya na utaratibu wa uteuzi wa Wajumbe.
- Ushauri wa Kisheria katika kuunda Tume uzingatie pia ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.
- Muundo wa Bunge la Katiba na Utaratibu wa Uteuzi wa Wajumbe.
- Utaratibu wa kuthibitisha katiba mpya kwa kura ya maoni kwa kila upande wa Jamhuri kukubali kwa asilimia iliyokubalika.

Maelezo haya tunakusudia kuyaleta kwa Waheshimiwa Wawakilishi ili kuwaelimisha, kuwaarifu na kutoa michango yao hivi karibuni baada ya kumaliza hatua ndogo ndogo za rasimu hiyo na baada ya kupeleka taarifa hii kwa Baraza la Mapinduzi na kupata idhibi yake pamoja na maelekezo yake. Vile vile utakuwepo utaratibu wa kuwaelezea Wazanzibari hatua zote za mswada huu ulipofikia. a Bunge la Katiba.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu marefu sana ya Mhe. Waziri ambayo nimeyakubali na ninayaamini, naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Katika majibu yake ameonesha kama kwamba mkataba huu kwa sasa hivi hanao kama vile uliwahi kupotea. Je, uliwahi kupotea wapi.

(b) Mhe. Waziri anaweza akatuahidi kwamba siku ya kusomwa bajeti ya wizara yake atatuletea humu ndani ya Baraza kopi halisi ya mkataba ule ili wawakilishi tukauona kwa niaba ya wananchi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nilitoa maelezo marefu ili kuwapa nafasi wananchi waelewe hali yote ilivyo na ninaamini wananchi pamoja na Baraza lako tukufu limeelewa. Bahati mbaya Mhe. Mwakilishi hakunifahamu niliposema kwamba, mkataba huo wa Muungano hivi sasa mimi sinao ofisini kwangu na nikasema kwamba nitajitahidi niweze kuutafuta angalau kama nikiupata sioni shida kuuleta. Lakini siahidi mbele ya Baraza lako Mhe. Spika, kwamba wakati wa bajeti nitauleta kwa sababu sijui kama nitaupata au sitoupata.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa na mimi fursa ya kuuliza swali la nyongeza. kwa kuwa Mhe. Waziri wakati alipokuwa akijibu ametueleza yale mambo ambayo yalikubaliwa katika mkataba wa Muungano, na kwa kuwa Muungano huu ulikuwa wa pande mbili zilizoshirikiana baina ya Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Zanzibar ndio ikaunda Serikali ya Muungano wa Tanzania, na kwa kuwa kati ya mambo haya 11 aliyoyataja kuna mambo ambayo tunayaona kwa upande wa Zanzibar ambayo yanarejesha nyuma. Kwa mfano, uchumi wa Zanzibar kama vile ushuru wa forodha, mambo ya nje na mengineyo.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Wananchi wa Zanzibar wanapoona kama kuna haja ya mambo haya kutolewa kwenye mkataba ule ni utaratibu gani unaotumika ili kuyatoa mambo hayo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, serikali hii ni ya wananchi, imewekwa na wananchi, na serikali hii inasikiliza maelezo ya wananchi.

Ninachoomba hivi karibuni tutakuwa na mchakato mzima wa maoni kuhusu utayarishaji wa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano, ni suala la wananchi wao wenyewe kusema na kuiambia serikali yao kipi wangelipenda kiwemo na kipi wangelipenda kisiwemo. Maelezo ya wananchi ndio yatatufanya sisi tuweze kuchukua hatua.

Kwa hivyo, ombi langu kwa wananchi kwa kupitia Baraza lako tukufu Mhe. Spika, ni kwamba unapokuja mchakato wa kuzungumzia masuala haya nawaombeni sana wananchi wote Wazanzibari tutoe maoni yetu kikamilifu ili tujue hasa serikali ijue nini wananchi wanahitaji katika suala la katiba mpya na tujue kwamba kwa utaratibu ambao upo Muungano huu ni wa nchi mbili; kwa hivyo, hata katika mazungumzo yetu na makubaliano ni kwamba lazima *two third* ya wananchi wa Zanzibar wakubali na *two third* ya wananchi wa Tanganyika wakubali.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Mhe. Spika, kwa sababu kifungu cha 132 cha Katiba ya Zanzibar kinatoa sharti la Miswada yote ya Sheria inayopitishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano na kutakiwa kutumika Zanzibar iletwe mbele ya Baraza la Wawakilishi, bilashaka kwa ajili ya kuidhinishwa. Je, waziri atalihakikishia Baraza hili kwamba mswada huu wa mchakato wa kuundwa kwa katiba mpya baada ya kukubaliwa na kutoa maoni yetu hatimaye ile *finally copy* utawasilishwa ndani ya Baraza kwa ajili ya wajumbe kutoa maoni.

(b) Katika majibu yake amesema serikali hii inatokana na wananchi na inawasilikiza wananchi, swali langu ni kwamba ikiwa wananchi wa Zanzibar katika mchakato huu wataona kwamba Muungano wenyewe umekuwa ni kero kwa Wazanzibari Serikali ya Zanzibar itaheshimu maamuzi hayo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwanza katika jibu langu mama nilisema kwamba hivi karibuni yale mazungumzo yote ambayo tumayafanya baina ya pande hizi mbili tutayaleta katika Baraza la Wawakilishi baada ya kuliarifu Baraza la Mapinduzi ili Wawakilishi watoe maoni yao na tuweze kuwaarifu. Kwa hivyo, hiyo ni hatua ya mwanzo ambayo kabla ya kutekeleza hicho kifungu cha 132.

Baada ya kukubaliana sote na mswada huu utakwenda Bungeni na itakuwa mswada ule tumeshaukubali sote Wazanzibari na upande wa Watanzania Bara.

Lakini kwa sababu kuna masharti ya kikatiba, lazima masharti hayo yatekelezwe kama ilivyo katiba.

La pili, ni kwamba alitaka kujua ikiwa wananchi wametoa maoni yao. Ni kama nilivyosema kuwa wananchi ndio wenye serikali. Lakini tujue tu, kwamba wananchi kwa upande mmoja na serikali kwa upande wa pili, maoni ya wananchi yataheshimiwa na serikali.

Lakini serikali pia ina jukumu kwa sababu ndio iliyowekwa na wananchi kuyatizama maoni yale ya wananchi na kuwashauri wananchi kwamba suala hili mlilolizungumza linaweza likawa na athari hii au halitokuwa na athari hii. Kwa hivyo, ninachotaka kusema ni kwamba maoni ya wananchi yataheshimiwa, lakini pia wananchi wajue kwamba serikali ina wajibu na wao wa kuwaeleza wananchi nini wanachohisi serikali.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa Mwaka 2011/2012

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tuna muda mchache wa kuendelea kuchukua michango na tunao wachangiaji wasiopungua wanane. Tutajitahidi tuone kwamba tuchangie kwa muda mchache bila ya kurudia rudia isipokuwa kwa kukazia tunaweza tukakazia, ili hatimae tumuombe Waziri atufanyie majumuisho.

Mhe. Salum Amour Mtondoo: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2011/2012. Mhe. Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili napenda kumpa pole Mhe. Waziri kwa kazi nzito aliyokuwa nayo.

Mhe. Spika, mimi nina machache tu kidogo. Kwanza ningependa kuchangia katika ukurasa wa 25 wa kitabu chake Mhe. Waziri. Hapa ameamua kuzisaidia *NGOs* ambazo zitashughulikia mazingira. Mhe. Spika, katika jimbo langu ninayo *NGOs* ambayo imeamua kuisaidia mazingira.

Mhe. Spika, kwanza napenda kuwashukuru Mamlaka ya Maji kwa kuruhusu kianzio cha maji cha Mwanyanya kiwe mikononi mwa wananchi. Kwa hivyo

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapofanya majumuisho tuone kwamba ataisaidia vipi jumuiya ile ili iweze kujikomboa.

Mhe. Spika, la pili nichangie uharibifu wa mazingira unaosababishwa na magari ya punda na ng'ombe. Mhe. Spika, jana mama yangu Mhe. Asha Bakari Makame aligusia kuhusu uharibifu uliofanywa Maruhubi. Maruhubi pale tuliachilia magari ya punda yalifanya kazi kwa kuchimba mchanga sasa pale pahala tunatia taka. Ina maana tumeruhusu uharibifu wa mazingira wa njia moja na sasa hivi tunaruhusu uharibifu wa mazingira wa njia ya pili. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri pale Maruhubi sasa pamekuwa pahala pa hatari kwa sababu wanafunzi wa Chuo cha Utalii Maruhubi, hoteli pamoja na wapita njia imekuwa kero. Mhe. Spika, naomba mazingira yale yatazamwe kwa jicho jengine.

Mhe. Spika, la tatu katika kitabu cha Mhe. Waziri nimeona kuna sehemu anategemea kukusanya shilingi milioni 9. Ningemuomba Mhe. Waziri kujua milioni 9 hizi si kusababisha kuharibu mazingira kwa njia nyengine baada ya kutoa vibali kwa uharibifu.

Mhe. Spika, naomba kuzungumzia madawa ya kulevya. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 28 amezungumzia madawa ya kulevya. Mhe. Spika, madawa ya kulevya ni tatizo sugu tulilonalo hivi sasa na linatusumbua. Lakini ningependa sana kugusia kuhusu hizi *Sober House* ambazo zimeanzishwa kurekebisha tabia za hawa vijana. Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Waziri kwamba *Sober House* hizi tuziangalie kwa sana.

Mhe. Spika, mimi katika jimbo langu la Bububu ilianzishwa hii *Sober House* tatizo ni kwamba watu wanakuja wanakodi nyumba tu katika maeneo ambayo wanaishi wananchi. Matatizo yake kama tunavyofahamu mtu wa dawa za kulevya hawezi kuacha mara moja kuna taratibu zinazotumika. Kwa hivyo, athari yake tayari baada ya kupunguza sasa tunaambukiza zaidi kwa watoto wetu ambao wanakwenda kuiga. Hawa vijana wanaranda mitaani imekuwa sasa hivi wana ushawishi mkubwa kwa hivyo tunaomba hizi *Sober House* ziwe nje ya maeneo wanayoishi jamii. Mhe. Spika, pia ningemuomba Mhe. Waziri angekuwa na uhusiano mkubwa na polisi jamii ili kurekebisha hizi tabia za vijana wetu.

Mhe. Spika, mwisho ningependa kuchangia suala ya Ukimwi. Mhe. Spika, ukimwi kwa kiasi kikubwa unasababishwa na mavazi. Mimi katika jimbo langu la Bububu nina Fuji pale na nyumba za kukodi nyingi ikifika saa tatu huwezi kukaa nje ukaangalia hali halisi ilivyo. Kwa hivyo Mhe. Spika, mavazi yanachangia kwa kiasi kikubwa maambukizi ya maradhi ya ukimwi. Mhe.

Spika, namuomba Mhe. Waziri katika mbinu moja ya kutatua tatizo la ukimwi vazi nalo tuliangalie kwa kina.

Mhe. Spika, kwa hayo machache kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Bububu naunga mkono hoja.

Mhe. Salim Nassor Ali: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2011/2012. Mhe. Spika, baada ya jana kupata taarifa kwamba nafasi ziliopo ni chache niliamua kuchangia kwa maandishi na tayari nimeshamkabidhi Mhe. Waziri. Kwa hivyo, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rahaleo naunga mkono hoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano na kuweza kuisoma hotuba hii kwa ufanisi na kwa ufasaha mkubwa.

Mhe. Spika, mimi niende kwenye Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa sababu imeguswa kidogo na nitoe maelezo kuhusu wizara yangu.

Mhe. Spika, nianze na suala la utalii. Mhe. Spika, kwa kweli utalii ni kitu kimojawapo ambacho kinatuletea mapato kwa taifa. Kwa kweli waheshimiwa wameuzungumzia utalii kwamba unaondosha mila na desturi kwenye nchi yetu. Mhe. Spika, naomba kwa kumsaidia Mhe. Waziri utalii si sababu ya kuondosha mila na desturi yetu kwa Zanzibar. Utalii ni pato la taifa na wanapokuja watalii huwa wanagusa maeneo mbali mbali yaliyopo kwenye visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Maeneo yenyewe ni kuona fukwe na kuweza kutembelea kwenye vianzio vyetu mbali mbali vya mapato kama vya kihistoria, mapango na mambo mengineyo.

Mhe. Spika, niende kwenye kivazi kwa kweli nalo hili linagusa kwenye wizara yetu. Mhe. Spika, naomba niwafahamishe Waheshimiwa Wajumbe kwamba mila na desturi tunaziondosha sisi wenyewe. Kama tutasimamia mila na desturi zetu za Kizanzibari kwa kweli tutafika pahala pazuri. Kivazi sicho kinachoendeleza ukimwi, bali ni mila yetu wenyewe kuiendeleza pamoja na hulka na desturi zetu za Kizanzibari kweli ukimwi utaondoka. Kwa sababu tunatakiwa tujihifadhi kwenye maungo yetu na tujihifadhi sehemu mbali mbali ambazo hazihitajiwi kuonekana. Kwa kweli hili nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi kama nyinyi ni *mas'ul* kwa wananchi muweze kusimamia kwa

kushirikiana na Mhe. Waziri wetu ili kumpa nguvu zaidi aweze kufanya kazi vizuri.

Mhe. Spika, pia niguse sehemu ya habari. Mhe. Spika, kwa kweli wizara yangu inajitahidi sana kushirikiana na walemavu na watu wenye virusi vya ukimwi ili kutoa taaluma mbali mbali kwenye vyombo vya habari.

Mhe. Spika, kwa kweli sina haja ya kutoa ufafanuzi mwingi kwa sababu mmenifahamu na nawaomba waheshimiwa wenzangu tushirikiane pamoja na waziri ili tumsaidie kazi tuweze kunufaika Wazanzibari sote kwa kuondokana na maradhi mbali mbali. Haya maradhi yaliyoletwa yameletwa na Mwenyezi Mungu kwa sababu ya maovu yetu mengi sana tunayoyafanya binadamu. Tujitahidi turudi kwa Mwenyezi Mungu na tutakaporudi kwake *inshaallah* atatupunguzia maradhi haya.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na kwa niaba ya wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba naipongeza hotuba hii mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi hii fupi ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2011/2012. Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati kwa ruhusa yako naomba nianze kwa haraka kama ifuatavyo.

Kwanza Mhe. Spika, tumeona katika kitabu hichi kwamba kulikuwa na mradi mkubwa wa kuua kunguru na kunguru laki tatu wameshauliwa. Kazi ya kuendeleza kuwaua kunguru hawa itaendelea baada ya kipindi hichi cha bajeti. Mhe. Spika, mimi swali langu ni kuwa hawa kunguru ni viumbe na ni lazima kuwepo kwao hapa duniani walikuwa wana kazi yenye maslahi kwetu sisi ikiwa ni pamoja na kusafisha mji na kadhalika.

Sasa kama kunguru wataondolewa wote kiasi hicho ni lazima kutakuwa na matatizo. Kwa hivyo, serikali inafanya mpango gani wa kuweka wanyama mbadala ambao hawatakuwa na kero kama kunguru baada ya kuondoka kunguru hawa.

La pili Mhe. Spika, kwa haraka haraka nizungumzie kuhusu madawa ya kulevya. Mhe. Spika, kisiwa chetu ambacho tunatangaza ni kisiwa cha amani, tunasema Zanzibar njema na atakae aje. Hichi kisiwa hivi sasa kinazungumzwa kwa kuingiza madawa ya kulevya kwa kiwango kikubwa. Ishara tosha ni kuwa tunapotembea hasa humu mijini tunawaona vijana wamelala hapa na pale ikiwa tayari wameshatumia madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, madawa ya kulevya yanatoka mbali na nasikia sina uhakika ni ghali sana na yanataka utaalam wa kweli kuweza kuyafikisha kutoka nchi hadi nchi bila ya kukamatwa. Mhe. Spika, jana mheshimiwa mmoja katika kuchangia alidhani tu kwa fikra kama nilizokuwa ninazo mimi kuwa lazima kuna watu wazito ndio wanaoweza kuifanya biashara hii, lakini kwa sababu ya utaratibu unavyosema una uhakika ikabidi aondoshe kauli yake.

Mhe. Spika, niiulize swali serikali. Kwa sababu madawa ya kulevya ni kitu kibaya sana na tunazungumzwa vibaya Wazanzibari na suala na kupambana na madawa ya kulevya halijaanza leo. Mhe. Spika, niiombe serikali kwa kuwa ina vyombo vya uchunguzi, maaskari na kadhalika kupambana na suala hili. Wamepata taarifa gani katika uchunguzi wao kuhusu hawa wanaoleta madawa ya kulevya. Ni vipi hasa hatua zifuatazo zifanywe kuona kuwa tatizo hili limeondoka ili kuondoa ile fikra tuliyonayo kwamba wanaofanya ni watu wazito na wenye uwezo wa kuingiza madawa haya.

Mhe. Spika, la tatu ni suala la Ukimwi. Mhe. Spika, Zanzibar tunaijua ni nchi yenye mila, desturi na silka nzuri tu. Asilimia kubwa sana ya Wazanzibari ni waislam *Alhamdullillah* wanajua athari za ukimwi kutokana na hiyo sababu ukimwi unapatikana kwa wingi.

Visiwa vyetu kama visiwa vyengine vya dunia wanaingia watu kutoka nchi mbali mbali, hawaingii kwa sababu ya maisha tu lakini kwa mazingira tunajua wanakuja pamoja na sababu nyengine. Kupambana na ukimwi ni kupambana na kutokuwepo viashiria vya ukimwi. Hali ya watu wetu tunaiona hasa hawa wanaotoka nje ya Zanzibar na kuna wengine hawana kazi ya kufanya, kuna wengine wanashinda mabaa na wengine tunajua hata hapa Zanzibar kuna maeneo huwezi kutembea. Hiyo ndio njia yao ya kuwapatia maisha.

Mhe. Spika, tunapambana na ukimwi lakini viashiria vya ukimwi vinaingia kila wakati. Kwa maana hiyo, kwa sababu maradhi haya hayatibiki itakuwa siku zote ni kupoteza mapesa lakini siku zote na watu wetu wakiathirika na wakishakupata ndio moja kwa moja hawezi kutibika akapona. Mhe. Spika, naiomba serikali inisaidie kwa sababu hili ni suala kubwa sana na ni lazima liepukike na baadhi ya viashiria tunavijua na serikali inaweza kufanya marekebisho angalau hali ikapungua. Kwa safari hii nguvu tunayokwenda serikali ina mpango gani hasa wa kupambana na maradhi ya ukimwi kwa viashiria vinavyoingia zaidi kuliko vile tunavyokwenda hivi sasa kuwachukua watu kuwapa dawa za kuongeza maisha na kadhalika.

Mhe. Spika, jengine kwa ufupi ni suala la mazingira. Mhe. Spika, mazingira yetu yanachafuliwa sana na Zanzibar ni nchi ndogo sana. Kuna ukataji wa miti ovyo, kuna uchukuaji wa mchanga, kuna uvunjaji wa mawe, kuna ukataji wa

ardhi kwa sababu ya matofali, kuna uharibifu wa mazingira ya baharini na kadhalika, yote haya yanafanywa na binadamu mwenyewe. Kuna mengine ni ya kuchafua mazingira na kuna mengine ni hatari zaidi kwa sababu yakiendelea na wakati yakishatokea pale pahala si rahisi kurekebishika kwa hivyo hali itakuwa mbaya sana hapo baadae.

Sasa katika shughuli za maendeleo Mhe. Spika, kuna wakati mwengine hulazimika hata serikali kushiriki katika suala zima la uharibifu wa mazingira lakini hakuna chombo cha kutuchukulia hatua. Kwa sababu ya maendeleo sisi wenyewe tunaomba angalau tusaidiwe ili maendeleo yapatikane.
Kwa mfano Mhe. Spika, tuna utengenezaji wa barabara, unajua barabara ikisha kutengenezwa kinachukuliwa kifusi kingi sana tu na nchi yetu sasa ina mashimo makubwa sana ya kifusi cha kutengenezea barabara. Miamba inakatwa tunafanya kokoto ardhi inazidi kupungua na kisiwa ni kidogo na watu wanaongezeka bila ya mpango maalum. Kwa hivyo, naomba kila wizara kwa pale ambapo wanaona wanaweza kuisaidia wizara hii katika kupunguza uharibifu wa mazingira ifanye hivyo.

Mhe. Spika, juzi kama unakumbuka Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano alitoa maelekezo mazuri sana aliposema kwamba jiwe liliopo Zanzibar halifai kutengenezea barabara kwa hivyo atachukua kokoto na kadhalika kutoka Tanga. Mimi ningeliomba ajipange katika hali hiyo kwa kusaidia kutokuharibika mazingira kifusi na mawe yasichimbwe tena. Katika haya maendeleo tunayoyapata ya barabara Mhe. Waziri ajitahidi hizo kokoto na kadhalika zitoke huko nje ya nchi. Vyenginevyo tutakuwa sisi tunamkamata mwananchi lakini serikali inachukua juhudi ya kutosha katika kufanya hivyo kwa sababu ya maendeleo.

Mhe. Spika, jengine kuna mambo ya ukataji miti ovyo hii ni hatari katika sekta yenyewe kwa sababu ya wakati sipendi kueleza. Hii Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ina majukumu mazito ya kitaifa. Nahisi ikiwa ni maliasili imo katika wizara ya Kilimo na Maliasili. Utaratibu uliopo hivi sasa kunakuwa na ukataji wa miti ovyo kwa sheha tu kutoa kibali kuwa huu mti unaweza ukakatwa na ruhusa inatoka.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri aweke mikakati ya hali ya juu dunia hivi sasa wako katika mpango wa kupanda miti kwa wingi sana na tunaona katika vyombo vya habari sisi badala yake tunaikata kwa wingi sana. Tufanye mpango miti isipungue ovyo na upandaji wa miti uwe mkubwa ili tuweze kuyamudu mazingira yetu.

Mhe. Spika, nilikuwa na mengi lakini kwa kuheshimu wakati wako na heshima uliyonipa ya lala salama nashukuru nimalizie hapo.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2011/2012. Mhe. Spika, awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu *Subhanahu Wataala* aliyetujaalia uhai tukawepo humu ndani asubuhi hii kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Spika, pia sina budi nikushukuru na wewe kunipatia nami nafasi hii ya kutoa mchango wangu mdogo kabisa katika Wizara hii iliopo mbele yetu sasa hivi. Mhe. Spika, mimi kwa kweli mchango wangu utakuwa mdogo sana kwani mengi yameshasemwa. Hivyo nianze moja kwa moja na mchango wangu katika ukurasa wa 22 kifungu cha 51 Afisi Kuu Pemba, malengo kwa mwaka 2011/2012 naomba kunukuu: Anasema "Kuimarisha mazingira ya utendaji wa kazi na kujenga uwezo wa wafanyakazi."

Mhe. Spika, hii ni hatua muhimu ambayo ndio itakayoweza kutekelezeka yale majukumu ambayo yamepangwa kufanyika katika kipindi hichi. Bila ya kulifanya hilo haiwezekani kabisa, kwani wafanyakazi lazima wawe katika mazingira yaliyotayarishwa rasmi kuweza kukabiliana na lolote lile katika kitengo chao.

Mhe. Spika, niende kwa ufupi niingie ukurasa wa 23 kifungu cha 53 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuja hapa alieleza kwa ufasaha na upana mkubwa mno na tulimuelewa vya kutosha. Lakini baada ya kuangalia jinsi ya utekelezaji wa jukumu hili la kiutafiti limeonesha kwamba fungu ambalo limepangwa kwa ajili ya kutumika kitengo hichi cha idara hii ni dogo mno. Mhe. Spika, shilingi milioni 15 kwenye utafiti sidhani kama linaweza likakidhi haja na kuweza kutekelezeka tafiti ambalo ndio jambo muhimu litakaloweza kuchimbua utekelezaji wa mpango huu.

Mhe. Spika, hivyo basi, nahisi kwenye fungu hili ni lazima liongezewe fedha ili waweze kukidhi matakwa ya utendaji wa shughuli hii muhimu kwa Wazanzibari.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango niende ukurasa wa 25 Idara ya Mazingira. Mhe. Spika, hapa ndipo penye kilio cha taifa, uharibifu wa mazingira hapa kwetu Zanzibar umekithiri hali ambayo imeiondolea hadhi Zanzibar katika utaratibu mzima hata wa wawekezaji wetu ambao ndio tegemeo la uchumi wa taifa hili.

Mhe. Spika, mimi binafsi katika Wilaya yangu ya Kaskazini "B" nimeathirika mno kwa uchimbaji wa mchanga hali ambayo imekuwa ni hatarishi mno sasa hivi hata kwa shughuli za kilimo. Hivyo basi, hali hii ambayo imejitokeza haina

budi tushirikiane kwa pamoja na sheria itayarishwe kwa ajili ya udhibiti wa uchimbaji holela wa mashimo ya mchanga.

Mhe. Spika, nina mashaka Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili alikuwepo katoka lakini nimwambie kwamba anajiandaa na kuleta mapinduzi ya kilimo lakini nina mashaka makubwa katika Wilaya ya Kaskazini "B" kwa athari ilivyojitokeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri anasema anataka kuwakomboa wananchi kiuchumi na hawawezi kukomboka bila ya kutumia ardhi na ardhi sasa imeshakuwa lemavu. Hivyo basi, nina mashaka makubwa wananchi wa wilaya yangu kuweza kufaidika na mpango huu kwa upana mkubwa na ufanisi. Ardhi imejaa mashimo, ardhi imekuwa haina tena mbolea, ardhi hiyo haiwezi kabisa kutumika kwa shughuli za kilimo, inahitaji marekebisho ya kina.

Mhe. Spika, naiomba wizara itumie sheria na utaratibu maalum wa uchimbaji wa mchanga, bila ya hivyo tutashtukia ardhi zetu zimetuondoka na ile hali ambayo dhana yetu inatulenga kwamba tuondokane na umaskini kwa wananchi kwa kuitumia ardhi yetu basi linawezekana likashindikana.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, niingie tena katika sehemu ile ambapo wananchi wetu wanatumia ardhi zao hususan kisiwani Pemba kwa kufanya matofali ya mawe na kuchimba. Mhe. Spika, ni lazima wananchi watafutiwe miradi mbadala ili waweze kuondokana na hii hali ya kuchimba huko kwa ajili ya kujipatia riziki. Lakini haya hayawezi kuondoka ni lazima wapewe kwanza taaluma waelewe kwamba kufanya hivyo ni athari. Pia serikali itafute mbinu na utaratibu maalum watengewe miradi maalum ili kuepukana na hali ile na kuinusuru ardhi hii na hali ya kutokuwepo kwake au kutokutumika kwake kwa ufanisi na uzuri zaidi.

Mhe. Spika, sasa nizungumzie Idara ya Watu wenye Ulemavu. Mhe. Spika, hapa nitasema kidogo tu kwa sababu jana waheshimiwa walizungumzia vya kutosha. Lakini na mimi niungane na waliotangulia kusema kwamba kwa masikitiko makubwa maofisi mengi kwa sasa hivi hayajengwi katika ujenzi ambao unaonesha ndugu zetu nao waweze kutembea au kuingia katika maofisi hayo kwa wepesi bila ya usumbufu.

Mhe. Spika, mfano hai ni jengo letu hili ambalo tumejenga sehemu ya mkahawa ambao umetunadi juzi tu lakini Mhe. Raya Suleiman Hamad hawezi kwenda kupata chai ambayo umeitangaza. Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa naomba kupitia wizara tuangalie sana ujenzi utakaofanyika katika ofisi zetu kuwafikiria ndugu zetu kwani hawa ni miongoni mwetu na wanahitaji maendeleo na kupata fursa sawa katika nchi yao.

Mhe. Spika, sasa niende katika sehemu ile ambayo wengi wao waliizungumza kwa kina kabisa ya madawa ya kulevya. Mhe. Spika, rasilimali watu inatutoka, nguvu kazi ya taifa ni vijana wanatuondoka, vijana wazuri wenye uwezo mzuri wengine tulikwishawasomesha lakini madawa ya kulevya yanawaathiri. Wapo katika hali ngumu wanatusababishia sisi tulio wazima kufanya kazi kwa bidii na kwa ugumu kabisa ili kuweza kuwakidhia wao matakwa yao, jambo ambalo kama wasingekuwa hivi hawa wangekuwa ni wazalishaji wakubwa na wapiganaji wakubwa katika shughuli za maendeleo ya taifa hili.

Hivyo basi Mhe. Spika, naiomba serikali kupitia wizara hii niseme kwamba kwa upande wao hawatoweza kabisa kulitokomeza balaa hili. Ni lazima tushirikiane sote kwa pamoja katika wizara tofauti na jamii kwa pamoja kwa ajili ya kuweza kuondoa hali hii. Askari anahusika kwa upande wake, mpelelezi anahusika, mtu wa kawaida anahusika na sote tushirikiane ndipo tuweze kuona kwamba hayaingizwi madawa haya. Tukisema kwmaba tunaiwachia wizara hii peke yake basi nasema kwamba halitowezekana. “Kidole kimoja hakivunji chawa”, kushirikiana ndiko kutatuletea mabadiliko ya kweli na kuweza kuzuia uingizaji huu wa madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini kwamba tunawafahamu vizuri waletaji, kwa sababu unga haupitii angani tu usiteremke *airport*, unapita huko, kama haukupita huko basi unapita bandarini. Tuna vikosi vyetu mbali mbali tuwaombe kwa huruma na mapenzi, waliombee huruma taifa lao, kwa sababu wao wanaofanyakazi nao ni wakaazi wa taifa hili na wana haki ya kuweza na wao kulinda maslahi ya Wazanzibari wenzao. Kwa hivyo, tushirikiane kwa pamoja kwa kupitia wizara yetu hii kwa ajili ya kuondoa janga hili, hili ni janga la taifa. Maendeleo tutayasikia harufu kwani tutakuwa tunawaangamiza vijana wetu siku hadi siku na hao ndio nguvu kazi ya taifa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, sasa nije kwenye hii Tume ya Ukimwi, hili janga la taifa. Mhe. Spika hapa nasema kidogo kwamba

Mhe. Spika: Jitahidi hilo liwe la mwisho.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika. Ukimwi ni janga lakini tujiulize na sisi wenyewe kila nchi ina mila na silka, utaratibu na utamaduni wake. Je, sisi Wazanzibari haya yaliopo leo ndio utamaduni wetu. Je, haya ndio tuliyoridhishwa sisi na mabibi na mababu wa Zanzibar. Mimi nasema sivyo.

Tumeridhi Zanzibar nzuri, iliyojaa heshima, nidhamu na watu wazima kabisa wenye uwezo wa kulitumikia taifa hili. Tuna nini sisi leo mpaka tumefika hapa. Nasema mila silka na utaratibu wa Zanzibar na utamaduni wake tumeupoteza. Tumeingia kwenye vivazi mambo sio yetu, vijana wa Kizanzibari wameleta

wigo wa nje na kufanya ndio utamaduni wa Zanzibar jambo ambalo halikuwepo. Kwetu sisi tulizowea wanaume kuvaa kanzu na kofia, utamaduni halisia wa Uzanzibari na wanawake kuvaa nguo ambazo zinastahiki kuvaliwa. Leo ni ajabu Zanzibar ukitembea huwezi kumtofautisha Mzanzibari na yule mgeni aliyekuja Zanzibar. Inawezekana mgeni akavaa vizuri kuliko Mzanzibari. Kwa mujibu na utaratibu wa mila na silka za Uzanzibari tumepoteza mwelekeo, turudi.

Nashauri katika wizara hii Mhe. Waziri kwa hapa huna budi kila mmoja na wengi kwa bahati nzuri ni Waislamu. Turudi kuwatumia mashehe katika vijiji vyetu, miji yetu, maeneo yetu. Tutumie jumuiya za Kiislamu kuweza kutoa taaluma kwani Mwenye Mungu anasema wacha kufanya, "la takrabu zinaa", tuwache kabisa tusiikaribie zinaa, hili ndilo jambo kubwa ambalo linasababisha kwa kasi kubwa uwambukizo wa ukimwi tofauti na kutogwa sindano ama kufanya jambo jengine, hii ni kwa asilimia kubwa kabisa.

Kwa hivyo, tuwatumie mashehe wetu, tuwatumie watu wa dini ili kuweza kutoa taaluma rasmi kwa huruma na mapenzi tangu vijijini, katika miji katika sehemu tofauti, katika mihadhara mbali mbali ya Kiislamu, wawaoneshe na waone kabisa kwamba hali hii haikuja bure bali wamebadilisha utaratibu na yale ambayo wameteremshiwa na Mola wao.

Naamini kwamba yakifanywa haya na serikali ikazingatia utaratibu wa shughuli zile za starehe kufungwa yale mambo ya mabaa, hapa kwetu hayakuwepo sana. Lakini leo yameenea na imekuwa ni mambo ya kawaida, mambo ambayo mila na silka za Kizanzibari basi tulikuwa hatumjui hata mlevi sisi wakati tunalelewa zama hizo. Ukimuuna mlevi unamstaajabu na unamkimbia, leo wakati wa kufanya kazi basi wenzetu wamekunywa pombe mchana, maendeleo hayo yatakujaje, ukimwi huo vipi usije na matamanio yanakuja kwa sababu watu hawavai nguo.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Namuomba Mhe. Waziri tushirikiane kwa pamoja Wazanzibari sote ili lituondoke janga hili na hili ni jinamizi la kuondoa maendeleo yetu. Tutajikaza na tutapanga bajeti nyingi lakini hazitotekelezeka, kwa sababu wananchi wake wameathirika ama ukimwi au madawa ya kulevya. Je, hao watakaotumika kwa ajili ya kufanya kazi hizo ni kina nana. Mhe. Spika, naliwacha swali hilo uwanjani ili Wazanzibari tulijadili huku nikiunga mkono hoja kwa asilimia mia.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, awali ya yote nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijaalia kusimama hapa nikiwa mzima wa afya njema.

Pia nichukuwe nafasi hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niwe mmoja wapo wa wachangiaji katika wizara hii ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, pia nichukuwe nafasi hii kwa dhati kabisa nimpongeze Mhe. Waziri wetu Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Pia nimpongeze zaidi kwa namna ya ufanyaji kazi wake mzuri. Naamini kwamba wanawake tukiwezeshwa tunaweza. Vile vile nichukuwe nafasi hii kwa dhati kabisa kumuomba Mhe. Rais pale ambapo anapata fursa ya uteuzi, basi wanawake atuangalie zaidi, kwa sababu wanawake tunapopatiwa nafasi kwa kweli tunaweza.

Mhe. Spika, nichukuwe nafasi hii niipongeze serikali kwa kuweka Ofisi hii ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuwa miongoni mwa ofisi ambazo zinashughulikia majukumu muhimu ya ukimwi, madawa ya kulevya na mazingira. Idara hizi nimuhimu sana kwa taifa letu. Lakini pia idara hizi zinapaswa kuwekewa wizara maalum ili zipate nafasi ya kushughulikia ipasavyo.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo basi mimi mchango wangu hautokuwa mrefu sana kutokana na muda ulionipatia. Naomba niingie katika kitabu hiki nianze moja kwa moja katika ukurasa wa 8 katika Idara yetu hii ya Mazingira.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wengi waliosimama walizungumza suala la mazingira na hapa kwetu Zanzibar kwa kweli tuna tatizo kubwa la uharibifu wa mazingira. Moja ya tatizo ambalo linapelekea uharibifu wa mazingira ni suala la uchimbaji michanga Mhe. Spika.

Mhe. Spika, suala la uchimbaji michanga katika maeneo mbali mbali linapelekea uharibifu mkubwa wa uchimbaji mchanga katika maeneo yetu mbali mbali ya mjini na vijijini. Mhe. Spika, kwa mfano maeneo ya Mwembemakumbi, sasa hivi maeneo haya yamefurika mashimo kutokana na uchimbaji michanga. Lakini ukenda katika maeneo ya Nyerere, kama tutafanya ziara sisi Waheshimiwa Wajumbe wako kwa kweli tunaweza tukakosa njia za kupita kutokana na mashimo mengi ambayo yapo katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, ukija katika maeneo ya Mwanakwerekwe. Mhe. Spika, sasa hivi mpaka makaburi yanachimbwa kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira yetu. Mhe. Spika, zamani zilikuwepo kamati ambazo zinasimamia uchimbaji wa mchanga. Hata ukiangalia gari zile zinazochukua michanga hazifuati utaratibu na sheria za kutumia shimo moja mpaka limalizike ndipo waingie jengine.

Sasa hivi magari yanayochukua michango wanapojisikia kuchimba shimo hili wanachimba, kabla halijamalizika shimo hili wanaingia jengine. Hii inapelekea kuwa na mashimo mengi katika maeneo yetu ya mashamba. Si hilo tu Mhe. Spika, kamati ambazo zinasimamia uchimbaji wa mchanga hapo zamani ilikuwa mtu anapokuwa na eneo lake lazima aandike barua kwa kamati ile. Lakini kamati ile inatoa ruhusa kwa mtu mmoja hadi shimo lake limalizike ndipo apewe ruhusa au kibali cha mtu mwengine ili kuchimbiwa shimo lake. Sasa hivi hakuna hivyo. Naamini kwamba kamati labda niseme kuwahazisimamii ipasavyo kudhibiti uchimbaji wa mchanga.

Mhe. Spika, naomba kupitia wizara hii ihakikishe kwamba zile kamati ambazo zilikuwa zinasimamia kuchimbwa mchanga ziendelee kuanya kazi zake ipasavyo, lakini pia ziendelee kufanya kazi kwa uwadilifu mkubwa katika kuhakikisha kwamba mazingira ya mji wetu hayaharibiki kutokana na uchimbaji wa mchanga.

Mhe. Spika, nikiendelea nije katika suala zima la maradhi ya ukimwi. Janga hili la maradhi ya ukimwi kwa kweli ni janga la kitaifa, sio janga la mtu mmoja. Mimi naipongeza serikali hapo mwanzo ilikuwa ukifungua vyombo vya habari unasikia namna gani serikali inavyohamasisha kujikinga na maradhi haya ya ukimwi. Sasa hivi ile kasi ya mwanzo imepungua. Naomba basi wizara yako iendelee kutumia vyombo vyetu vya habari kuhakikisha kwamba wananchi wanaelimishwa kuhusu suala zima la kujikinga na ukimwi.

Mhe. Spika, bado wananchi wetu wako nyuma katika kuhakikisha kuwa wanapima ili kujua afya zao. Wananchi wetu bado wana uwoga, wana hofu na wanahisi watakapokwenda kupima atakapoonekana na maradhi haya basi anajihisi kuwa atakuwa keshakata tamaa au keshakuwa hayuko duniani tena. Kwa hivyo, naomba nichukuwe nafasi hii kwa kupitia kwako Mhe. Spika, nimuomba waziri ahakikishe kwamba bado ipo haja kwa serikali kuhamasisha wananchi wetu ili kupima masuala ya ukimwi.

Suala hili la upimaji Mhe. Spika, kwa mfano sisi Waheshimiwa Wajumbe ambao tunawawakilisha wananchi basi tuanzie kwetu. Kwa kupitia kwako Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri wa Afya watuletee madaktari ili tuoneshe mfano bora, kuwa sisi Waheshimiwa Wajumbe tunaanza kupima afya zetu.

Mhe. Spika, kama itawezekana basi nimuombe Mhe. Waziri kabla hatujamaliza bajeti hii, waje madaktari ili watupime afya zetu, tujijuwe kama wazima au tunaumwa na kama tunaumwa tuanze kutumia dawa mara moja.

Mhe. Spika, kipindi kilichopita, walipelekwa madaktari katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano. Waheshimiwa Walichangia wakasema, jamani Mhe.

Waziri wa Afya tuletee madaktari ili tupime na tuzijuwe afya zetu. Mhe. Waziri wa Afya wa Jamhuri ya Muungano alipeleka madaktari. Lakini baada ya matokeo yale kwa kweli mwisho wa Bunge letu lile la Jamhuri ya Muungano, walipohamasishwa Waheshimiwa Wabunge wakapime afya, basi wale madaktari walikuta ni Waheshimiwa Wabunge kama kumi tu ndio waliopima, wengine wote walitokea kwa milango ya pembeni. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Spika, katika Baraza letu hili tukufu la Uwakilishi, yasije yakatokea yale ambayo yametokea katika Bunge letu. Waheshimiwa Wawakilishi, sisi ndio wa kuonesha mfano bora kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo basi niingie katika suala la madawa ya kulevya. Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, wengi wamezungumzia suala la madawa ya kulevya. Mimi bajeti iliyopita ya Mhe. Waziri Kiongozi nilichangia suala zima la madawa ya kulevya. Mhe. Spika, usituchoke wajumbe wako ukitusikia tunapiga kelele katika suala hili la madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, madawa ya kulevya yanatuumiza, sisi kina mama ndio wazazi na kina baba ndio wazazi. Kwa hivyo, tunapoona watoto wetu wanaathirika na madawa ya kulevya jambo hili linatuuma sana. Nakuomba Mhe. Spika, kupitia kwako, Mhe. Waziri wa Makamo wa Kwanza wa Rais nawaomba muhakikisha kwamba tunawanasua vijana wetu na janga hili.

Vijana ndio taifa letu, vijana ndio tunawategemea na tukiwa na vijana wote ambao wamefikia kuwa wote wanakula madawa ya kulevya, kwa kweli taifa hili halitokuwa taifa. Nakuomba Mhe. Waziri ujipige kifua na uhakikishe kwamba kipindi hiki cha miaka mitano useme kweli nimefanya jambo, wananchi watakukumbuka kwa suala hili kwa sababu linatugusa sote.

Mhe. Spika, umenipa dakika chache na kwa vile Mhe. Waziri anatakiwa afanye majumuisho hivi asubuhi. Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi, nachukua nafasi kuiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia juu ya mia, ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Amina Iddi. Kampeni ya kupima nitaongoza mimi. *(Makofi).*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Naibu, kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais. Vile vile nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima kuweza kufika hapa na kuchangia bajeti hii.

Kwanza nitaanza kuchangia katika ukurasa wa 12 kuhusu madawa ya kulevya. Mhe. Spika, vijana wengi wameshapata athari ya madawa ya kulevya, vijana

hao walioathirika wanatunzwa na NGOs ili kupatiwa uzima kwa hali zao. Lakini haitoshi, kuchangiwa na NGOs haisaidii kitu. Ni bora serikali iweze kuchangia fedha maalum ili kuwapatia vijana hao, kupatiwa chakula na kupatiwa malazi ili hizi ziwe ndio uzima wao, bila hivyo hawawezi kupata uzima wa kuweza kujali hali zao.

Mhe. Spika, hivi sasa vijana wetu ambao wameathirika kwa madawa ya kulevya hawana makazi maalum, utakuta tunawakodia nyumba karibu na maeneo ya wananchi wengine. Mimi mwenyewe nimeshajionea mwenyewe. Nilikwenda katika *NGOs* ya Bububu pale kuwaone jinsi wagonjwa wetu wa maradhi ya madawa ya kulevya.

Kwa kweli hali zao ni mbaya sana, hawana uwezo hata wa kuzungumza, hawana uwezo hata pa kukaa. Ni afadhali serikali ijikite kuweza kuwaondoa katika maeneo hayo waliyo hivi sasa na wajengewe nje ya mji hasa katika maeneo ya nje ya bahari kama vile Nungwi au pengine popote. Kwa sababu kukaa katika maeneo ya watu ni hali halisi kwamba kuwapa nafasi na vijana wengine kuweza kupata maradhi ya madawa hayo, wanarushiana katika mitaa na wanaendelea kula madawa hayo.

Vile vile madawa hayo ya kulevya wahusika sio hasa wale walaji wa madawa hayo. Kwa hivi sasa ni afadhali tutupie macho kwa wale waletaji wa madawa hayo, ndio wahusika wakubwa wa kuweza kupata hatia na sio walaji. Badala ya kuwakamata walaji ni afadhali serikali itupie macho kwa waletaji madawa hayo ili wao ndio wapate nafasi kubwa ya kukamatwa na serikali na kupewa adhabu kali. Adhabu zao ni lazima kwanza waweze kufikia adhabu ya kufungwa si chini ya miaka 20 au adhabu ya kuweza kulipa fidia kuanzia Shs. 20 milioni na kuendelea, huo ni mchango zaidi wa madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, nikiwaangalia vijana wetu au wazee ambao ni walemavu. Hivi sasa walemavu ni wengi na ni wa kila aina. Kuna walemavu wa akili na walemavu wa viungo. Lakini utaona serikali yetu bado haijatupia macho kuweza kuwatunza kisahihi walemavu kwa hapa Zanzibar. Walemavu wanataka kutunzwa kama nchi nyengine yoyote duniani. Walemavu wanahitaji kupatiwa nyumba za kisasa ili watunzwe kama wanavyotunzwa wazee ama watoto yatima, hapo ndio tutakuwa tumewajali walemavu na tumewachangia kama vile watu ambao wako huru katika nchi yao.

Mhe. Spika, walemavu wapo mashamba. Mimi mwenyewe Mhe. Spika, katika jimbo langu kuna walemavu ambao hivi sasa haijui Zanzibar ikoje. Tangu amezaliwa ana umri wa miaka 20 mzee wake anamficha ndani, hatuki nje wala watu hawamjui. Ukiuliza nyumba ile kuna mlemavu utaambiwa nyumba ile

hakuna mlemavu. Isipokuwa mtu anayekaa mtaa mmoja na yeye ndiye atakuambia yumo mlemavu.

Kwa hivyo, ipo haja kwa walemavu kuweza kuwanunulia gari la kisasa na likaweza kupita katika mikoa yote kuwatembeza katika mji wa Zanzibar na kuwaonesha mahoteli ya kisasa au kuona hali ya Zanzibar ikoje na wao ikawa tumewatunza na tumewajali.

Mhe. Spika, niende kwenye kifungu cha 16 inayohusu matatizo ya ukimwi. Matatizo ya ukimwi ni janga la dunia hivi sasa. Wengi tunaozungumzia ukimwi, tunazungumzia jinsi gani tuvae nguo, jinsi gani tujitibu. Mimi naona kwamba kivazi peke yake hakitoshi kuondoa ukimwi, isipokuwa tuwe na kamati maalum ya waganga wa asili kutafuta tiba kama wanavyotafuta wazungu kupata dawa za kutibu ukimwi na sio kulia tu kwenye kivazi, kivazi hakitotusaidia kuondoa ukimwi.

Kama tutakuwa na waganga wa jadi na waganga wa kiasili tukikaa kama kamati maalum na wakatunzwa na serikali hapo ndipo tutakapoweza kupata dawa ya ukimwi na tukaweza kuondoa ukimwi hasa hapa kwetu Zanzibar, kwa sababu dawa za asili zipo na zinaaminika.

Mhe. Spika, huo ndio mchango wangu kuwa tujitahidi kutafuta madawa na sio kutafuta kivazi kinachoweza kuondoa ukimwi, ukimwi hauondoki kwa kivazi. Ahsante Mhe. Spika, kwa mchango wangu huo kwa leo. Kwa hayo machache mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani tunaunga mkono kwa asilimia mia kwa mia ili bajeti hii ipitishwe bila ya matatizo, ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Awali ya yote kwanza Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa pumzi ya uzima na afya, nikaweza kufika leo kwenye Baraza lako hili. Pia nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa ya kuchangia.

Mhe. Spika, kwanza naomba kuunga mkono hoja ya hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kwa niaba ya wanawake wa Wilaya wa Magharibi ambao wamenileta hapa ili niwawakilishe. Pia kwa niaba ya Wizara yangu ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, mengi yamezungumzwa hapa kutoka jana wakati bajeti hii ilipowasilishwa. Mimi yangu yatakuwa ni machache katika zile sehemu ambazo niliguswa katika Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, wajumbe wako wa Baraza hili tukufu, hususan Mhe. Raya hapa, jana alizungumza sana kuhusu suala la watoto walemavu na namna ambavyo

wanahitaji mazingira maalum ya kupatiwa elimu. Nakubaliana naye Mhe. Spika, kwa kusema ni kweli na serikali suala hili imeliona na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imeanzisha maskuli mbali mbali ya kuhakikisha kama watoto wetu hawa wanapata elimu Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, yale ambayo aliyoyazungumza Mhe. Mjumbe wako Mhe. Raya, kuwa walemavu ambao wana athari ya akili, walemavu wa akili tunawaita. Mhe Spika, tuna skuli kwa Unguja na Pemba, kwa Unguja ni Skuli ya Kisiwandui, Jang'ombe, Mwembemakumbi na Mwanakwerekwe E. Kwa Pemba tunazo Skuli ya Michakaeni na Pandani.

Vile vile kwa walemavu wa macho yaani wasioona, tunayo madarasa Skuli ya Kisiwandui pale darasa pekee, pia na Haile Sellasie kwa Sekondari. Katika skuli zetu takriban nyingi tuna madarasa ambayo tunayaita ni madarasa mjumuisho. Madarasa haya hujumuisha watoto wetu ambao sio walemavu na wale watoto ambao wana ulemavu wa aina moja au nyengine.

Kwa kweli Mhe. Spika, mimi binafsi pamoja na waziri wangu tulifanya ziara baada ya kupata uteuzi wetu na tuliona ni namna gani watoto hawa wanavyofanya kazi na wenzao wakiwemo madarasani. Sio wanafunzi tu, lakini tunao na walimu ambao ni walemavu wako katika madarasa yetu haya, hususan Skuli ya Kisiwandui.

Kwa hivyo, ninachotaka kuomba zaidi hapa ni wazazi kuwatoa watoto majumbani na kuwapeleka katika madarasa yetu haya. Elimu hii ambayo wataipata naamini itawasaidia wao pamoja na nchi kwa jumla.

Jengine ni suala la kulipa, watoto hawa ambao wana ulemavu ni kwa nini walipishwe. Mhe. Spika, kwenye jibu langu la swali nambari 84 juzi, nilizungumza kuhusu malipo ambayo yanatolewa ya mwaka kwa wanafunzi wetu. Nilizungumza kwamba sio ruhusa kwa wale watoto ambao wana mazingira magumu, kutoleshwa malipo yoyote na tumetoa toleo maalum kupeleka maskulini kwetu. Sasa Mhe. Spika, inawezekana yale aliyoyasema Mhe. Raya Suleiman Hamad inawezekana kweli yanafanyika, kwa sababu tuna-*deal* nao ni binadamu na binadamu anayo mazuri na mabaya ndio maana tunaambiwa tukumbushane.

Kwa hivyo, nataka nichukue fursa hii adhimu Mhe. Spika, kuwakumbusha Walimu wetu Wakuu pamoja na zile Kamati ya Skuli, ambao ndio wanaosimamia michango hii. Kwa maana hiyo, si ruhusa kwa mtoto yeyote mlemavu Mhe. Spika, kutoleshwa mchango wowote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunaondoa malipo haya, ili kumpa mzazi motisha ya kuhakikisha mtoto huyu anampeleka skuli na badaya ya mazingira yale ya kumshughulikia kuhakikisha kuwa anakwenda skuli, basi tusimpe na mzigo mwengine ambao unahitaji malipo. Hivyo, nawaomba Walimu Wakuu washirikiane na Kamati za Skuli, mara nyingi Kamati hizi za Skuli wanaokuwa Wenyeviti ni Masheha wetu, ambao wanajua kuwa nyumba hii na ile ina mtoto gani. Kwa maana hiyo, Masheha wetu watusaidie, ili kuhakikisha kama watoto hawa wanapata elimu bure bila ya kulipia. *(Makofi)*

Nakushukuru sana Mhe. Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tumalizie kwa kumsikiliza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Vile vile niwaombe radhi Mhe. Saleh Nassor Juma pamoja na Mhe. Salma Mohammed Ali kwa bahati mbaya walipoitwa walikuwa hawapo na muda wetu umekwenda sana. Kwa hivyo, niwaombe radhi kwamba hawatopata nafasi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nikushukuru sana na mimi kupata muda huu mchache kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Awali ya yote na mimi niungane na wenzangu kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba hii na hasa alivyozungumza kwa uwazi kabisa haya mambo makubwa matatu, ambayo tunasema ni *cross cutting issues*, suala la UKIMWI, Madawa ya Kulevya pamoja na Mazingira.

Kwa kweli masuala haya yanatuhusu jamii, yaani sote na sisi kama Wawakilishi wa wananchi wetu kwenye majimbo, basi Mhe. Spika, hatuna budi kuwa mstari wa mbele kabisa kusaidia wizara, kwa sababu wizara wao wako mbele kwa sera, lakini sisi ndio ambao tunao watu majimboni pamoja na mitaani.

Kwa hivyo, ni vyema kabisa kwa kushirikiana na sisi upande wetu Serikali za Mitaa, Madiwani, basi tutashirikiana na wizara, ili tuhakikishe kwamba haya majanga makubwa yanayoharibu nguvu kazi yetu, yanayopinga usalama wetu wa vijana na kuhatarisha maisha yao tunayapiga vita kwa kadri tunavyoweza.

Mhe. Spika, si mambo ya kuficha na wala sisemi ya kificho, kwamba haya matatizo ni makubwa na hasa madawa ya kulevya, yaani vijana wabichi nguvu kazi wanaoweza kufanyakazi, lakini utawakuta wanasinzia na wanazungumza lugha wala huifahamu mpaka utege sikio vizuri ndio ufahamu.

Kwa mfano, kuna ujumbe mmoja mara nyingi wanautoa Sauti ya Tanzania Zanzibar wa ndani ya daladala ule na wala sipendi kuurudia, lakini wanaigiza kidogo na mwisho konda anaambiwa amsamehe, yaani asitoe nauli.
Jambo kubwa ambalo hatuna budi ni kama nilivyosema tuungane sote na tusaidie wizara na wizara wenyewe wamesimama kidete, pia hatuna budi kuipongeza sana hii Tume ya UKIMWI kwa kazi zao nzuri sana. Vile vile naunga mkono kama Waheshimiwa Wajumbe wengi walivyosema kwamba labda tupunguze semina na twende zaidi kwa vijana. *(Makofi)*

Lakini hakuna namna vijana hawa lazima wapewe taaluma jinsi ya kubadilika, yaani wageuze tabia zao na njia nzuri wenyewe wataalamu wanasema ni kuwanasihi au kuwaasa, kufanya mazungumzo nao kuwaonesha tabia nzuri. Mhe. Spika, nashukuru kwenye Jimbo langu kuna Vikundi kama vile Tomondo wapo vijana wamebadilika na hivi sasa wako mstari wa mbele kabisa katika kujenga nchi.

Mhe. Spika, naomba nigusie mambo matatu ambayo yaligusiwa na Waheshimiwa Wajumbe. Kwanza kuhusu suala la *bars* za mitaani. Kweli Mhe. Spika, kwenye mitaa yetu tunazo *bars* ambazo zinaathiri amani ya wananchi wetu mitaani. *(Makofi)*

Lakini utaratibu upo Mhe. Spika, kwamba *bar* yoyote haipewi leseni bila ya ridhaa ya wananchi wenyewe wa mtaa na wao wanapokata leseni *Municipality* wanafuata taratibu zote. Kwa hivyo, kabla ya kutolewa leseni basi wananchi wa mtaa ule wanashirikishwa na wanapewa fursa ya kukata *appeal* kwamba *bar* hii ilioko kwa Kwaalinato sisi hatuitaki au *bar* iliopo Shangani inatunyima usingizi. Hivyo, *bar* ile Mhe. Spika, haipewi leseni na inazuiliwa ku-*operate*.

Mhe. Spika, tunafahamu wako wengine wabishi sana wanapozuiliwa wanakuwa wana-*operate* kwa mlango wa nyuma. Kwa hivyo, naomba sana hili na sisi ndio Wawakilishi wenye majimbo, basi tushirikiane na tuulize. Kwa mfano, tunao Madiwani wetu kweli *bar* zile zina-*operate* kihalali na kama hazi-*operate* kihalali, basi sisi tufuatilie na tuchukue hatua. Vile vile *Inspectors* wetu wanafuatilia, ili kuona kwamba *bar* hizo zinapata leseni kwa zile ambazo hazina matatizo.

Lakini baya zaidi na kinachogomba sana ni kelele za mziki, *disco* kwenye mitaa hii. Sasa hili nimezungumza na mwenzangu Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo hili tulishughulikie, kwa sababu vibali vya *disco* za mziki hatutoi sisi kwenye *Municipality* au Mabaraza ya Miji wanatoa wenzetu watu wa Sanaa, sasa hili tutalifanyia kazi. Mhe. Spika, sisi tunasema mziki umalize saa 6:00 usiku lakini wao wametoa ruhusa mpaka saa 8:00 usiku au alfajiri na hii inakuwa ni kero mitaani. *(Makofi)*

Kwa hivyo, suala hili Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe watuachie sisi wizara mbili tutakaa, tuone kwamba tunatengeneza sheria kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuona kwamba adha hii kwa wananchi wetu tunaiondoa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, rafiki yangu Mhe. Abdalla Juma Abdalla alitoa *live experience* ya uvutaji wa bangi ndani ya Chuo cha Mafunzo na alisema kwamba ameshuhudia mwenyewe, sasa kitu mtu akishuhudia huwezi kumkaidi. Lakini ninachosema tokea wakati alipokuwepo Chuo cha Mafunzo nadhani miaka mingi imepita. Mhe. Spika, ninachosema kwa kweli tumebadilika na tumejirekebisha nakumbuka niliwahi kujibu swali na kusema kama tunambaini askari yeyote anafanya vitendo hivyo, basi hatumuachii na tutajitahidi kumchukulie hatua isavyo.

Suala jengine ili kuondoa msongomano, ndio maana hivi sasa serikali imeamua kujenga Chuo cha Mafunzo kipya na Mhe. Mjumbe alisema ndilo hilo gereza jipya aa! Sisi tumekubaliana kiitwe Chuo cha Mafunzo (*Reformatory School*), yaani tuwabadilishe vijana wetu.

Sasa namuomba sana na yeye alitumie jina hili, kwa sababu yeye ni Mhe. Mwakilishi akipata jina zuri basi hilo ndilo atakalolipeleka kwa wananchi. Mhe. Spika, kweli haya yalikuwepo huko nyuma, lakini tunajitahidi kuweka sawa mambo na moja wapo ni hilo la kujenga Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Spika, pia kulikuwa na suala la maambukizi ya UKIMWI kwenye ukurasa wa 17, kwamba utafiti umeonesha kuwa Chuo cha Mafunzo asilimia ya maambukizi ni asilimia 2.8 na hiyo ilikuwa ni mwaka 2008. Mhe. Spika, kweli kama huo utafiti umeonesha ni suala la kutisha na zaidi malalamiko haya tumeyapata kwa wale wanafunzi ambao ni watoto.

Mhe. Spika, naomba nichukue dakika chache kidogo nielezee takwimu ambazo zitajieleza vizuri sana. Mwaka 2005 tulipokea wanafunzi 230, waliorejea tena, maana yake wanakwenda wakirudi 34, mwaka 2006 tulipokea wanafunzi 277, waliorejea tena baada ya muda ni 50, mwaka 2007 tulipokea wanafunzi 310, waliorejea ni 52.

Vile vile mwaka 2008 tulipokea wanafunzi 314, waliorejea ni 53, mwaka 2009 tulipokea wanafunzi 317, waliorejea ni 50, mwaka 2010 tulipokea wanafunzi 309, waliorejea ni 50 na mwaka huu tumepokea wanafunzi 157, wanaorejea ni 23.

Mhe. Spika, hii imesema makusudi wanaorejea, kwa sababu wengine kule wanaona ndio nyumbani kwao na wanapokaa huku hawana kazi na wala la kufanya na kuona ni vyema kurejea kule tu. Kwa mfano, wakati anaporudi anasema sahani yangu asiiguse mtu wala godoro langu asiguse mtu, kweli basi kule nje anakwenda kufanya uhuni wowote na baada ya muda mfupi anarudi tena, kama vile kulewa au mambo mengine.

Point kubwa ambayo nataka kusema Mhe. Spika, kuhusu hawa wanaorejea wengi wao wana matatizo ya madawa ya kulevya, hayo tunayoyasema ya kuvuta bangi, uzinzi wa UKIMWI ndio yote si ajabu kwa utafiti huo kwa wakati huo huko Chuo cha Mafunzo ulionekana.

Lakini kule hawana nafasi yak ku-*practice* hayo na moja moja kesi zinatokea kama alivyoisimulia Mhe. Zahra Ali Hamad mwaka jana, imetokezea. Mhe. Spika, tunajitahidi sana kuwadhibiti. Sasa vyanzo au kesi hizi wanatokanazo nje ndio wanazileta kule.

Kwa hivyo, Mhe. Spika nilisema nitoe data hizi kwa sababu ni muhimu sana kuonesha kwamba sisi ndio wenye wananchi, hivyo naomba sana tusaidiane tuwanasihi wawe raia wema na baada ya kufunzwa basi warudi na wawe wamesafika na kufanyakazi zao na wala wasiseme warudi tena Chuo cha Mafunzo.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kusema kwamba naunga mkono hoja na ninamtakia kila la kheri Mhe. Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama na kutukutanisha hapa leo hii tukiwa katika hali ya afya na uzima, kwa ajili ya kuendelea na shughuli zetu za kuiletea maendeleo nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kukupongeza wewe binafsi, lakini pia na Mwenyekiti wako Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa kwa kuweza kuendesha vyema mijadala muda wote ambapo Wajumbe wa Baraza lako tukufu walikuwa wakijadili na kuchangia Hotuba ya Bajeti inayohusiana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia kwa kuzungumza na pia kwa maandishi. Vile vile niwashukuru hata wale Wajumbe ambao walikuwa watulivu kusikiliza michango nia ikiwa ni kuboresha hotuba yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais naomba kupokea pongezi pamoja na shukurani zote tulizopewa kama ofisi na pia kwa serikali kwa jumla. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niruhusu kumshukuru tena Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniamini na kunipa uongozi wa ofisi hii muhimu, yenye majukumu nyeti na mtambuka ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya ustawi wa jamii yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba pia uniruhusu kuendelea kuwashukuru Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharif Hamad, pia na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi kwa ushauri na msaada wao wanaonipa katika kufanikisha majukumu yangu ya kazi za kila siku. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kumalizia napenda kuwashukuru wananchi wote wa Zanzibar kwa kudumisha hali ya amani na utulivu, ambao unaipa nafasi nzuri serikali yetu kushughulikia maendeleo yao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wamepata fursa ya kuchangia hotuba hii na niwashukuru kwa kuanza awali mapema kuiunga mkono bajeti yetu, isipokuwa kwa ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija ambaye najua baada ya kupata maelezo na yeye hataonosha shilingi katika bajeti hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kutoa shukurani maalum kwa Waziri na Manaibu Mawaziri ambao wamefanyakazi ya kusaidia kujibu hoja ambazo zinahusiana na taasisi zao. Shukurani Maalum kwa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Naibu Waziri wa Afya, Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba pia kuchukua nafasi hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Hamza Hassan Juma na chini ya Makamu Mwenyekiti Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, kwa maelekezo yao pamoja na ushauri mzuri walioutoa ambao utakuwa dira muhimu ya utekelezaji wa kazi mbali mbali za ofisi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imepokea ushauri wote uliotolewa na naomba niahidi kuwa ushauri huo utatekelezwa kikamilifu, kwa ajili ya kusimamia shughuli za Usimamizi wa Mazingira hapa nchini, Vita dhidi ya UKIMWI, Madawa ya Kulevya na Kuimarisha Fursa Sawa kwa Watu Wenye Ulemavu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jumla ya Waheshimiwa Wajumbe 30 walipata fursa ya kuchangia kwa kuzungumza katika hotuba hii, pia Waheshimiwa Wajumbe 12 walipata nafasi ya kunichangia kwa maandishi katika hotuba hii. Hivyo, naomba uniruhusu niwatambue kwa kuwataja kwa majina wale wote waliochangia katika Hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:-

1. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa);
2. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa;
3. Mhe. Rashid Seif Suleiman;
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu;
5. Mhe. Farida Amour Mohammed;
6. Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi
7. Mhe. Salmin Awadh Salmin;
8. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa;
9. Mhe. Abdalla Juma Abdalla;
10. Mhe. Abdalla Moh'd Ali;
11. Mhe. Raya Suleiman Hamad;
12. Mhe. Abdi Mosi Kombo;
13. Mhe. Suleiman Hemed Khamis;
14. Mhe. Hassan Hamad Omar;
15. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak;
16. Mhe. Rufai Said Rufai;
17. Mhe. Hija Hassan Hija;
18. Mhe. Asha Bakari Makame;
19. Mhe. Mwanasheria Mkuu;
20. Mhe. Naibu Waziri wa Afya;
21. Mhe. Ashura Sharif Ali;
22. Mhe. Amina Iddi Mabrouk;
23. Mhe. Mussa Ali Hassan;
24. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali;
25. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Waliochangia kwa maandishi ni pamoja na

1. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko;
2. Mhe. Bikame Yussuf Hamad;
3. Mhe. Asha Abdu Haji;
4. Mhe. Mgeni Hassan Juma;
5. Mhe. Mohammed Haji Khalid;
6. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman;
7. Mhe. Naibu Waziri Biashara, Viwanda na Masoko;

8. Mhe. Nassor Salim Ali;
9. Mhe. Wanu Hafidh Ameir;
10. Mhe. Salma Mohammed Ali;
11. Mhe. Mussa Khamis Silima;
12. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na
13. Mhe. Panya Ali Abdalla.

Mhe. Spika, baada ya kuwashukuru Wajumbe sasa naomba nichukue fursa hii kujibu maswali ambayo yameulizwa. Mhe. Spika, naomba niliarifu Baraza lako tukufu kwamba nimepokea kwa moyo mkunjufu kabisa ushauri pamoja na michango yote ya Wajumbe ya moja kwa moja pamoja na ile ya maandishi na ofisi yangu inaahidi kwamba tutaifanyiakazi kama ambavyo itastahiki, lakini kwa kuzingatia taratibu na sheria zilizopo.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza kujibu swali moja moja naomba kwanza nitoe maelezo ya jumla katika suala la mazingira ambalo limechangiwa karibu na Wajumbe wote waliobahatika kuchangia. Mhe. Spika, kwa hapa Zanzibar maliasili zisizorejesheka zinajumuisha mchanga, mawe, kokoto, kifusi, udongo, uchimbaji wa matofali na mfano wa hayo.

Mhe. Spika, naomba niliarifu Baraza lako tukufu kuwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na wadau wote imetayarisha Kanuni za Usimamizi wa Maliasili Zisizorejesheka, ili kusimamia vizuri uchimbaji wa rasilimali hizi ikiwa ni pamoja na kuendeleza maeneo yaliyomaliza kuchimbwa. Kanuni hizo hivi sasa zipo katika hatua za mwisho za kumalizika.

Mhe. Spika, serikali haikatazi matumizi ya maliasili zisizorejesheka, kwani ni jambo lisilowezekana, kwa sababu maendeleo yoyote yanahitaji matumizi ya maliasili hizo. Hata hivyo, ni lazima uchimbaji, uchukuwaji, uvunaji na usafirishaji wa maliasili hizo ufuate taratibu na miongozo maalum, ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na matumizi endelevu za maliasili hizo bila ya kuathiri mazingira ya nchi kwa faida yetu pamoja na kizazi kijacho.

Mhe. Spika, nchi yetu ni visiwa ambavyo muhimili wake ni milima, miamba pamoja na mawe yaliopo kwenye ardhi. Kwa hivyo, kama hatutokuwa makini na kuanza kuondoa mihimili hiyo na kuikata bila ya utaratibu maalum, basi ni dhahiri kuwa tutakarisha janga ambalo hatutakuwa na uwezo wa kulizuia.

Kutokana na hali hiyo, serikali imechukua hatua ya kupiga marufuku ukataji wa matofali na maliasili nyengine zisizorejesheka kwa maeneo ya Mwambe Kwasanani, Makangale Mnarani, Pujini Mtumbikuhama. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda Waheshimiwa Wajumbe wafahamu kwamba suala la kuwapatia wananchi njia mbadala kwa ajili ya kipato ni muhimu sana, ili kupunguza shindikizo la uchukuwaji wa maliasili za aina mbali mbali na inapaswa kuzingatiwa na wadau wote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kila mmoja wetu tunamuomba afikirie namna gani ataweza kushirikiana na serikali na jamii kwa jumla, ili kuona jamii yetu inapata njia mbadala itakayoimarisha uhifadhi wa mazingira katika visiwa vyetu.

Kwa kweli ukataji wa minazi, miti kwa kutumia misumeno ya moto. Mhe. Spika, ni kweli hivi sasa kumekuwa na ongezeko kubwa la ukataji wa minazi, miti na matumizi mabaya ya msumemo wa moto. Ofisi ya Makamu wa Kwanza imechukua hatua mbali mbali za kuielimisha jamii juu ya ukataji ovyo miti ya aina mbali mbali. Vile vile tumechukua hatua za kuielimisha jamii juu ya umuhimu wa upandaji miti na utunzaji wa miti hasa ile miti ya matunda.

Mhe. Spika, hivi karibuni katika Kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani ambazo hufanyika tarehe 5 Juni kila mwaka. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeweza kupanda miti 10,000 na siku ya Jumamosi ya tarehe 25 Juni kwa kushirikiana na *Kenya Commercial Bank* tumeweza kupanda miche 1,500 katika maeneo mbali mbali. Nafahamu kwamba zipo juhudi kama hizi zinaendelea kuchukuliwa na Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka. *(Makofi)*

Aidha nachukua nafasi hii pia kuhamasisha Wajumbe wa Baraza la wawakilishi tuendelee kushiriki kwenye Kampeni za Upandaji Miti, ili visiwa vyetu vibakie kuwa visiwa vya kijani. Sambamba na hilo naomba niliarifu Baraza lako kuwa serikali imo katika hatua za kukamilisha Kanuni ya Udhibiti wa Msumemo wa Moto, ili kupunguza kasi ya ukataji wa miti iliopo hapa nchini.

Mhe. Spika, kuhusiana na usafi wa mazingira na matumizi ya mifuko ya *plastic*. Mhe. Spika, ni wazi kuwa bado usafi wa mazingira katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar haujawa wa kuridhisha, kwenye maeneo mengi ya Zanzibar kumekuwa na usimamizi ambao si mzuri na utupaji ovyo wa taka.

Kwa hivyo, ili tuweze kuimarisha usafi kwenye maeneo yetu ushiriki wa kila mmoja wetu ni jambo lisiloepukika. Ofisi yetu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais kupitia Tawala za Mikoa ina lengo la kuandaa mpango wa kuwa na siku maalum ya usafi, ili kila mmoja wetu apate nafasi ya kushiriki katika kuweka maeneo yetu katika hali ya usafi. Aidha nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuvisaidia Vikundi vya Mazingira vilivyomo kwenye maeneo yao kwa kuvipatia vifaa vinavyohitajika. Mhe. Spika, naiomba jamii ya

Zanzibar ibadilile na iwe jamii inayopenda usafi kama historia yetu inavyotuelekeza.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutoa maelezo yakina juu ya kesi mbili za Mifuko ya *Plastic*, kwenye kesi hizo tumeweza kujifunza na kulazimika kufanya marekebisho ya Kanuni na Udhibiti wa Mifuko ya *Plastic*. Nimategemeo ya ofisi yetu kuwa marekebisho hayo yatasaidia kudhibiti uzuri matumizi ya mifuko ya *plastic* hapa nchini.

Mhe. Spika, naomba sasa nizungumzie kuhusu mabadiliko ya tabia ya nchi, uharibifu wa fukwe na maeneo yanayoingia maji ya chumvi. Hivi sasa ni kweli Zanzibar inakabiliwa na changamoto zinazoambatana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Miongoni mwa changamoto hizo ni mashamba kuingia maji ya bahari, upungufu wa mvua na maji ya visima, mmong'onyoko wa fukwe, uharibifu wa matumbawe, kilimo na kadhalika

Mfano wa maeneo yaliyoathiriwa na bahari ni kama vile Kilimani, Bwawani, Jambiani, Uroa, Chwaka, Makunduchi, Nungwi, Tumbatu, Mkokotoni, Kiwengwa, Mangapwani, Chumbe, Wingwi, Ukele, Kisiwapanza, Kengeja na maeneo mengineyo. Ni dhahiri basi ili kuweza kukabiliana na hali hiyo mikakati madhubuti itahitajika, kutokana na hali hiyo Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ipo katika hatua ya kutayarisha mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, mkakati huo utaonyesha kipaumbele cha maeneo na hatua zinazofaa kuchukuliwa pamoja na miradi ya utekelezaji.

Mhe. Spika, naomba sasa nizungumzie juu ya tathmini za athari za kimazingira, suala la tathimini za athari za kimazingira ni mchakato ambapo duniani unafuata mfumo mmoja lengo la tathmini hii ni kubainisha na kutambua athari za kimazingira na kijamii zinazoweza kujitokeza kutoka na mradi unatarajiwa kutekelezwa.

Tathmini hii hufanywa mwanzo kabka mradi husika haujaanza na hutoa muongozo hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kikabiliana na athari zitakazotokea, mchakato uliopo hutoa nafasi kwa taasisi za mazingira kutayarisha hadudi rejea kwa ajili ya tathmini hiyo ambayo hufanywa na kampuni ya ushauri.

Aidha taasisi ya mazingira hupata nafasi ya kuangalia ubora wa kazi uliofanywa ili kuhakikisha kazi hiyo imefanywa kwa mujibu wa hududi rejea iliyotolewa, kama tathmini hiyo imekizi viwango vilivyotajwa kwenye hadudi rejea cheti cha mazingira hutolewa, hivyo kwa kuwa ni mchakato ambao unatumika dunia nzima ni wazi kabisa Zanzibar nayo inapaswa kufuata mchakato huo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu alionyesha wasi wasi wake juu ya usimamizi wa shughuli za mazingira na akadhania ni kauli za kisiasa tu kutokana na kuingiziwa fedha, hasa pale alipotaja asilimi 19.1 kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Mhe. Spika, nataka kumhakikishia na waheshimiwa wengine wote ambao walionyesha wasi wasi huo kuwa haya sio matamko ya kisiasa tu, kwani ukaangalia yalivyotekelezwa kwa mwaka huo huo wa 2010/2011 utaona ni kwa kiasi gani tumeweza kutekeleza malengo yaliyopangwa mwaka huo wa 2010/2011.

Ni kweli mwaka huu Idara haikupata fedha kama ilivyokadiriwa kwa sababu ya kiufundi na wala sio utashi, tutakumbuka kuwa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alipokuwa akiwasilisha bajeti ya serikali alitoa taarifa kuwa serikali ya awamu ya saba ilipoingia madarakani haikuomba *supplementary budget* kwa vile kilichofanyika ni kuhaulisha vifungu tu kwa bajeti ile ile iliyopitishwa.

Hivyo Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ilianzishwa kwa kuanzia na bajeti ya idara tatu Idara ya mazingira, Idara ya watu wenye ulemavu na Tume ya dawa za kulevya pamoja na nyongeza ya fedha kidogo kutoka Hazina ambazo kwa ujumla ilikuwa ni kama milioni 686,735,932 kwa ajili ya matumizi ya kuendesha kazi na mishahara kwa kipindi cha Januari hadi Juni mwaka 2011.

Hivyo tukalazimika kuhaulisha vifungu ili kuanzisha Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ambapo bajeti hiyo pamoja na idara hizo ilihudumia Ofisi ya faragha, idara mpya ya mipango sera na utafiti, idara ya uendeshaji na utumishi na pia Afisi kuu iliopo Pemba. Aidha asilimia iliyoonekana haikuingiza kiwango cha mshahara waliyoipata kabla ya Disemba ambapo walikuwa chini ya Wizara ya Kilimo.

Mhe. Spika, natumai Mhe. Ismail Jussa Ladhu amefahamu ni kwa nini asilimia ya mgao wa fedha unaoonekana ni mdogo lakini kwa ujumla hadi mwezi wa Mei, Shilingi milioni 599,861,1866 zilikwishapatikana kwa Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, pia naomba nimjibu Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Hija Hassan Hijia Muwakilishi wa Kiwani kuhusu kutokuwa na fungu maalum la Ofisi ya faragha kama vile zilivyo Ofisi ya Rais na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, naomba kwanza kutoa maelezo yafutayo.
Ofisi ya faragha ni Ofisi rasmi za viongozi wa kitaifa zenye majukumu ya kuratibu shughuli za viongozi wa kitaifa, Ofisi hizi zimetolewa utaratibu maalum na serikali juu ya wasaidizi na watendaji wa Ofisi hizi pamoja na huduma zao. Mhe. Spika, Ofisi ya faragha ya Mhe. Rais na Ofisi ya faragha ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais zina historia ndefu kuliko Ofisi ya faragha ya

Makamo wa Kwanza wa Rais, Ofisi hizi mbili zilianza na kuwa na huduma ya Rais na Waziri Kiongozi idara hizi zilisimamia nyumba za viongozi hawa ziliopo Unguja, Pemba, Dar es Salaam na Dodoma.

Mwaka 1994 idara ya huduma ikaondosha na kubaki ofisi ya faragha na cheo cha Mkurugenzi wa huduma kikachukuliwa na mnikulu ambae amekuwa akifanya kazi chini ya Katibu wa Rais na kwa upande wa ofisi ya Waziri Kiongozi ikabaki kuongozwa na Katibu wa Waziri Kiongozi na wanaoshughulikia shughuli za nyumba wakawa watunza nyumba, hivyo ofisi hizi ziliwekewa mafungu yao ndani ya Ofisi zao.

Kwa wakati huo kulilazimika kufanywa hivyo kwani viongozi wa kitaifa walikuwa wakihudumiwa moja kwa moja chakula chao na serikali ndio iliyokuwa ikitoa dhabuni za vyakula na kununua, kinyume na sasa ambapo kila kiongozi ameshakadiriwa chakula chake na anakabidhiwa mwenyewe kwa kutumia mfumo aliokubaliana na wasaidizi wake.

Ofisi ya Makamo wa Pili imerithi kila kilichokuwa cha Afisi ya Waziri Kiongozi Mhe. Spika, Ofisi ya faragha ya Makamo wa Kwanza ni mpya na miezi sita tu tokea ianzishwe na bado haijakamilika, kwani wasaidizi wengine bado hawajateuliwa hadi sasa na bado hajapata nyumba Dar es Salaam na serikali inategemea kuanza ujenzi wa nyumba huko Pemba mwaka huu wa fedha. Hii haina maana kwamba ukiita faragha inakosa zile huduma muhimu zinazohitajika, ofisi ya faragha ina fursa sawa na ofisi nyengine yoyote ile kwani mafao na maslahi yote ya wafanyakazi wa faragha yanafanyika.

Mhe. Spika, ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ni Ofisi mpya na kutokana na bajeti yetu ya jumla huwa haitoshi kujitanua hivyo Idara zote zilizopo Makao makuu zinapata huduma sehemu moja, kwa maana hiyo Ofisi ya Faragha ya Makamo wa Kwanza wa Rais Idara ya Mipango sera na utafiti na Idara ya Uendeshaji na utumishi zinahudumiwa pamoja chini ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi, ndio maana Idara ya Mipango sera na Utafiti imepata mgao wa shilingi milioni 15 kwa ajili ya shughuli ambazo ni maalum. Mambo mengine yaliyobakia kuanzia mishahara nauli za likizo, ununuzi wa vitendea kazi, mafunzo, ununizi wa shajala, mafuta, vifaa vya usafiri, malipo yia umeme, simu, fax, *internet*, maji na matumizi yote chini ya matumizi ya kazi za kawaida yanatumiwa kwa pamoja na kufanywa malipo sehemu moja.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kuchukua waandishi wa habari kwa safari za nje naliomba kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa serikali imeshatoa muongozo nani wafuatane na viongozi wa kitaifa katika ziara zao za ndani na nje ya nchi, kwa bahati mwandishi wa habari ni sehemu ya watakaoungana katika safari hizo za viongozi wa wakuu.

Aidha Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitaka kujua taarifa kamili juu ya ziara pekee ya nje ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais aliyoifanya, katika hotuba yangu nimesema nini serikali imefanya katika kufuatia mafanikio yaliyopatikana katika ziara ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Mhe. Spika, naomba baraza lako tukufu nilitahadharishe kwamba viongozi wetu wa kitaifa wanapokwenda safari na kufanya mazungumzo huwa tunajaribu kwa nia njema kutafuta misaada ambayo inaweza kuifikia nchi yetu kwa ajili ya kukwamua matatizo yetu mbali mbali, inawezekana tukapewa ahadi na ahadi hizo zikawa hazikutekelezwa.

Kwa sababu Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitaka nifafanue kama ambavyo imefafanuliwa katika Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais katika ziara zake, mimi naomba nitoe pamoja na angalizo nililolisema hapo mwanzo . Kwamba kimsingi ziara zilikuwa ni katika kufufua mahusiano yaliyoko kati ya nchi yetu na hasa Oman ambao tumekuwa na udugu wa muda mrefu, kubwa ilikuwa ni kufufua ule udugu lakini kwa Oman mazungumzo yalifanyika na sasa hivi tayari Oman *Air* tayari imeshaanza safari zake za moja kwa moja kutoka Oman na kutua Zanzibar hayo ni mafanikio ya ziara.

Lakini pia kuna ujumbe ulitoka Oman siku hizi za karibuni kwa nia ya kusaidia shughuli za nyaraka na mambo ya asili, vile vile katika ziara hiyo ya Oman Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais alipata kufanya mazungumzo na wafanya biashara na wawekezaji kuhusiana na mambo yafuatayo.

- Kusaiaida katika utafutaji wa mafuta
- Kusaidia kuanzisha Shirika la Ndege la Zanzibar
- Kusaidia uendelezaji wa taasisi za dini.

Katika ziara hiyo ya Oman tayari tumeshawasilisha maombi yetu kuhusiana na maombi ya lami , mabomba ya maji, dawa za hospitali, vifaa mbali mbali vya elimu.

Mhe. Spika, katika ziara ya Falme za Nchi za Kiarabu mazungumzo pia yalifanywa na wawekezaji katika nia ya kusaidia katika kuendeleza bandari ya Zanzibar mpya ya Mpiga Duri kusaidia katika kuendeleza maeneo huru ya kiuchumi, na pia kukisaidia Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar katika kubadilishana wanafunzi lakini pia kupata nafasi za masomo katika Chuo Kikuu cha Oman.

Mhe. Spika, naomba kuunganisha hapa hapa suala la Mhe. Hija Hassan Hija muwakilishi wa kiwani kuhusiana na ushiriki wa mama wetu mpendwa mama Awena katika shughuli maalum za maendeleo, kwa maana hiyo basi ushiriki wa mke wa kiongoziwa kitaifa ni wa hiyari, napenda kulieleza baraza lako

tukufu kwamba mama Awena na yeye hayuko nyuma katika hili, amekuwa akishiriki katika shughuli mbali mbali za kijamii pale anapoalikwa au anapofanya ziara rasmi za kazi, na afisi yetu ya faragha imekuwa ikiratibu shughuli hizi na kumhudumia ipasavyo kila inapohitajika.

Mhe. Spika, sasa naomba nizungumzia juu ya Idara ya watu wenye Ulemavu, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mheshimiwa Ashura Sharif pamoja na waheshimiwa wengine walitaka kuona ni vipi sheria inatekelezwa juu ya majengo kwa watu wenye ulemavu, sheria namba 9 ya mwaka 2006 ya watu wenyewe ulemavu haki na fursa sawa imezungumzia kuwa na mazingira rafiki na kutopata kizuizi katika nyumba za umma na vifaa kwa ajili ya matumizi ya umma, kifungu namba 12(1), (2) na (3) kinaeleza upatikanaji na uwezo wa kufikia huduma. Hata hivyo Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais haijaandaa kanuni za utekelezaji wa sheria hii kwanza tunahitaji kufanya mabadiliko ya sheria ya watu wenye ulemavu, ambayo sasa inafanyiwa mapitio ili tuweze kuandaa kanuni hizo.

Lakini pia kulikuwa na suala ni kwa nini hakuna lugha ya alama katika vyombo vya habari vyetu vya hapa nchini na hasa TVZ, ni kweli mpaka sasa katika vyombo vya habari hasa TVZ hakuna mkalimani wa lugha ya alama kwa ajili ya mawasiliano kwa wenzetu wenye ulemavu wa kusikia, hasa katika baraza letu hili tukufu hakuna mkalimani huyo ambae ataisaidiashughuli zetu hizi za baraza kufahamika vizuri kwa wenzetu wenye ulemavu. Mhe. Spika, tayari Ofisi yetu imeshashajihisha vyombo vya habari katika suala hili na tutategemea Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo watalishughulikia suala hili kwa umuhimu wake.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mbwana Hamad wa jimbo la Chambani kuhusiana na mfumo wa ukusanyaji wa taarifa masuala ya watu wenye ulemavu umejionyesha kwa upande mmoja tu wa Unguja, lakini haikuonekana wilaya hata moja kwa huko Pemba. Mhe. Spika, idara ya watu wenye ulemavu ilianza kukusanya taarifa kwa hapa Unguja tarehe 11/4/2011 na kumaliza tarehe 26/5/2011 katika Wilaya mbili tu za Unguja Kaskaini (A) na Kaskazini (B). Pia mpango huu unatarajiwa katika kisiwa cha Pemba katika Wilaya ya Mkoani na Chake-Chake katika Mkoa wa Kusini Pemba, mapema katika kipindi cha fedha 2011/2012 lakini pia kuendelea katika mikoa mingine ya Zanzibar hadi kumaliza mikoa yote kumi iliyomo ndani ya visiwa vyetu.

Mhe. Spika, naomba kuuliza juu ya suala la kwamba Pemba kuna mfanyakazi mmoja tu na anashindwa hata kupewa likizo kwa sababu hakuna mtu wa kuchukua kazi zake, ni kweli Idara ya watu wenye Ulemavu kwa Pemba ilikuwa na mfanyakazi mmoja, ila kwa sasa ina wafanyakazi wawili, lakini vile vile kwa kuliona hilo ofisi yangu katika mwaka wa fedha 2011/2012 imetenga

nafasi nne na tayari zimeshakubaliwa katika kuajiri wafanyakazi wapya. Nafasi hizo ni katika Afisi ya Walemavu Mkoa nafasi mbili katika Mkoa wa Kusini na Moja Mkoa wa kaskani Afisa uhamasishaji na Afisa mhudumu mmoja.

Mhe. Spika, mara tu bajeti yetu itakapopita maafisa hao wataajiriwa rasmi na kuziba nafasi tupu kwa upande wa Pemba, naomba ieleweke kwamba nafasi hizi za uajiri hazipo tu kwa ajili ya watu wenye ulemavu pekee kwa ajili ya watu wote wenye sifa za kufanya kazi katika sehemu hizo.

Mhe. Spika, naomba nizungumze juu ya mchango wa Mhe. Mtumwa Kheir Mbaraka anaeleza kwamba waziri akae na wizara ya miundo mbinu pamoja na madereva na kondakta kuzungumzia suala la unyanyasaji wa watu wenye ulemavu katika usafiri wa umma, namuarifu kwamba ushauri wake tumeupokea na kweli unaweza kutuletea mambo mazuri katika jamii yetu tutafanya hivyo kwa kujipanga.

Mhe. Raya Suleiman Hamad alielezea kwamba Wizara haina Afisi Pemba naomba nitoe ufafanuzi Mhe. Spika, idara ya watu wenye ulemavu kwa upande wa Pemba tokea kuanzishwa kwake mwaka 2008 ina ofisi ya kudumu na ilikuwepo chini ya ofisi ya Waziri Kiongozi Pemba, mara tu baada ya serikali ya muundo wa kitaifa idara hii imehamishwa chini ya Ofisi ya Makamo wa kwanza wa Rais pamoja na mambo mengine idara haijapunguza wafanyakazi hata mmoja na ina mpango wa kuengeza wafanyakazi kama nilivyoeleza hapo mwanzo.

Mhe. Raya Suleiman Hamad pia alizungumzia umoja wa watu wenye ulemavu ambao imekumbwa na matatizo ya fedha za wahisani, nataka nimuarifu tu kwamba kama NGos basi inakumbwa na matatizo yale yale ambapo taasisi hizi zisizo za serikali zote zina matatizo ya fedha na mambo kama haya ya ofisi ambayo ameyaelezea. Vile vile alisema Baraza la watu wenye ulemavu haliko kihalali kwa sababu halina muwakilishi yoyote kutoka Pemba, naomba kumfahamisha Mhe. Raya Suleiman Hamad kwamba kwa mujibu wa sheria namba 9 ya mwaka 2006 ya watu wenye ulemavu haki na fursa haikuondoa uhalali wa kuweko baraza la taifa la walemavu kwa sababu tu ya kutokumteua mtu kutoka Pemba.

Hata hivyo ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais haina mamlaka ya kuchaagua mjumbe kutoka Pemba, ila jumuiya ya watu wenye ulemavu ndizo zinazopendekeza majina ya nani aingie katika baraza la watu wenye ulemavu. Naomba nichukue nafasi hii kumshauri Mhe. Raya Suleiman Hamad kuzishawishi jumuiya za watu wenye walemavu kupendekeza wajumbe kutoka

Pemba ili baraza liwe na uwiano unaokusudiwa, kilichopo kwenye sheria ya kuunda Baraza hili ni uwiano wa kijinsia na ambao ofisi yangu unauzingatia.

Mhe. Raya Suleiman Hamad vile vile alizungumzia juu ya kuwa na mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu, wajumbe wa baraza la watu wenye ulemavu, baraza hili lilifanya ziara katika taasisi mbali mbali za serikali na kutoa ushauri kwa wakurugenzi na waheshimiwa Mawaziri juu ya kuweka mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu. Mhe. Spika, kinachotushangaza kwamba hata taasisi kubwa bado ziko nyuma katika suala hili la majengo, ushauri wangu ni kwamba tuwe tunaliangalia hili kama jamii taasisi zote ambazo zinapaswa kutoa huduma za kijamii katika majenzi yetu tuzingatie san asana uwezekano wa wenzetu ambao wana ulemavu kuweza kufikia huduma katika majengo haya. Mhe. Spika, naliomba Baraza lako tukufu pia liweke mkalimani wa lugha ya alama ili kuwafikishia taarifa hizi muhimu wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, sasa naomba nizungumzie masuala ya Ukimwi na kabla sijenda kwenye hoja zilizotolewa na wajumbe naomba kueleza mambo ya ujumla yafuatayo ambayo yatasaidia kuelewa mazingira ambayo tume ya ukimwi inahusika katika mapambano dhidi ya Ukimwi. Kwanza tume ya Ukimwi ni taasisi inayojitegemea ambayo imeundwa kwa sheria namba tatu ya mwaka 2002 na inaongozwa na bodi ya makamishna, lakini Wizara yake mama ndio hii Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Tume hii ya Ukimwi kazi zake kubwa ni kuratibu shughuli zote za ukimwi katika ngazi za kitaifa, baadhi ya majukumu ya Tume katika kutekeleza wajibu wake ni kutafuta fedha kwa ajili ya mapambano haya, kusaidia wadau mbali mbali wanaotekeleza program za ukimwi.

Mhe. Spika, naomba sasa uniruhusu kutofa ufafanuzi wa hoja zilizoelezwa ambazo nimeweka katika makundi yafuatayo, katika hili naomba wajumbe wanivumilie kwamba karibu wote walizungumzia masuala ya ukimwi basi hapa nitakuwa nimepata majibu yao, kwa sababu yalikuwa ni masuala ya kijumla jumla. Kulikuwa na tuhuma kuhusu kuhusika na tume katika kutoa huduma zake kwenye matamasha na mikusanyiko mbali mbali labda haitoi ushirikiano katika sehemu hizo, lakini pia hali ya fedha katika tume na jinsi zinavyotumika wajumbe walitaka kupata ufafanuzi, lkini pia kulikuwa na hoja kwa nini bajeti ya tume ya ukimwi imevimba sana ukilinganisha na idara nyengine za ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, lakini pia kulikuwa na masuala jinsi gani tume inasaidia katika shughuli za kupunguza maambukizo kwenye maeneo ya utalii.

Vile vile kulikuwa na hoja kwamba wajumbe walitaka kujua mafanikio yaliyopatiana katika utekelezaji wa mkakati wa kwanza ambao umemalizika na

hivi sasa tunaingia katika mkakati wa pili, lakini pia kulikuwa na ushauri ambao umetolewa na waheshimiwa wjumbe.

Mhe. Spika, naomba sasa uniruhusu nizungumzie mambo haya kama ifuatavyo. Kuhusiana na mikusanyiko kama kwenye matamasha na mikusanyiko mingine hata ya kidini, tume ya ukimwi mara nyingi hupokea maoni mbali mbali kushiriki katika mikusanyiko mbali mbali ikiwemo hii ya matamasha, pia katika mikusanyiko ya dini kama vile Ijitimai na hata katika mikutano ya kijamii yenye malengo mbali mbali, katika mikusanyiko hiyo tume hufanya mambo mawili yafuatayo.

Kwanza kuelimisha wananchi kwa lengo la kukinga maambukizi ya Ukimwi ikiwa ni pamoja na kugawa vipeperushi, lakini pia kutoa huduma ya kupima kwa wale wanaoshawishika kupima, kuhusiana na hali ya fedha Mhe. Spika, kama nilivyosema katika utangulizi hapo juu kama moja ya majukumu makubwa ya tume ni kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa program za ukimwi kwa ujumla wake. Fedha zikishapatikana hutumika kama ifutavyo.

Sehemu ya fedha hutumika kutekeleza yale majukumu ya msingi ya tume, majukumu hayo ni pamoja na utayarishaji wa sera na mikakati ya kitaifa mpango wa kitaifa wa ufuatiliaji wa mwenendo wa ugonjwa, miongozi mbali mbali ya kitaifa, lakini pia kuratibu tafiti katika eneo la ukimwi.

Lakini pia fungu la pili la fedha hupelekwa kwa wadau mbali mbali kwenye program za ukimwi, katika hili nina kiambatanisho na naomba nitoe mfano kwa njisi gani fedha zile zilizokuwa *consultative* katika tume ya Ukimwi kwenda katika maeneo mengine, lakini wajumbe watakuwa na nafasi ya kuliangalia zaidi.

Kunzia Julai, 2008 mpaka Juni, 2011 *Agakhan Foundation* imepatiwa 10,011, 173,000/= *Business collection Zanzibar* hizi ni *NGOs* ambazo zinashiriki katika mapambano dhidi ya Ukimwi, imepatiwa 12, 964,950/=

Wizara ya Elimu imepatiwa 92,375,000,
Wizara ya Kazi imepatiwa 3,558,000,
Wizara ya Afya imepatiwa 28,047,500,
Wizara ya Biashara imepatiwa 3,000,000,
Mkuu wa Wilaya ya Mjini imepatiwa 13,915,000,
Mkuu wa Wilaya ya Wete imepatiwa 12,622,050,
Mkuu wa Micheweni Pemba amepatiwa 6,623,250.
Mkuu wa Wilaya ya Chake-Chake wamepewa 12,557,000
Mkoa wa Mjini Magharibi wamepewa 22,179,000 na mfano ya hayo
Lakini vile ile kwa wenzetu wa *ZAPHA* $^{+}$ wamepata 267,046,248.

Mhe. Spika, madhumuni ya kusoma kiambatanisho hiki ni kuleta ufafanuzi ni juu ya jinsi gani matumizi ya fedha zile nyingi ambazo zipo katika fungu la ukimwi hasa katika shughuli za maendeleo, ni imani yangu wajumbe wamefahamu jinsi gani zinatumika.

Kuhusiana na bajeti ya ukimwi kuvimba Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo juu wadau wa Ukimwi ni wengi na wanainchaji nyezo, nyezo zenyewe zikiwa ni utaalam na fedha katika kutekeleza shughuli walizojipangia na fedha zao zote hupitia tume ya Ukimwi, hiyo ndio sababu bajeti ya Ukimwi kuonekana kuvimba. Aidha tatizo lenyewe la Ukimwi ni kubwa na linahitaji fedha nyingi hata hivyo imebainika kuwa fedha kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo katika siku za hivi karibuni zimeonekana kupungua kutokana na matatizo mbali mbali ya kiuchumi duniani.

Mhe. Spika, nilihudhuria mkutano wa viongozi wa juu kuhusiana na suala la Ukimwi wa Umoja wa Kitaifa hivikaribuni na wito ni kwamba, kila nchi iwajibike ione kwamba wao wana *responsibility* wenyewe kuangalia kwamba gonjwa hili la Ukimwi wanaweza kulidhibiti. Kwa sababu wenzetu ambao wanasaidia katika eneo hili nchi nyingi nazo zinakubwa na matatizo na baadhi yao tayari wameanza kurudisha mkono nyuma.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kupungua huko kwa fedha ni kwa ulimwengu mzima, katika hali hiyo nchi sasa zinapaswa kuongeza matumizi ya bajeti zao kufidia pengo linaloachwa wazi na wafadhili, na ndio maana hata mchango wa Serikali ya Mapinduzi katika bajeti hii imeongezeka japo kuwa ni kidogo, kutoka shilingi 44 milioni hadi shilingi 472 milioni.

Mhe. Spika, pamoja na kujua uhaba wa fedha tulioano, lakini serikali imeamua kuongeza fungu hili katika bajeti hii ya Ukimwi. Hili ni jambo la kijasiri na ofisi yangu inaipongeza sana serikali.

Kuhusiana na Ukimwi na maeneo ya utalii Mhe. Spika, Tume ya Ukimwi inasaidia taasisi mbali mbali katika kutayarisha mipango yao ya kupambana na janga hili la Ukimwi kwa sababu ya ukimwi kuwa ni mtambuka. Kila taasisi hutakiwa kuwa na mpango wa kupambana na Ukimwi katika sehemu za kazi.

Sekta ya Utalii nayo inapaswa kuwa na mpango kama huo, Tume ya Ukimwi imeshirikiana na inaendelea kushirikiana na sekta hiyo, ziko hoteli ambazo hivi sasa zinafanya vizuri katika utekelezaji wa program kama hizo na mfano mzuri ni hoteli ya Serena iliyopo Mambo Msiige katika Jimbo la Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mafanikio yaliyopatikana. Mhe. Spika, Waheshimiwa awlitaka kujua je, mafanikio gani yamepatikana katika mkakati wa kwanza wa kupambana na ukimwi.

Mkakati huo umeweza kudhibiti ongezeko la maambukizi hapa Zanzibar, hayo ni mafanikio makubwa. Kiwango cha maambukizi hapa Zanzibar katika kipindi chote kimebaki chini ya asilimia 1, hayo ni mafanikio. Tukumbuke kwamba Zanzibar ni kisiwa kidogo, lakini mabadiliko yanayotokea ni makubwa katika nyendo za wananchi wake. Utokaji na uingiaji wa watu umeongezeka sana, wenyeji na wageni. Hapa nataka kusema tusiangalie upande mmoja tu wa shilingi tukasema labda wageni yaani watalii ndio chanzo kikubwa cha kuenea kwa Ukimwi. Bali hata Wazanzibari nao wanaweza wakawa chanzo.

Mhe. Spika, katika hili na hasa tukiangalia kwa wenzetu tumeweza kuona kuwa kiwango cha Ukimwi kilipungua na baadaye kuongezeka kutokana na kuregeza kasi ya mapambano. Kwetu hapa tumeweza kudhibiti. Tunachotakiwa kufanya hivi sasa ni kuongeza kasi ya mapambano na sio kupunguza ili kufikia lengo la *New Zero Infection* iliyowekwa na Umoja wa Mataifa.

Uelewa wa wananchi wetu kuhusu Ukimwi kwa ujumla upo juu, kuhusu kwanini hauondoki ni suala zito. Hili linaambatana na watu kubadili tabia. Jambo ambalo linatukwaza sisi kama Afisi ni jambo la mtu mmoja mmoja. Pamoja na kwamba unyanyapaa bado unaendelea kuwepo kiwango chake ni cha kiasi gani kimepungua. Wapo wengi wanaishi na virusi vya Ukimwi na wamejitokeza hadharani na wanafanya kazi nzuri ya kuelimisha wengi wenye virusi na wasio na virusi.

Pia taasisi nyingi zimeanzisha mipango ya kupambana na Ukimwi katika sehemu zao za kazi. Pia ushiriki wa viongozi wa dini umeimarika na mchango wao ni mkubwa katika kuelimisha jamii katika ngazi zote mpaka katika madarsa.

Mhe. Spika, kwa sababu waliochangia kwenye eneo hili ni wengi naomba tu kwa hapa niseme kwamba ushauri uliotolewa unachukuliwa. Pia rai ya kwamba fedha hizi za wafadhili zisimamiwe vizuri, tunalichukua. Naomba niwajulishe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba fedha hizi nazo Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali ana fursa ya kuziangalia na anakuwa anaziangalia.

Sifa moja iliyopata Tume ya Ukimwi ni kuwa wanaendelea kupata maksi nzuri kwa wale ambao wanatumia fedha za wahisani. Ndio maana wanaendelea kupata fedha hizi. Waheshimiwa Wajumbe niwatoe wasi wasi. Hapa hakuna

ubadhilifu wa fedha ambao umetokea mpaka muda huu. Lakini kama angalizo Afisi itajitahidi kuona kwamba fedha zinatunzwa vyema.

Mhe. Spika, naomba sasa nimalizie kwa kuliangalia suala la madawa ya kulevya. Hapa

1) Mhe. Makamo Mwenyekiti
2) Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa,
3) Mhe. Rashid Seif Suleiman,
4) Mhe. Ismail Jussa Ladhu

Waheshimiwa wengine, Karibu wote walizungumzia masuala haya. Katika ushauri serikali tumepewa kujenga kituo kwa ajili ya wateja wa dawa za kulevya ili kwenda sambamba na kukidhi matakwa ya sheria ya udhibiti wa dawa za kulevya. Pia tumeshauriwa serikali itenge fedha kwa ajili ya huduma za *sober house* na uimarishaji wa ulinzi katika viwanja vya ndege na bandarini. Mhe. Spika, ushauri tumeupokea Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ipo katika hatua ya kufanya juhudi za makusudi ili kuona kwamba kituo cha tiba na marekebisho kwa ajili ya wateja wa dawa za kulevya kwa kushirikiana na taasisi nyengine zinafanikiwa ili kwenda sambamba na matakwa ya sheria. Aidha afisi yetu imetenga Bajeti kwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kusaidia *sober houses.*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu alikuwa anasuala kwamba mchango wa serikali kwa *Sober House* ana wasi wasi kwamba serikali labda haina mkono wake katika kusaidia kama tulivyoandika katika hotuba yetu.

Mhe. Spika, harakati za huduma za malazi kwa vijana wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya ni matokeo mashirikiano kati ya Idara ya Kupambana na Madawa ya Kulevya na taasisi ya Afya ya jiji la *Detroit* nchini Marekani kupitia kituo cha *Detroit Drug Recovery Programme*. Watendaji wa Idara yetu pamoja na vijana ambao waliacha matumizi ya dawa za kulevya, walifanya ziara maalum ya mafunzo nchini Marekani kwa ajili ya kuona *programme* za kuachana na matumizi ya dawa za kulevya zinazoendeshwa na vijana walioacha matumizi ya dawa hizo.

Matokeo ya ziara hiyo na mafunzo mbali mbali ya *program* za kuachana na madawa ya kulevya kupitia mafunzo yaliyofadhiliwa na. Taasisi ya *Meringue International Health Aliance* hapa Zanzibar ambayo iliwashirikisha vijana walioacha dawa za kulevya wanaendesha *programme* hizo katika vituo mbali mbali vya *Sober House*. Aidha Afisi yetu kwa kushirikiana na vijana hao na wadau wengine imeandaa muongozo maalum kwa ajili ya uendeshaji wa

huduma katika vituo hivyo. Afisi yetu kupitia Tume ya Ukimwi imetenga jumla ya shilingi Milioni 47 kwa ajili ya huduma katika *Sober Houses*.

Mhe. Spika,

1) Mhe. Abdalla Juma Abdalla
2) Mhe. Mgeni Hassan Juma
3) Mhe. Asha Abdu Haji
4) Mhe. Salmin Awadh Salmin
5) Mhe. Rufai Said Rufai
6) Mhe. Asha Bakari Makame
7) Mhe. Abdalla Suleiman Ali
8) Mhe. Abdi Mosi Kombo
9) Mhe. Nassor Salim Ali
10) Mhe. Salim Abdalla Hamad
11) Mhe. Mussa Ali Hassan,
12) Mhe. Asha Abdu Haji
13) Mhe. Wanu Hafidh Ameir na
14) Mhe. Fatma Mbarouk Said

Wao walitaka kuona kuna mikakati gani ambayo serikali imeandaa katika kukabiliana na dawa za kulevya. Vile vile wako waliozungumzia katika hao sheria iliyokuwepo imepitwa na wakati na adhabu iongezwe, maeneo ya Bandari na *Air Port* yadhibitiwe. Pia vijana walioachwa na wanatoka *Sober House* kupatiwa mafunzo ya Kazi za Amali ili waweze kujiendeleza kimaisha.

Afisi yetu ina jukumu kubwa la kuratibu harakati za mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini kwa kushirikiana na taasisi husika mbali mbali. Afisi yetu tayari imefanya juhudi za makusudi za kuonana na taasisi husika mbali mbali katika kushajihisha juu ya kuongeza kasi katika mapambano dhidi ya dawa ya kulevya.

Aidha Afisi yetu imo katika mchakato wa mapitio ya sheria ya udhibiti wa madawa ya kulevya Zanzibar ili kuona kwamba sheria hiyo inawezesha kufikia malengo ya kutokomeza janga hili.

Afisi yetu tayari imeshawasiliana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ili kuona vijana wanaotoka *Sober House* wanapata fursa ya kujiendeleza kwa kupatiwa mafunzo ya amali. Aidha afisi yetu tayari imeshawapatia mafunzo ya awali ya kompyuta jumla ya vijana 25 walioacha matumizi ya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, naomba nimalizie sasa kwa waliochangia Mhe. Salum Abdallah Hamad alikuwa anasuala lake maalum kuhusiana na kunguru. Naomba tufahamu kwamba kunguru sio ndege wa asili hapa Zanzibar. Ndege hawa waliletwa kwa ajili ya kusaidia usafi wa mji. Hata hivyo kunguru hao hao wamegeuka na kuwa tishio kwa ndege wenye asili ya Zanzibar, mifugo na mazao ya kilimo.

Kuendelea kuwepo kwa kunguru hawa kunatishia uhai wa Bio Anuwai wa Zanzibar Kutokana na tishio hilo serikali imeona ipo haja ya kuwaondoa ndege hao. Na kwa kuwa ndege hao wameletwa kwa usafi hivyo njia pekee ni kuimarisha usafi wa mazingira pamoja na uhifadhi wa utupaji wa taka ovyo. Jambo hili linahitaji kila mmoja wetu kubadili tabia na kushiriki katika usafi wa mazingira. Kutakuwa hakuna athari kubwa ya kimazingira kwa kuondolewa kunguru hapa Zanzibar. Isipokuwa tu itasaidia kuimarisha Bio Anuwai zetu.

Mhe. Salum pia alizungumzia kuhusu kusaidiwa kwa *NGOs* za mazingira. Mhe. Spika uwezo ukiruhusu basi serikali itajitahidi kusaidia *NGOs* mbali mbali za kimazingira. Hata hivyo natoa wito kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili Tukufu Wawakilishi lakini pia na Wajumbe, wajitahidi kuzisaidia *NGO's* zetu ili yale mambo mazuri ambayo wameyafikia yasipotee.

Kuhusiana na suala la Maruhubi, Mhe. Spika kweli eneo hili ni miongoni mwa maeneo yaliyoathiriwa kutokana na uchimbaji wa mchanga. Kutokana na athari zilizokuwepo ikaonekana ili kuweza kufikia eneo hili basi Manispaa waruhusiwe kufukia mashimo kwa kutumia taka na baadaye taka hizo zifukiwe kwa kutumia mchanga. Afisi yangu inaahidi kulifuatilia suala hili kwa uongozi wa Baraza la Manispaa ili tatizo hili liweze kuondoka.

Mhe. Spika, makofi haya yanaashiria kwamba majibu yametosheleza. Na naomba nishukuru sana na niombe tena Mhe. Spika, kupitia kwako, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kama ambavyo waliunga mkono, waendelee kuiunga mikono bajeti hii na waipitishe bila ya kikwazo chochote. Labda kama kuna ufafanuzi kidogo unatakiwa nipo tayari kutoa ufafanuzi. Nawasihi tena nakuombeni muipitishe bajeti hii kwa lengo la kuisaidia jamii yetu, nakushukuru.

Mhe. Spika, sasa naomba rasmi kutoa hoja.

(*Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri amejaribu kutumia muda mkubwa ili kutoa ufafanuzi, mambo yalikuwa mengi. Hapana shaka hilo tunalielewa na amejitahidi sana. Sasa waheshimiwa wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 06 - OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS

Kifungu 901	Idara ya Mazingira	9,000,000
Jumla ya Fungu		**9,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 06 – OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS

Kifungu 301	Afisi Kuu Pemba	214,115,000
Kifungu 401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilitaja kwamba Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 92 inaelekea imepitwa na wakati sana. Na hata Mhe. Waziri alionesha dalili kwamba labda kunakuja sera mpya. Je hili jambo alilisahau naomba anipe ufafanuzi kwamba kuna sera mpya iliyotayarishwa na ambayo hakuitolewa ufafanuzi au sera ndio hii, hakuna matarajio yoyote ya kutolewa Sera Mpya ya Mazingira kwa vile sera hii iliyokuwepo imepitwa na wakati. Naomba ufafanuzi Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuombe radhi Mhe. Rashid Seif, ni kweli alitaka ufafanuzi juu ya hilo. Lakini muda ndio uliobana nilikuwa sijamfikia.

Ni kweli ofisi yetu ipo katika mchakato wa kurekebisha sera ili kupata sera mpya na hatimaye kuandaa mkakati wa utekelezaji wa sera hiyo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, mchakato ni jambo kubwa, jambo ambalo halina mpaka. Hebu anieleze hasa ni lini itapatikana hii sera mpya.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuahidi Mhe. Rashid Seif, kwamba sera hii haina muda tena kwa sababu ipo katika hatua za mwisho. Imani yangu kwamba mwanzoni au mwishoni mwa mwezi ujao sera hii itakuwa tayari.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika tuendelee.

Kifungu 401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	15,001,000
Kifungu 501	Idara ya Uendeshaji wa Utumishi	704,204,000

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia suala la Ofisi hii ya Faragha ya Makamo wa Kwanza hasa katika suala la huduma kwa makamo wa kwanza. Namshukuru Mhe. Waziri amenipa majibu mazuri ya kutosheleza. Hoja yangu ni ndogo tu.

Katika majibu yake amesema huduma hizi zote zinashughulikiwa chini ya fungu hili la Idara ya Uendeshaji na Utumishi nikilitizama hapa jumla yake ni shilingi mia saba na nne milioni mia mbili na nne elfu.

Mhe. Mwenyekiti nilikuwa nataka waziri atusaidie kwamba ninapolinganisha hili na kwa mfano na Ofisi ya Makamo wa Pili, nitafanya hivyo kwa sababu ndio karibu pa kuweza kulinganisha. Unakuta Idara ya Utumishi katika Afisi ya Makamo wa Pili ina jumla ya shilingi mia tatu na thalathini na sita milioni laki tisa tisini na tatu elfu na Idara ya Huduma za Makamo wa Pili ambazo zimetajwa *specifically* ina mia mbili thamanini na tano milioni laki nne na elfu nne. Jumla yake itakuwa mia sita na ishirini na mbili milioni mia tatu tisini na saba elfu, kwa hayo mambo mawili.

Sasa kwa sababu hapa Ofisi ya Makamo wa Kwanza jumla ya fungu hili ni mia saba na nne milioni mia mbili na nne elfu, linazidi hata hili ambalo limewekwa katika Afisi ya Makamo wa Pili. Nilikuwa naomba Waziri atupe uhakikisho wa kuligawa fungu hili ili tujue shughuli zinazohusika na Idara ya Huduma za Makamo wa Kwanza ni kiasi gani, ambalo litasimamiwa moja kwa moja na Afisi ya Faragha na zile ambazo zitasimamia kwa ujumla shughuli za uendeshaji na utumishi ni kiasi gani turidhike kwamba shughuli za Makamo wa Kwanza hazitokuwa zimejumlishwa katika shughuli nyengine lakini zitakuwa zimetenganishwa kama zilivyo kwa Afisi ya Rais Ikulu na zilivyo kwa Afisi ya Makamo wa Pili. Naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais napenda kutoa ufafanuzi juu ya suala ambalo limeulizwa na Mhe. Jussa kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Mwakilishi atakumbuka vizuri Mhe. Waziri alipokuwa anatoa ufafanuzi alieleza kwa kina kwamba Ofisi ya Faragha ya Mhe. Mkamo wa Kwanza wa Rais ndio tunaijenga. Katika steji hii isingekuwa rahisi kuweza kusema kwamba baadhi ya fedha ziwekwe kule ili aelewe hasa kiasi gani kitakwenda katika Afisi ya Faragha. Kwa sababu unapojenga hujui utatumia kiasi gani.

Mimi namuomba Mhe. Mwakilishi astahamili kwanza tuweze kuijenga na tuone kwamba tukishakuikamilisha kiasi gani cha fedha kitakachohitajika katika bajeti ya mwaka ujao ndio ataweza kuona hasa ni kiasi gani kitaweza kuhitajika. Hivi alivyoweka Mhe. Waziri nadhani itakuwa ni uzuri zaidi kwa sababu ataweza kutumia zaidi kuliko hata vile Mhe. Mwakilishi angependa iwe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti namuelewa Mhe. Waziri wa Nchi anayeshughulikia Fedha lakini hoja yangu ni kwamba najua kwa jumla bado *accounting officer* kwa ofisi nzima ataendelea kuwa Katibu Mkuu. Lakini kunakuwa na urahisi wake katika matumizi hasa unapohudumia ofisi kubwa kama hizi yanapotenganishwa. Nakubali kwamba ofisi hii inajengwa lakini Afisi hii ya Makamo wa Kwanza imeanzishwa tangu mwezi Novemba. Bila shaka kama inataka kujengwa itakuwa hawajakamilishwa watu wa kuteuliwa lakini nafasi gani zinapaswa ziwepo pale na huduma zake nyengine nadhani lingekuwa linaeleweka kabisa.

Nilikuwa nataka nipewe kauli tu kutoka upande wa Serikali. Nikishakupewa kauli hiyo nitaruhusu tuendelee kwamba itakapokamilika ofisi hii patatengenishwa ili tutakapokuja kuripotiwa mwakani katika matumizi ya fungu hili tujue hasa Ofisi ya Makamo wa Kwanza shughuli zake zilikuwa ni zipi na fungu lake lilikuwa mbali na shughuli za jumla za Wizara katika Mambo ya Uendeshaji na Utumishi zitakuwa ni zipi. Kwa hivyo nataka kauli hiyo halafu niliruhusu fungu liendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba tukishakuimaliza kuijenga hii Ofisi tutaliarifu Baraza lako Tukufu kwamba majukumu yake ni nini na mwaka wa kesho ataona bajeti ya Afisi hii imekaa peke yake na inajitegemea. Hilo tunamuahidi tutalifanya.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nimeridhika na naomba tuendelee.

Kifungu 501	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	704,204,000
Kifungu 601	Idara ya Madawa ya Kulevya	142,527,000
Kifungu 901	Idara ya Mazingira	

Mhe. Salmin Awadh: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri katika Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa kujibu hoja nyingi za Waheshimiwa Wajumbe, lakini kuna hoja moja kidogo pengine ameisahau au mimi sikusikia. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri basi anipe kidogo majawabu ili na mimi niweze kujua.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia hoja ya Mhe. Waziri katika maeneo ya mazingira nilionesha wasi wasi wangu juu ya takwimu alizozitoa za mifuko ya plastiki ambayo imekamatwa. Ambapo kwa mujibu hotuba ya Mhe. Waziri ametaja tu kiasi cha tani 68 za mifuko ya plastiki zilizokamatwa katika maeneo ya Bawe na Rasi Shangani, lakini hakutueleza ni tani ngapi za mifuko ya plastiki ambayo imekamatwa katika maeneo mbali mbali. Zaidi ukizingatia kwamba mifuko hii ya plastiki inaonekana imeenea na wakati mwengine inakamatwa.

Ningemuomba Mhe. Waziri hebu atueleze kiasi cha mifuko mengine ambayo imeweza kukamatwa pengine na kuangamizwa au pengine wahusika waliopelekwa Mahakamani na hukumu ambazo zimetolewa juu ya wale waliokamatwa na mifuko ya plastiki.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti ni kweli wakati akichangia hoja ya ofisi yangu Mhe. Salmin Awadh Salmin alitaka ufafanuzi juu ya hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na muda finyu ambao ofisi yangu imepata katika kujiandaa kujibu hoja za waheshimiwa Wajumbe naomba nimtake radhi sana Mhe. Salmin Awadh Salmin kwamba suali lake lilihitaji kwenda kufanyiwa utafiti wa takwimu ambao kwa usiku mmoja ambao nimepata watendaji wangu hawakuweza kulifanya. Lakini niko tayari kuliarifu Baraza lako na kumletea kwa maandishi kwa siku za mbele zinazofuata.

Mhe. Salmin Awadh: Mhe. Mwenyekiti, inaonekana Mhe. Waziri katika hili hakuwa makini. Na kwa sababu mara nyingi wakati wa vikao vinavyoendelea mara nyingi tunawataka Wakurugenzi wa Idara, Makatibu Wakuu na wote wanaohusika wawepo hapa, ili waweze kusikia yale maendeleo yanayoendelea.

Mimi naamini kama Mkurugenzi anayehusika na Wizara hii au Katibu Mkuu angekuwepo angepata muda tosha, kwa sababu mimi nimechangia jana tokea wakati wa mchana kama Mhe. Mwenyekiti, unakumbuka. Sasa inasikitisha kuona kwamba jambo hili halikuweza kupata ufafanuzi. Lakini naomba sana Mhe. Waziri wakati Baraza hili linapoendelea wahusika wa Wizara zinazohusika wawepo hapa ili waweze kutoa ufafanuzi kwa wananchi juu ya masuala yanayoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Kifungu 901 Idara ya Mazingira

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kwa niaba ya watu wa Kiwani naomba niseme tu kwamba kauli yangu ya kutokuiunga mkono Bajeti hii nimeiondosha na naunga mkono bajeti hii.

Lakini pamoja na kumuheshimu mama na kwamba ofisi yake ni changa, lakini nazingatia sana matatizo ya watu wa Muambe kimazingira. Mhe. Mwenyekiti, naomba basi anisaidie miradi ya ujenzi wa barabara, gati na mambo mengine. Serikali hupatiwa asilimia 10 ya uharibifu wa mazingira. Nilitegemea kwamba Idara ya Mazingira Unguja na Pemba hizi fedha zinapatikana ili iwezeshe kufanya ufatiliaji. Katika hili anisaidie fedha hii inakwama wapi ili wale wenzetu wa mazingira isiwafike wakaenda huko huko vijijini kuangalia hali ya uharibifu wa mazingira.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa suala la Mhe. Hija wa Jimbo la Kiwani kama ifuatavyo.

Ni kweli wakati wa kufanya shughuli za maendeleo Kampuni ambazo zinaingia mkataba labda wa kujenga barabara na kufanya mambo mengine huwa wanatakiwa kuweka kama *deposit* asilimia 10 ili kama kutakuwa na uchafuzi wa mazingira fedha hizo ziweze kutumika na hata kama hazikutosha mkataba unataka waweze kuongeza ili kufanyiwe ukarabati katika eneo ambalo limeharibiwa kimazingira.

Naomba nimuahidi sana Mhe. Mwakilishi kwamba ofisi yangu itajitahidi sana kuona kwamba asilimia 10 hiyo inapatikana kutokana na watu ambao wanaendeleza miradi ili shughuli za marekebisho zifanywe. Lakini suala lake kubwa linahusiana na kuharibiwa mazingira katika eneo la Mwambe.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Mwakilishi ataona jitihada za ofisi yangu na za serikali katika kuona kwamba eneo lile ambalo limeharibiwa mazingira linaweza kurekebishwa. Mhe. Mwenyekiti, tayari timu za wataalamu zimekwenda huko na ni imani yangu kama wakati huo alikuwa katika jimbo atakuwa ameziona, mipango pamoja na miradi mbali mbali inaandaliwa ili kuona jinsi gani mazingira yale yataweza kuboreshwa katika eneo lake.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli timu za wataalamu zitakwenda Mwambe hata Mhe. Rais amekwenda Mwambe, Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais pia amekwenda na hata Waziri wa Kilimo amekwenda Mwambe na wameiona hiyo hali. Mhe. Mwenyekiti, wataalamu wanafanyakazi usiku na mchana kuona kwamba ile hali iliyoko Mwambe inaondoka, hivi sasa kuna ujenzi wa barabara sita za Kusini Pemba na kifusi chote kinatumika kutoka Mwambe. Mhe. Mwenyekiti, ili tukubaliane Mhe. Waziri tungekaa na watu wa mawasiliano ukaniambia ni shilingi ngapi ambazo pale zinaatikana ili watu wa Idara ya Mazingira wazipate zile fedha wasaidiwe kufukia. Lakini kuwapeleka wataalamu tu kuona kwa macho ni kuwasaliti na kuwalaumu.

Kwa hivyo, mimi ushauri wangu ni kwamba haja yangu ni fedha inaingia wapi ili wataalamu wetu tuwatume baadae ndio tuwalaumu kwamba nyinyi wazembe lakini fedha ipo. Mhe. Mwenyekiti, kumpeleka mtaalamu nadhani utampeleka miaka 40 na hana atakalolifanya, ninachoomba kukijua mimi ni lini nikaa kama mwakilishi wa Jimbo la Kiwani pamoja na yeye na watu wa Mawasiliano wakaniambia hasa kwamba figer hii ndio malipo ya fidia ya Mwambe na wataalamu hiyo wafanyie kazi. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tangu mwaka 1999 tumejenga gati ya Mkoani, tumejenga barabara ya Mkoani-Makombeni, Mtuhaliwa-Chokochoko na sasa barabara sita za Kusini Pemba lakini watu wa Mwambe hawajapata hata shilingi moja ya fidia, hivyo zinakwenda wapi fedha hizi?

(Baraza lilirudia)

HOJA YA KUONGEZWA MUDA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa shughuli iliyo mbele yetu haijamalizika tunahitaji kuongeza muda kwa hiyo naomba tutengue kanuni ya muda na Baraza lako liridhie ili tuweze kumaliza shughuli iliyo mbele yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nimekubali ushauri ambao Mhe. Mwakilishi ametupa ofisi yangu itakaa pamoja na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na yeye tutampa taarifa na hata kumualika katika mazungumzo yetu hayo ili kutafuta ufumbuzi wa jambo hili.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Waziri na kwa vile na Naibu Waziri yuko karibu na mimi tutakwenda kutembelea huko.

Kifungu 901

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, na mimi katika mchangio wangu jana nilipokuwa nachangia hapa nilitaka kujua juu ya bandal zile za mifuko ya plastik iliyokamatwa kesi zake zimefikia wapi kwa sababu mifuko ile iliachiwa wakapewa wenyewe nilimtaka Mhe. Waziri akija hapa atueleze lakini sikupata maelezo mazuri juu ya suala hili. Kwa hivyo, nilikuwa nataka ufafanuzi katika hili.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu wawe wanabakia humu ndani ya ukumbi ili kufuatia yanayoendelea humu ndani ya ukumbi. Naomba sana Mhe. Mwakilishi kwa maelezo ya kina aweze kutafuta hansard lakini Mhe. Mwanasheria Mkuu jana alieleza kwa urefu sana suala hili na kwa kweli ni suala refu na pana ambalo tukianza kulielezea tena sasa hivi litachukua muda mrefu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, bado sijamfahamu Mhe. Waziri maelezo yake.

Mhe. Mwenyekiti: Labda nimsaidie alivyosema, anasema kwanza ameomba sana kwa heshima zote kwamba wajumbe wawepo ndani ya ukumbi kwa sababu ufafanuzi huwa unatolewa hapa na pale tena sio yeye peke yake lakini katika hili Mhe. Mwanasheria Mkuu jana alilieleza kwa pana na vya kutosha. Kwa hivyo, kama wakati huo ungekuwepo ufafanuzi ambao pia nakubaliana nao basi ingekuwa hii imetosha kuwa ni ufafanuzi wake. Kwa hivyo, anachoomba ni kwamba ufuatilie hansard hilo jibu utalipata.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na hayo.

Kifungu 901	Idara ya Mazingira	239,158,000
Kifungu 2101	Idara ya Watu wenye Ulemavu	177,995,000
	Jumla ya Fungu	**1,493,000.000**

FUNGU 12 - TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Kifungu 201 Utawala Unguja

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa mara nyengine tena naomba nimshukuru pia Mhe. Waziri kwa maelezo yake ya kina katika fungu hili ambalo nilikuwa mmoja katika watu waliolihoji. Mimi kwa jumla nataka niseme nimeridhika na maelezo yake isipokuwa kuna fungu moja baadae huko mbele tutafika katika fungu la maendeleo, lakini katika hapa nina hoja ndogo tu. Mhe. Mwenyekiti, kwenye Utawala Unguja kwenye 220200 kuhusu viburudishaji.

Mhe. Mwenyekiti, nimepata mshituko kidogo hapa viburudishaji ni shilingi 21,900,000. Mimi nilikuwa najaribu kulinganisha nasema sijui wanakunywa nini huko kwenye Tume ya Ukimwi kwa sababu nilikuwa nalinganisha na maeneo mengine ambayo nilitegemea labda yanalingana, lakini pia kuna ofisi kubwa kubwa tu. Kwa mfano, Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia Ofisi ya Makamo wa Pili kwenye huduma viburudishaji vyake mwaka mzima ni milioni 4, Idara ya Uratibu ambayo inafanya shughuli kubwa sana katika Ofisi ya Makamo wa Pili viburudishaji ni milioni 2. Lakini hata Ofisi ya Makamo wa Kwanza viburudishaji Idara ya Mipango ni milioni 3 na laki 1. Lakini hapa Mhe. Mwenyekiti, kuna milioni 21

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri naweza kuambiwa ni semina lakini nasema semina hizo zinakuwa zinafanyika hapa Unguja tu kwa sababu nikilinganisha hiyo hiyo na ya Pemba katika kifungu kinachofuata hatujafika tunalinganisha tu, Pemba unakuta kuna 2 na laki 4. Kwa hivyo, hili fungu la viburudishaji na vitafunwa na kila kitu naomba maelezo kidogo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kama nilivyotoa kwenye maelezo kwamba kazi kubwa ya Tume ya Ukimwi ni kuratibu katika ngazi ya kitaifa shughuli zote za mapambano dhidi ya gonjwa la ukimwi. Fedha hizi zinazoonekana hapa Mhe. Mwenyekiti, ni kwa ajili ya kuwahudumia katika kuratibu huko saa nyengine kunahitaji kufanywa mikutano na semina mbali mbali, fedha hizi ni kwa ajili hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini Pemba kuna fungu dogo siwezi kusema hapa ndio Makao Makuu ya Nchi lakini *activities* nyingi zinafanyika Unguja na wale ambao wanaotoka Pemba wanahudumiwa katika kasma hii.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nipewe maelezo zaidi katika hili kwa sababu nilivyodhani mimi na kama sivyo naomba anirekebishe yeye Mhe. Waziri na nikielewa kama kawaida yangu sina matatizo. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba nilidhani haya mafungu yanayohusu masuala ya semina kwa upande wa Tume ya Ukimwi yako katika fungu lile la maendeleo, lakini hapa pana shughuli za utawala nilidhani haya yanahudumia shughuli zao za jumla katika maofisi yao na ndio maana nilitaka nisaidiwe kwamba kwa utawala Unguja kuna 21 milioni, lakini utawala Pemba ni milioni 2 na laki 4.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimesema ukilinganisha na ofisi nyengine hailingani na kasma hii kubwa iliyoko kwenye viburudishaji. Kwa hivyo, mimi naomba nisaidiwe kwamba semina zinaingia hapa au programu hii ya semina ndio shughuli zenyewe za maendeleo za Tume ya Ukimwi ambazo zinapatikana katika hili fungu la maendeleo. Naomba tusaidiwe zaidi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, napenda kidogo kutoa ufafanuzi kwa Mhe. Mwakilishi. Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Ukimwi moja ya jukumu lake ni kuwahamasisha Wazanzibari waachane na vitendo ambavyo vinaongeza ukimwi. Sasa katika suala hilo Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima la mikutano, na kuna suala zima la semina.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mikutano na semina kama utaifanya Unguja na ukaifanya na Pemba gharama zinaweza zikawa ni kubwa zaidi. Kwa hivyo, hii wamei-*centralize* wameweka fedha zake Unguja kwa maana ya kwamba itakapotokea mikutano na semina ndugu zetu kutoka Pemba basi huwa wanaalikwa wanakuja wanashiriki na hizi fedha zinatumiwa na wote. Kuhusu suala la mikutano na semina kama ni *contribution* ya serikali mara nyingi linakuwa katika sehemu ya utawala. Kwa hivyo, ndio akazikuta hapo na hapo ndipo pahala pale penyewe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika naomba tuendelee.

Kifungu 201	Utawala Unguja	378,948,000
Kifungu 301	Ofisi Kuu Pemba	93,052,000
Jumla ya Fungu		**472,000,000**

FUNGU 06 – OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa mara nyengine tena katika mchango wangu nilihoji katika majumuisho ya Mhe. Waziri sikubahatika kulisikia la kama itakuwa nimeghafilika atanielekeza kwenye hansard nitashukuru. Katika ukurasa wa 26 wa hotuba yake kulikuwa na programu pale tulisema nane katika mchango wangu nimezitaja, lakini nilisema nikiangalia kwenye fungu hili linalohusu shughuli za maendeleo katika Ofisi ya Makamo wa Kwanza tumekuta kuna mafungu mawili tu yaliyotengewa fedha ambayo ni mitego ya kunguru ni milioni 50 na mradi wa usimamizi wa maji taka ni milioni 30. Kwa hivyo, nilikuwa naomba maelezo kwamba hii miradi mengine ambayo imetajwa hapa katika ukurasa wa 26 wa hotuba yake inategemewa ipate fedha zake wapi katika kutekeleza miradi hii ya maendeleo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Mwakilishi alitaka ufafanuzi juu ya hilo na nimuombe radhi kwamba kwa sababu ya wakati tu basi sikuweza kumpa ufafanuzi huo. Lakini ni kweli kama alivyosema katika fungu la mazingira fedha za maendeleo zilizopo ni milioni 50 kwa ajili ya mradi wa kunguru lakini pia milioni 30 kwa ajili ya mradi wa maji machafu Chake-Chake Pemba. Kwa hivyo, namuomba nimpe taarifa kwamba haya aliyoyaona hapa kuanzia namba moja mpaka nane ambayo hayakutengewa matumizi ya shughuli za maendeleo hizi ni kazi za kawaida za idara na zinahudumiwa chini ya fungu lile ambalo tunaliomba pale la shilingi milioni 239, 158,000 la idara hii.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

FUNGU 06 – OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS

Kifungu 401	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	155,000,000
Jumla ya Fungu		**155,000,000**

FUNGU 12 – TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Kifungu 201	Utawala Unguja

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ambayo naamini inshaallah itakuwa ya mwisho. Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba ya Mhe. Waziri ukurasa wa 30 kifungu Nam. 67 pale juu aliliomba Baraza kuidhinisha jumla ya shilingi milioni 472,000,000 kwa shughuli za kawaida, shilingi 90 milioni ikiwa ni mchango wa serikali kwa shughuli za maendeleo na shilingi bilioni 1,300,000,000 ikiwa ni mchango wa washirika wa maendeleo kwa mwaka wa fedha. Mhe. Mwenyekiti, hapa katika shughuli za maendeleo tunaziona hizi milioni 90 tu, hizi bilioni 1, 300,000,000 ambazo

ameliomba Baraza liidhinishe sikuziona katika sehemu ya *foreign grand's* katika sehemu, tena nimejaribu kupekuwa sana kwenye kitabu sikuziona popote. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo katika hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli anayosema Mhe. Mwakilishi na kwa sababu kama unavyoelewa kwamba tulifanya masahihisho makubwa sana ndani ya hiki kitabu na kutokana na utaratibu wa kutoka wizara 13 kwenda wizara 16 ndio kidogo hiki kitabu kimebaraganyika, lakini tunaandaa kitabu chengine nakala safi na hiyo ambayo anaizungumza Mhe. Mwakilishi basi itakuwemo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika tuendelee.

Kifungu 201	Utawala Unguja	90,000,000

Mhe. Mwenyekiti: Haya sasa *foreign component* inatajwa kama alivyoomba katika kitabu.

Kifungu	Utawala Unguja	1,300,000,000

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Ofisi ya Makamo wa Rais kifungu kwa kifungu bila ya mabadiliko, naomba sasa kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makisio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe si kuna marekebisho tuliyafanya hapa, Mhe. Waziri samahani kuna ile *foreign component* tumekubaliana kwamba itaingia kwenye kitabu ndio marekebisho yenyewe.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais pamoja na kufanya mabadiliko naomba sasa kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makisio hayo pamoja na mabadiliko yake. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na makisio hayo pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Nakushukuruni Waheshimiwa Wajumbe, tuliongeza muda kwa sababu ya kumaliza kazi hii, nakushukuruni kwamba mmekubali kuongeza muda huo na sijui kama kuna shughuli nyengine katika hii.

(Saa 7:20 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa Mwaka wa fedha 2011/2012

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu, likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili, kuzingatia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha, ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa wazima na wenye afya njema pamoja na kunipa nguvu ya kuweza kuwasilisha mbele ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa Fedha 2011/2012. Shukrani zangu za dhati nazitoa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri katika Ofisi yake yaani Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, tumshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kumaliza uchaguzi mkuu wa Oktoba 2010 kwa salama na amani. Kama kawaida yetu uchaguzi huo ulikuwa ni kielelezo tosha cha kuimarika demokrasia Zanzibar na taarifa zinaonesha kuwa asilimia 89 ya waliojiandikisha walijitokeza kupiga kura. Nachukua fursa hii adhimu kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar wa awamu ya saba. Kuchaguliwa kwake kunatokana na imani kubwa walionayo wananchi wa Zanzibar katika kuwatumikia na kuwaletea maendeleo. Namuomba Mwenyezi Mungu ampe afya njema ili aweze kutekeleza majukumu yake na kutimiza ahadi alizozitoa kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa namna ya pekee naomba kutumia nafasi hii adhimu pia kumpongeza Mhe. Dk. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Dk. Mohammed Gharib Bilal kuwa Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia uchaguzi mkuu uliofanyika mwezi wa Oktoba 2010. Ni matumaini yetu kwamba kuchaguliwa kwao kutazidisha uimara wa Muungano wetu ikiwa ni pamoja na kuzishughulikia changamoto zake. Namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekima na busara katika kuwatumikia wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamo wa Pili wa Rais kwa kuteuliwa kushika nyadhifa hizo. Uteuzi wao umewafurahisha wananchi wa Zanzibar na wana matumaini kuwa watamsaidia na kumshauri kwa karibu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kupeleka mbele gurudumu la maendeleo na kuifanya Zanzibar yenye neema.

Mhe. Spika, pongezi zangu za dhati zije kwako wewe binafsi kwa kuchaguliwa tena kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi. Naamini uwezo na uzoefu wako katika kuliendesha Baraza la Wawakilishi ndiko kulikopelekea Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kukuchagua tena kushika wadhifa huu. Aidha, nampongeza Mhe. Ali Abdalla Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Vile vile nawapongeza Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa, Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni na Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mwakilishi wa Viti Maalum – Wanawake CCM kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Baraza hili tukufu. Kwa pamoja nakutakieni kila la heri katika kutekeleza majukumu yenu.

Mhe. Spika, natoa pongezi maalumu kwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zinazofanya kazi na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nazo ni Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura na Kamati ya Kusimamia Hesabu za Serikali inayoongozwa na Mhe. Omar Ali Shehe, Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake. Ushauri na miongozo yao mizuri imesaidia sana katika kufanikisha utekelezaji wa kazi zetu na tunawaahidi kuwa tutaendelea kutoa ushirikiano wetu wa hali ya juu kwao.

Mhe. Spika, kabla sijamaliza salamu zangu za pongezi, kwa heshima pia naomba uniruhusu kuwapongeza wananchi wa Zanzibar kwa kushiriki katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 2010 kwa salama na amani na kukichagua Chama cha Mapinduzi kuendelea kuongoza. Salamu zangu za pongezi na shukrani pia ziende kwa Tume ya Uchaguzi kwa kuandaa mazingira mazuri ya uchaguzi na

kwa vyombo vya ulinzi na usalama vyote kwa kuhakikisha kuwa amani na utulivu inakuwepo katika kipindi chote cha uchaguzi na baada ya uchaguzi.

Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Dimani kwa kuweza kunirudisha tena kuwa Mwakilishi wao katika Baraza hili tukufu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Bila ya shaka yoyote wameonesha imani na upendo mkubwa kwangu na nawaahidi kushirikiana nao kikamilifu kwa hali na mali katika kuleta maendeleo katika jimbo letu.

Mhe. Spika, matayarisho ya bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2011/12 yamezingatia mipango ya kisekta iliyowekwa katika Dira 2020, Malengo ya Maendeleo ya Milenia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA II) na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010-2015. Kipaumbele kimewekwa katika mambo yafuatayo:-

- Kuendeleza Umoja wa Kitaifa na mshikamano.
- Kuimarisha uwezo, utoaji wa huduma ikiwemo usafishaji wa miji na uendeshaji wa Serikali za Mitaa, Wilaya na Mikoa.
- Kuimarisha na kuongeza uwezo wa Idara Maalum za SMZ.
- Kuimarisha huduma bora katika Vyuo vya Mafunzo pamoja na kupunguza msongamano.
- Kuimarisha mfungamano wa Kikanda ili Wazanzibari waweze kutumia fursa za kiuchumi zinazotokana na Jumuiya za Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Jumuiya nyengine za Kikanda.
- Kuwashajihisha Wazanzibari wanaoishi nchi za nje katika kushiriki na kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
- Kutoa elimu ya kujikinga na Maambukizi ya UKIMWI na VVU.

MUUNDO NA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Spika, Muundo wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi unajumuisha ofisi, idara na vitengo 11 kama vifuatavyo:-

a) Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.
b) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
c) Idara ya Uendeshaji na Utumishi
d) Ofisi ya Faragha ya Rais
e) Idara ya Mawasiliano Ikulu
f) Kitengo cha Usalama wa Serikali (*GSO*)
g) Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho

h) Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Shughuli za Wazanzibari waliopo Nchi za Nje (*DIASPORA*).
i) Idara ya Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
j) Idara ya Uratibu Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
k) Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba

OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Spika, baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010 Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein aliunda Baraza la Mapinduzi lenye sura ya Umoja wa Kitaifa na kuwateua wajumbe 22. Baraza la Mapinduzi ndiyo chombo kikuu cha kumshauri Mhe. Rais. Shughuli za Baraza la Mapinduzi zinasimamiwa na Ofisi ya Baraza la Mapinduzi. Shughuli hizo ni pamoja na kuratibu na kusimamia vikao vyote vya Baraza la Mapinduzi. Katibu wa Baraza la Mapinduzi ambaye pia ndio Katibu Mkuu Kiongozi na Msimamizi Mmkuu wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi ambapo katika kutekeleza malengo yake husaidiwa na Sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi inayojumuisha Naibu Katibu wa Baraza la Mapinduzi, maafisa na watumishi wengine mbali mbali. Sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi pia inajukumu la kuratibu Vikao vya Kamati ya Makatibu Wakuu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iliidhinishiwa shilingi 534.9 milioni. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Ofisi imeingiziwa Shilingi 445.9 milioni sawa na asilimia 83 ya makadirio ya matumizi.

Mhe. Spika, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi imeandaa vikao 11 vya Baraza la Mapinduzi na kujadiliwa nyaraka mbali mbali. Katika nyaraka hizo pia zilihusisha Sheria nane na Sera moja. Miswada hiyo hatimae ilipitishwa na Baraza la Wawakilishi, kuwa sheria. Pia imeandaa vikao 13 vya Kamati ya Makatibu Wakuu. Vile vile, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi imewapatia mafunzo watumishi wake watatu katika ngazi ya Shahada ya Pili ya Utawala, Stashahada ya Juu ya Uhasibu na Stashahada ya Uzamili ya Uhasibu.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kwamba watendaji wanayaelewa na kuyatekeleza vyema majukumu wanayopangiwa, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iliandaa semina kwa ajili ya Viongozi wa Kisiasa wa Serikali na Watendaji Wakuu wa Serikali chini ya Uenyekiti wa Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Semina ya kwanza ya siku tatu ilifanyika kuanzia tarehe 5 Mei 2011 hadi tarehe 7 Mei, 2011 na kuhudhuriwa na Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu

wa Pili wa Rais. Semina ya pili ilifanyika kuanzia tarehe 24 Juni 2011 hadi tarehe 26 Juni 2011 katika ngazi za Makatibu Watendaji, Wakurugenzi, Maafisa Wadhamini, Makamishna, Wakuu wa Taasisi zinazojitegemea na Mashirika ya Serikali. Semina hizo zilikuwa na madhumuni ya kuwawezesha viongozi wa siasa na Watendaji Wakuu wa Serikali kuwa na mahusiano na mashirikiano mazuri na hatimae kuwa timu moja imara yenye ari kubwa ya kuwatumikia na kuwaletea maendeleo ya haraka wananchi. Pia semina hizo zililenga kuwafahamisha kuhusu misingi ya sheria, kanuni za uongozi, taratibu, maadili na uwajibikaji.

Mhe. Spika, semina hizo zilimalizika kwa ufanisi na maazimio kadhaa kupitishwa kwa madhumuni ya kuimarisha utekelezaji wa kazi na majukumu serikalini kwa lengo la kuongeza ufanisi. Viongozi walikubaliana kubadilika na kuacha kufanya kazi kimazoea na kikawaida (*business as usual*). Utendaji bora wenye manufaa kwa jamii umetiliwa mkazo kwa faida ya kila mmoja wetu. Wanasemina walionesha nidhamu ya hali ya juu kwa kuhudhuria kikamilifu, kuchangia ipasavyo na kushirikiana vizuri na watoa mada kwa kubadilishana fikra na mawazo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Baraza la Mapinduzi imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuimarisha Sekretarieti ya Baraza la Mapinduzi kwa kuipatia wataalamu mbali mbali na vifaa vya kufanyia kazi
- Kuandaa vikao 12 vya kawaida vya Baraza la Mapinduzi na vikao 48 vya kawaida vya Kamati ya Makatibu Wakuu pamoja na vikao vya dharura pale haja inapotokea. Vikao hivyo vyote ni kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya uandaaji wa Sera na Sheria.
- Kuwajengea uwezo wafanyakazi kitaaluma kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wanne katika fani za Sheria, Utawala, Uwekaji kumbukumbu, Katibu muhutasi na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi watatu katika fani za uandaaji miradi, uandishi wa taarifa za vikao na uhudumu.
- Kuandaa vitabu vya kumbukumbu za vikao vya Baraza la Mapinduzi pamoja na Vikao vya Kamati ya Makatibu Wakuu na kuhifadhi kumbukumbu hizo kwa njia ya elektroniki.
- Kulifanyia matengenezo makubwa jengo la Ofisi ya Baraza la Mapinduzi liliopo Forodhani kwa kutengeneza chumba kikubwa kwa ajili ya kuwekea kumbukumbu pamoja na kutengeneza Ofisi kwa ajili ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, ili Ofisi ya Baraza la Mapinduzi iweze kutekeleza malengo yake, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 836 milioni kwa kazi za kawaida.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina jukumu la kuandaa na kusimamia utayarishaji wa Sera, Sheria, Mipango na kufanya Utafiti na tathmini kwa miradi ya maendeleo. Aidha, ina jukumu la kufuatilia, kukusanya na kuchambua takwimu zitakazosaidia kufanya tathmini na kupanga mipango ya maendeleo. Vile vile, idara inaratibu utekelezaji wa DIRA 2020, MKUZA II, Mageuzi Makuu (*Core Reforms*), Ilani ya Uchaguzi na mipango mengine mikuu ya Kitaifa na Kimataifa. Jukumu jengine ni kuratibu kazi za kuandaa ripoti za utekelezaji wa Bajeti na Mipango ya Maendeleo. Idara hii ni mpya baada ya kutenganishwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Hii inatokana na agizo la serikali kusisitiza kuwa shughuli za mipango zinapewa kipaumbele.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliidhinishiwa jumla ya shilingi 649.7 milioni kwa matumizi ya kawaida ambazo zilikuwa ni kwa ajili ya kazi za Idara ya Mipango, Sera na Utafiti pamoja na Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Idara imeingiziwa shilingi 500 milioni sawa na asilimia 77 ya makadirio ya matumizi na kutekeleza yafuatayo:-

- Imeandaa semina ya kuwajengea uwezo Maafisa Mipango 52 Unguja na Pemba ili waweze kutekeleza malengo yao kwa ufanisi. Ikiwa pamoja na kutayarisha ripoti za Ilani ya Uchaguzi, Kuandaa ripoti ya Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi, ujazaji wa fomu za miradi ya maendeleo pamoja na mfumo bora wa mawasiliano miongoni mwa watendaji.
- Kutembelea jumla ya miradi minane ya maendeleo na kujua hatua iliofikia.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iliidhinishiwa kutekeleza miradi 11 ya maendeleo na fedha zilizotengwa kwa miradi hiyo ni shiligi 3,860 milioni.

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeratibu utekelezaji wa miradi hiyo kwa ufanisi mkubwa. Naomba kuitaja miradi hiyo kama ifuatavyo:-

- Ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ikulu na nyumba za Serikali
- Mradi wa Mawasiliano Ikulu
- Marekebisho ya Serikali za Mitaa

- Mradi wa Uendelezaji Vitambulisho
- Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu Mkoa Kaskazini Unguja
- Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu Mkoa Kusini Unguja
- Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu Mkoa Kaskazini Pemba
- Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu Mkoa Kusini Pemba
- Mradi wa Shamba la Mfano la Mboga Mboga Bambi
- Ujenzi wa Makao Makuu ya Valantia
- Ujenzi wa Hospitali mpya ya Kikosi cha KMKM

Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu na Nyumba za Serikali

Mhe. Spika, Mradi wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ikulu na nyumba za serikali uliidhinishiwa shilingi 1,450 milioni. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2011, Mradi umeingiziwa shilingi 1,192 milioni sawa na asilimia 82 ya makadirio ya matumizi na kutekeleza yafuatayo:-

- Matengenezo makubwa katika nyumba ya Migombani anayoishi Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Miongoni mwa matengenezo hayo ni kuezeka upya mapaa ya nyumba zote kwa kutumia vigae vya mabati (*Harvey tiles*) na ujenzi wa "*canopy*".
- Ujenzi wa nyumba ya mapokezi na uwekaji samani.
- Ujenzi wa ukuta unayoizunguka Ikulu ya Migombani kwa ajili ya kuweka uhifadhi na usalama wa nyumba hiyo.
- Kuzifanyia matengenezo nyumba mbili za askari ikiwa ni pamoja na uwezekaji wa paa, upakaji rangi, uwekaji milango, madirisha, vyoo pamoja na uwekaji wa samani mpya.
- Kuzifanyia matengenezo nyumba za wafanyakazi pamoja na kuziweka samani.
- Ujenzi wa nyumba ya kufulia na ujenzi wa jiko jipya la askari na wahudumu.
- Ununuzi wa Jenereta ya KVA 200 na uwekaji wa vifaa vyake.
- Kuweka matangi mawili ya maji yenye uwezo wa ujazo wa lita 10,000 kila moja.
- Matengenezo kwenye Ikulu Kubwa ya Mnazi mmoja ikiwa ni kuweka vipoza hewa kwenye ukumbi wa Baraza la Mapinduzi, kukata vyumba vya ziada kwa *Aluminium* sehemu ya Ofisi ya Faragha ili kuongeza Ofisi za watendaji, kufanya ukataji wa vyumba kwenye sehemu ya chini ya jengo kuu kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Ushirikiano wa Kimataifa na *diaspora*, kuweka vigae "*tiles*" kwenye varanda ya juu na chini ya Jengo

Kuu pamoja na kupaka rangi jengo lote na ukuta unaozunguka Ikulu.

- Matengenezo katika jengo lililokuwa likitumiwa na *ZIPA* kwa kukata vyumba vya ziada vya Ofisi kwa kutumia *Aluminium* na kupaka rangi kwa lengo la kuongeza ofisi ambazo zinatumiwa na watendaji mbalimbali wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
- Matengenezo ya mfumo mpya wa maji wa nyumba ya Laibon iliopo Dar es Salaam.
- Nyumba ya Bwefum imeezekwa kwa kutumia vigae na kuibadilisha sura yake ya awali ambapo ilikuwa na zege.
- Matengenezo pamoja na kuweka samani nyumba anayoishi Makamo wa Pili wa Rais iliopo Mazizini.
- Matengenezo makubwa kwenye nyumba itakayotumiwa kuwa Ofisi ya Rais Wastaafu wa Zanzibar iliopo Mazizini ikiwa ni pamoja ya samani zao.
- Matengenezo mengine ni kwenye nyumba ya "Mazizini namba 1" na "Mazizini namba 2" ambazo hutumiwa kwa shughuli maalum za Viongozi wa Kiserikali.
- Upakaji rangi wa nyumba anayoishi Makamo wa Kwanza wa Rais maarufu Bosnia kabla hajahamia.
- Matengenezo madogo kwenye Ikulu ya Chake Chake Pemba ikiwa ni pamoja na kuweka vipoza hewa vipya na kuweka Jenereta jipya lenye uwezo wa KVA 100.

Mradi wa Mawasiliano – Ikulu

Mhe. Spika, Mradi wa Mawasiliano - Ikulu uliidhinishiwa shilingi 50 milioni. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, fedha zilizoingizwa ni shilingi 49.9 milioni sawa na asilimia 99.9 ya makadirio ya matumizi na kutekeleza mambo makuu matano yafuatayo:-

- Kuchapisha kalenda 3,500 za mwaka 2011 zinazoonesha matukio muhimu yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
- Kumpatia mafunzo ya muda mrefu mfanyakazi mmoja katika Shahada ya Pili ya Taaluma ya Maendeleo katika Chuo Kikuu Cha Sokoine, Morogoro.
- Kununua kompyuta tano kwa ajili ya matumizi ya Kitengo cha Mawasiliano pamoja na Ofisi ya Faragha.
- Kuwafanyia semina Maafisa mawasiliano wa Wizara za SMZ
- Kubadilisha mfumo wa mtandao [internet] baada ya kuonekana mapungufu yalikuwepo hapo mwanzo ikiwa ni pamoja na sehemu muhimu za Ofisi kukosa huduma hiyo.

Mradi wa marekebisho ya Serikali za Mitaa

Mhe. Spika, Mradi wa marekebisho ya Serikali za Mitaa uliidhinishiwa shilingi 250 milioni. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, fedha zilizoingizwa ni shilingi 70 milioni sawa na asilimia 28 na kutekeleza yafuatayo:-

- Kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya utayarishaji wa rasimu ya Sera ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.
- Kufanya mikutano miwili ya wadau kwa lengo la kuipitia na kupata maoni yao.
- Kuandaa vikao vya wataalamu kwa ajili ya kupitia na kufanya marekebisho rasimu ya Sera ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kufuatia maoni ya awali ya wadau.

Mhe. Spika, utekelezaji wa miradi mingine minane niliyoitaja hapo juu nitaitolea maelezo katika idara husika.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, katika utekelezaji wa kazi za kawaida Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kutoa elimu ya uibuaji na uimarishaji wa miradi kwa maofisa miradi.
- Kuanzisha kituo cha nyaraka (*Documentation Centre*).
- Kuanzisha Tovuti (*Website*) na Barua Pepe rasmi (*Official E-mail Address*).
- Kuanzisha kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA).
- Kuanzisha kitengo cha Utafiti na kitengo cha takwimu.
- Kuwajengea uwezo watendaji kwa kufanya ziara za kujifunza, mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wanne na kufanya semina mbili kwa maafisa mipango.
- Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
- Kununua vitendea kazi vikiwemo kompyuta nne, fotokopi moja, skana na samani za Ofisi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti itaratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo itakayotekelezwa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambayo ni Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ikulu, mradi wa Mawasiliano Ikulu na mradi wa Marekebisho ya Tawala za Mikoa na Serikali Mitaa.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ikulu na nyumba za serikali, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imelenga kutekeleza yafuatayo:-

- Kumalizia Ukarabati wa Ikulu Ndogo ya Migombani na kuiwekea vifaa vya tahadhari ya moto
- Kuendelea kulifanyia matengenezo jengo la Ikulu ya Bwefum
- Kulifanyia ukarabati jengo la Ikulu Kuu (Mnazi Mmoja) na kuweka vifaa vya tahadhari ya moto
- Kuweka paa, kuezeka na kuifanyia matengenezo Ikulu ndogo ya Mkoani
- Kuanza ujenzi wa nyumba ya wahudumu iliopo Ikulu ndogo ya Dodoma
- Kuanza ujenzi wa Ikulu ndogo ya Laibon Dar es Salaam

Mhe. Spika, Mradi wa Mawasiliano – Ikulu, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imekusudia kufanya yafuatayo:-

- Kufanya mapitio ya Mkakati wa Mradi wa Mawasiliano, Ikulu.
- Ununuzi wa gari la Mawasiliano na vifaa vyake.
- Kununua vitendea kazi vipya na vya kisasa vikiwemo TV mbili, vifaa vya kurekodia (*audio* moja na *video* moja), *LCD projector* moja na kompyuta sita, *printer* mbili na *Camera* tatu.

Mhe. Spika, katika mradi wa marekebisho ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imelenga kufanya yafuatayo:-

- Kukamilisha na kuchapisha Sera ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.
- Kuandaa mpango mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.
- Mapitio na marekebisho ya Sheria Nam.1 ya Mwaka 1998 ya Mamlaka ya Utawala wa Mikoa na Sheria Nam. 3 na 4 ya mwaka 1995 za Serikali za Mitaa,
- Kuandaa utafiti unaolenga kujua tatizo linalopelekea ukusanyaji mdogo wa mapato na uwezo wa kiutendaji katika Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe shilingi 240 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 550 milioni kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ina jukumu la kusimamia shughuli za utawala na utumishi za siku hadi siku zikiwemo kusimamia Sheria na Kanuni za Utumishi kwa wafanyakazi pamoja na kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi, kusimamia Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa mali chakavu za serikali, kuwaendeleza wafanyakazi kielimu pamoja na kusimamia maslahi yao.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Idara ya Uendeshaji na Utumishi iliidhinishiwa shilingi 649.7 milioni kwa matumizi ya kawaida ambazo zilikuwa ni kwa ajili ya kazi za Idara ya Uendeshaji na Utumishi pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2011, idara imeingiziwa shilingi 500 milioni sawa na asilimia 77 ya makadirio ya matumizi na imetekeleza yafuatayo:-

- Kushughulikia ajira mpya wafanyakazi wanne
- Kushughulikia taratibu za kustaafu kwa wafanyakazi sita
- Kushughulikia upatikanaji wa viinua mgongo kwa wastaafu watatu
- Kushughulikia likizo za wafanyakazi 77
- Kushughulikia uteuzi wa wafanyakazi bora sita na kupatiwa zawadi
- Kushughulikia udhamini wa mikopo ya Benki kwa wafanyakazi 66
- Ununuzi wa samani za Ofisi zikiwemo viti, meza, makabati, kompyuta katika Ofisi za Naibu Katibu Mkuu Idara Maalum na Ofisi ya Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti
- Kuwajengea uwezo wa kielimu wafanyakazi 18 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika viwango na fani tofauti. Viambatanisho Namba 1, 2, na 3 vinatoa ufafanuzi wa kina juu ya masuala ya Utumishi na Uendeshaji kama yalivyoelezwa hapo juu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imejipangia kutekeleza malengo sita yafuatayo:-

- Kuongeza ufanisi wa kazi kwa kununua vitendea kazi vya kisasa vikiwemo vespa moja, kompyuta mbili (2), vifaa vya Ofisi na samani.
- Kuwajengea uwezo wafanyakazi 10 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ndani ya nchi pamoja na kutoa taaluma ya kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI.

- Kutoa motisha kwa wafanyakazi kwa kuwapatia malipo baada ya saa za kazi, sare kwa madereva na matarishi na kutoa zawadi kwa wafanyakazi bora.
- Kuweka mfumo bora wa usimamizi na utoaji wa taarifa katika uwajibikaji kazini.
- Kufanya uhakiki wa mahitaji ya mafunzo kwa wafanyakazi pamoja na kuandaa mpango wa mafunzo hayo.
- Kuandaa mkutano wa kupitia majukumu ya kazi kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Spika, ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 1,858.5 milioni kwa kazi za kawaida. Fedha hizi zitatumika kwa kulipia mishahara na maposho ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Ofisi ya Faragha ya Rais, Idara ya Mawasiliano, Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara ya Uratibu wa Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

OFISI YA FARAGHA YA RAIS

Mhe. Spika, Ofisi ya Faragha ya Rais ina jukumu la kupanga na kuratibu shughuli za kila siku za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili zifanyike kwa ufanisi. Majukumu mengine ya ofisi hii ni kusimamia ratiba ya kazi pamoja na kupokea maagizo ya Mhe. Rais na kuwasiliana na taasisi mbali mbali kwa utekelezaji wa maagizo hayo. Pia, ofisi hii ina jukumu la kuweka kumbukumbu za mazungumzo ya Mhe. Rais na viongozi mbali mbali, mabalozi, taasisi na wananchi kwa jumla pamoja na kufuatilia maagizo na maelekezo yanayotokana na mazungumzo hayo. Pamoja na majukumu hayo, ofisi hii ina wajibu wa kutayarisha muhtasari wa Ripoti zinazomhusu Mhe. Rais pamoja na kuwasiliana na vyombo vya habari kwa ajili ya kutoa taarifa kamili ili kuwapatia habari zilizo sahihi wananchi na wahusika wote.

Mhe. Spika, Ofisi ya Faragha ya Rais pia inahusika na huduma nyenginezo muhimu za Rais wa Zanzibar, zikiwemo huduma za makaazi, chakula, usafiri pamoja na utunzaji na matengenezo ya majengo yaliyo chini ya Ikulu. Aidha, ofisi hii ndio inayoratibu safari za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi za ndani na nje ya nchi. Ofisi pia ina jukumu la kusimamia shughuli za Rais Dar es Salaam na Dodoma.

Mhe. Spika, Ofisi ya Faragha ya Rais kwa mwaka wa fedha 2010/2011, iliidhinishiwa shilingi 1,036 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi

Machi 2011, ofisi hii ilitumia shilingi 763 milioni sawa na asilimia 74 ya makadirio ya matumizi.

Mhe. Spika, Ofisi ya Faragha ya Rais imeimarishwa kwa kuongezewa watendaji, wakiwemo Wasaidizi wa Rais katika nyanja mbali mbali zikiwemo uchumi, maendeleo ya jamii, sheria, hotuba pamoja na kupatiwa vitendea kazi vipya. Aidha, ofisi imefanikisha kazi zake kwa kiwango kikubwa kwa kutoa huduma za chakula, usafiri na makaazi kwa wageni wote wa serikali wanaostahiki kupatiwa huduma za Ikulu.

Mhe. Spika, ofisi hii, imesimamia vyema ratiba za Rais ambazo zimegawika sehemu mbili, Julai hadi wiki ya mwanzo ya Novemba 2010 kipindi kilichokuwa chini ya uongozi wa Rais wa Awamu ya Sita, Mhe. Dk. Amani Abeid Karume na kipindi kinachoendelea chini ya uongozi wa Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein.

Katika kipindi hiki, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar alikutana na mabalozi na viongozi mbali mbali na kufanya mazungumzo nao yenye mustakabala mwema kwa maendeleo ya nchi yetu. Mazungumzo hayo yalilenga zaidi katika kuiletea maendeleo Zanzibar katika nyanja za uchumi, biashara, viwanda, siasa na ustawi wa jamii. Wageni wote aliokutana nao Mhe. Rais, katika kipindi hicho, waliimwagia sifa nchi yetu kutokana na kupevuka kisiasa na hali ya umoja, amani na utulivu inayoendelea kuwepo nchini mwetu. Wananchi wameweza kuishi pamoja na kushirikiana katika kujenga nchi bila ya kujali itikadi zao za kisiasa ndani ya Muundo mpya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(Kiambatanisho Nam. 4 kinatoa ufafanuzi wa kina juu ya orodha ya Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa waliokuja kuonana na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi).

Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amefanya ziara nne nje ya Zanzibar katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Mei, 2011. Ziara mbili nchini Kenya na Namibia zilifanywa na Mhe. Dk. Amani Abeid Karume na ziara za Libya na Uturuki zilifanywa na Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein. Ziara ya Kenya na Namibia zilikuwa ni za kumuwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dk. Jakaya Mrisho Kikwete katika uundaji wa Katiba mpya ya Kenya na kikao cha *SADC* mjini Windhoek, Namibia. Ziara hizo zilikuwa na umuhimu mkubwa katika kuimarisha uhusiano na ujirani mwema. Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, alikwenda Libya kumuwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano wa tatu wa ushirikiano kati ya Jumuiya ya Ulaya na Umoja wa Afrika. Pia, alifanya ziara ya Kiserikali nchini Uturuki kuanzia tarehe 28 Aprili, 2011 hadi tarehe 2 Mei, 2011. Katika ziara hiyo, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein alikutana

na mwenyeji wake Rais wa Uturuki Mhe. Abdullah Gul na viongozi wengine wa nchi hiyo. Ziara hiyo imefanikiwa sana na makubaliano kadhaa yamefikiwa ambapo Uturuki itashirikiana na Zanzibar katika kuimarisha sekta za afya, utalii, elimu na kilimo.

Mhe. Spika, mashirikiano katika sekta ya afya yatajumuisha kupatiwa wataalamu wa afya kutoka Uturuki kuja kufanya tathmini ya mahitaji yetu katika Wizara ya Afya, kuongezwa nafasi za masomo ya udaktari, madawa, ufundi, teknolojia ya habari na kupatiwa wataalamu wa matibabu ya moyo na maradhi mengineyo. Katika utalii, ujumbe kutoka Zanzibar utafanya ziara nchini Uturuki hivi karibuni kuanzisha rasmi uhusiano katika sekta hii hasa katika miji ya Ankara na Antalya. Aidha, jengo la Beit el Ajaib hapa Zanzibar litaimarishwa. Chuo cha Maendeleo ya Utalii Maruhubi nacho kitaimarishwa na watembezaji watalii wazalendo watasaidiwa kwa kujengewa uwezo. Shirika la Ndege la Uturuki *(Turkish Airline)* litaangalia uwezekano wa kuanzisha safari za moja kwa moja baina ya Zanzibar na Uturuki.

Mhe. Spika, katika sekta ya elimu, uhusiano baina ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar *(SUZA)* na Vyuo Vikuu vya Ankara na Istanbul vitaimarishwa kwa kubadilishana taarifa za kitaalamu na wahadhiri kutembeleana. Kwa upande wa kilimo, Uturuki itasaidia kwa kukiimarisha Chuo cha Kilimo Kizimbani ili kiweze kutoa wataalamu hadi kufikia kiwango cha Stashahada na wataalamu wa chuo hicho watakwenda Uturuki kujifunza zaidi mambo ya utafiti katika Chuo cha West Mediterranean, Antalya. Ofisi ya Faragha ya Rais na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa pamoja zitasimamia utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa kwenye ziara ya Uturuki kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mhe. Spika, kufuatia kuundwa upya kwa Wizara mbali mbali, baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 2010, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikutana na kuzungumza na Mawaziri na Watendaji wa Wizara zote 16 za SMZ, kila moja kwa wakati wake, kuanzia tarehe 6 Disemba, 2010 mpaka 27 Disemba, 2010. Madhumuni ya mikutano hiyo ilkuwa ni kubadilishana mawazo, kuyaelewa malengo na kuhakikisha muundo wa Wizara hizo unatekelezwa kwa ufanisi. Vikao hivyo vilifanikiwa sana kwa kuweka wazi majukumu ya kila Idara na Wakurugenzi wanaoziongoza.

Mhe. Spika, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, katika kipindi kifupi tokea kuchaguliwa kwake na wananchi wa Zanzibar ameonesha mfano wa kuwa karibu sana na wananchi. Kwa kuthibitisha hilo, amefanya ziara za aina yake katika wilaya zote kumi Unguja na Pemba. Katika ziara hizo, Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein alifuatana na Mhe. Mama Mwanamwema Shein, Mawaziri, Naibu Mawaziri, Katibu

Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi na viongozi wengine. Viongozi hao walipata fursa ya kutembelea miradi mbali mbali ya maendeleo pamoja na miradi iliyoanzishwa na wananchi katika sekta za elimu, biashara, afya, kilimo na huduma za jamii.

Mhe. Spika, mambo ya kufurahisha zaidi ni mtindo wa kusaidia nguvu za wananchi kwa njia ya mchango wa papo kwa papo (harambee) uliokuwa ukiongozwa na Mhe. Rais mwenyewe ambapo pia Waheshimiwa Mawaziri, Wanasiasa wengine na Watendaji Wakuu wa Serikali walishiriki kikamilifu. Aidha, kila baada ya kumalizika ziara katika Mkoa, palifanyika majumuisho ambapo mambo yaliyobainika katika taarifa ya Mkoa na ziara halisi yalielezwa kwa viongozi na wananchi kwa uwazi zaidi. Katika ziara hizo wananchi walipewa fursa ya kutoa maoni na maelezo yao kwa njia ya uwazi. Mtindo huu, umezindua ari na kuwatia moyo wananchi na kuwajengea matumaini mapya.

Mhe. Spika, katika ziara hizo, Mhe. Rais alivutiwa sana na juhudi za wataalamu wazalendo katika suala zima la utafiti aliwasisitiza wataalamu kutoa kipao mbele katika ya utafiti wa udogo na mbegu za mpunga hasa mbegu mpya ya mpunga aina ya *NERICA* inayotegemewa kuwa mkombozi katika kupata uhakika wa chakula. Katika kuangalia maendeleo ya sekta ya afya, Mhe. Rais alitembelea Hospitali ya *Cottage* ya Makunduchi ambayo itapandishwa daraja na kuwa hospitali ya Wilaya, pamoja na ujenzi wa kituo kipya cha afya hapo Mbuzini.

Maeneo mengine aliyoyaangalia ni pamoja na Skuli za Cekechea Bweleo na Meya, kilimo cha mpunga wa juu na umwagiliaji, ufugaji wa kisasa wa ng'ombe, kuku na bidhaa mbali mbali zitokanazo na mifugo. Aidha, wananchi wametakiwa kuacha uharibifu wa mazingira kufuatia uchimbaji wa matofali unaofanyika, Kangagani, Mwambe na Micheweni, kisiwani Pemba. Maendeleo ya ujenzi wa Skuli za Sekondari 19 za Wilaya, Unguja na Pemba zinazojengwa kwa mkopo wa Benki ya Dunia ni mazuri na skuli hizo zitakabidhiwa rasmi kwa Serikali mnamo Septemba, 2011. Watoto wetu wanatarajiwa kuanza kuzitumia skuli hizo mpya mnamo Januari, 2012. Mafanikio hayo ni ya kupigiwa mfano.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Faragha na Huduma za Rais imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendelea kuimarisha shughuli mbali mbali za kila siku za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

- Kuratibu na kusimamia upatikanaji wa huduma bora za Mhe. Rais wa Zanzibar, wageni wa Serikali wanaostahiki kupatiwa huduma za Ikulu pamoja na safari za nje na za ndani.
- Kutunza nyumba zote za Ikulu.
- Kuratibu mafunzo kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Faragha.
- Kununua vitendea kazi vikiwemo kompyuta.
- Kuimarisha Maktaba ya Ofisi ya Faragha.

Mhe. Spika, ili Ofisi ya Faragha ya Rais iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 520 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MAWASILIANO – IKULU

Mhe. Spika, Idara ya Mawasiliano Ikulu ina jukumu la kutoa, kuratibu na kupokea taarifa za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusu utekelezaji wa Sera na Mipango ya Serikali inayolenga kuwaletea maendeleo wananchi. Aidha, Idara hii ina jukumu la kuthibitisha na kuhakikisha kuwa taarifa zote za Rais zinazotolewa kwa wananchi na wadau wengine ni sahihi na zinatolewa kwa wakati muafaka.

Mhe. Spika, majukumu mengine ni kutambua fursa ambazo zinaweza kutumika ili kuimarisha mawasiliano baina ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Taasisi za Serikali na wananchi pamoja na kuhakikisha kuwa wananchi wanaarifiwa kila hatua za yale yote yaliyoahidiwa kwao na Mhe. Rais wa Zanzibar. Lengo ni kuweka taswira nzuri baina ya Mhe. Rais wa Zanzibar, wananchi na washirika wengine wa maendeleo. Ofisi ya Rais itaandaa utaratibu utakaomuwezesha Mhe. Rais kukutana na kuzungumza na vyombo vya habari kuhusu mambo yanayohusu Zanzibar na maendeleo yake kila baada ya miezi mitatu.

Mhe. Spika, Idara ya Mawasiliano Ikulu, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, iliidhinishiwa TZS 39.7 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia Machi 2011, Idara imeingiziwa TZS 32.5 milioni sawa na asilimia 82 ya makadirio ya matumizi na kutekeleza mambo matatu yafuatayo:-

- Imetoa taarifa kwenye vyombo vya habari (Magazeti, Redio na Televisheni) vya Serikali na watu binafsi.

- Kutayarisha vipindi maalum 22 kwenye Televisheni. Vipindi hivyo vililenga kuonesha utekelezaji wa ahadi mbali mbali za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika sekta na maeneo tofauti.

- Imeandaa kipindi maalum kuhusiana na maendeleo yaliyopatikana katika kipindi cha siku mia moja (100) baada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa kuingia madarakani.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Mawasiliano Ikulu inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuandaa program maalum yenye lengo la kutoa taarifa kuhusiana na utekelezaji wa ahadi za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kama zilivyoelezwa kwenye Ilani ya CCM pamoja na ahadi alizozitoa wakati alipokuwa akifanya kampeni za uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010.
- Kutoa mafunzo kwa Watendaji Wakuu wa Serikali, Maafisa Mawasiliano wa Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Masheha na Jumuiya zisizo za Kiserikali juu ya umuhimu wa kutoa taarifa hasa zile zinazohusiana moja kwa moja na utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar ambazo utekelezaji wake utafanyika kwenye maeneo yao ya kazi.
- Kuwajengea uwezo wafanyakazi watatu kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mmoja atapatiwa mafunzo ya muda mrefu.
- Kutayarisha machapisho na vijarida vyenye ujumbe unaohimiza utekelezaji wa ahadi za Mhe. Rais wa Zanzibar katika sekta za kisiasa, kiuchumi na kijamii.
- Kununua vitendea kazi vikiwemo vifaa vya kompyuta.

Mhe. Spika, ili Idara ya Mawasiliano Ikulu iweze kutekeleza malengo yaliyoelezwa hapo juu, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 80.7 milioni kwa kazi kawaida.

KITENGO CHA USALAMA WA SERIKALI *(GSO)*

Mhe. Spika, Kitengo cha Usalama wa Serikali kimeanzishwa kufuatia Sheria Nam. 5 ya mwaka 1983 na kina majukumu ya kusimamia Usalama na Siri za Serikali, kutoa ushauri katika udhibiti na utunzaji wa nyaraka za Serikali, kutoa ushauri kuhusu ulinzi na usalama wa vituo muhimu vya Serikali ikiwa pamoja na miundo mbinu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kitengo kilikadiriwa kutumia TZS 29.8 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Ofisi

hii ilipatiwa TZS 15.9 milioni sawa na asilimia 53 ya makadirio ya matumizi na kutekeleza yafuatayo:-

- Kimefanya upekuzi kwa wafanyakazi 529. Wanne (4) kutoka Taasisi za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, (172) kutoka Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, (328) kutoka Wizara ya Habari Utamaduni na Utalii, (2) Wizara Afya, (2) Wizara ya Maji, Ujenzi na Nishati, (15) Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na (6) Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
- Kimekagua Ofisi za Baraza la Wawakilishi Unguja, Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali Pemba, Hospitali ya Wete – Pemba na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Ikulu – Zanzibar na kutoa mafunzo ya ndani kwa watumishi wa masjala.
- Kimekagua kituo cha kupokea na kusambaza umeme Mtoni Unguja, ikiwa ni sehemu ya vituo muhimu vya Serikali.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Kitengo cha Usalama wa Serikali kinakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kufanya ukaguzi wa Taasisi za Serikali 10 katika eneo la udhibiti wa utunzaji wa nyaraka za Serikali na kutoa ushauri unaofaa.
- Ukaguzi wa vituo muhimu vitatu vya Serikali, yakiwemo majengo, maeneo na miundo mbinu ya Serikali na kutoa ushauri unaofaa.
- Kuwafanyia upekuzi wa awali na upekuzi endelevu watumishi wa Serikali 500.
- Kuendeleza ushirikiano na Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora katika kusimamia kanuni za utumishi na kuhakikisha zinatekelezwa hususan zile zinazogusa usalama wa mali na nyaraka za Serikali.
- Kuendelea kushirikiana na Maofisa Usalama wa Taasisi za Serikali katika kusimamia na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria zinazohusu utunzaji wa siri za Serikali.

Mhe. Spika, ili kitengo cha Usalama wa Serikali *(GSO)* kiweze kutekeleza kazi zake, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe TZS 49.9 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

OFISI YA USAJILI NA KADI ZA UTAMBULISHO

Mhe. Spika, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho imeanzishwa rasmi mwaka 2005 chini ya Sheria Nam. 7 ya 2005 ikiwa na majukumu ya kuwasajili na kuwapatia vitambulisho Wazanzibari wakaazi wenye umri wa miaka 18 na kuendelea. Ofisi hiyo pia imepewa jukumu la kutoa vitambulisho kwa kila Mzanzibari Mkaazi aliyetimiza masharti ya usajili na kutunza taarifa za usajili wa wananchi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho iliidhinishiwa kutumia TZS 910 milioni kwa kazi za kawaida na TZS. 800 milioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2011, Ofisi hii ilipatiwa TZS 687 milioni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na TZS 785 milioni sawa na asilimia 98 ya makadirio ya matumizi ya maendeleo.

Mhe. Spika, Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho imefanya kazi zifuatazo:-

- Imesajili Wazanzibari Wakaazi wapya 6,102 waliotimiza masharti ya usajili.
- Imetengeneza vitambulisho 460,784 ambavyo vimemaliza muda wake wa matumizi na kuvigawa kwa wahusika.
- Imetengeneza vitambulisho vipya vya watumishi wa Serikali. Vitambulisho hivyo vimetolewa kwa Ofisi ya Makamo wa Kwanza, Ofisi ya Makamo wa Pili na baadhi ya wafanyakazi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.
- Kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imesimamia kwa kutoa ushauri wa kitaalamu katika utekelezaji wa kuanzisha mtandao wa kompyuta wa SMZ *(Zanzibar E-Government).*
- Imetayarisha vipindi 63 vya kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.
- Imewajengea uwezo wa kielimu watendaji wake tisa kwa kuwasomesha katika viwango vya Cheti, Stashahada na Shahada ya kwanza ndani na nje ya nchi.
- Imeandaa Rasimu ya marekebisho ya Sheria ya usajili Namba 7 ya mwaka 2005 ili kuruhusu utoaji wa vitambulisho maalum kwa wageni wanaoishi nchini. Rasimu hiyo bado inaendelea kujadiliwa katika ngazi za wataalamu.
- Imefanyiwa ukaguzi na wakaguzi wa kimataifa juu ya muundo, mfumo na taratibu zake za utendaji na imethibitishwa kuwa inaendelea kufanya kazi zake kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vilivyowekwa na *International Standard Organisation na IQ Net.*

- Imenunua kompyuta kuu tano *(Servers)*, kompyuta za kawaida saba (7) kwa ajili ya kufanikisha kazi za usajili na kuwekea kumbukumbu.
- Imejenga jengo la Ofisi ndogo kwa ajili ya Mkuu wa Usajili na Vitambulisho Pemba.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendelea kuwasajili Wazanzibari wanaotimiza masharti ya usajili na kutoa Vitambulisho.
- Kuendelea kubadilisha na kutengeneza vitambulisho vya wafanyakazi wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwa kuzingatia muundo mpya wa Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika kutekeleza agizo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya uanzishwaji wa mtandao wa kompyuta wa SMZ *(Zanzibar E-government).*
- Kuanza kutoa vitambulisho maalum kwa wageni wanaoishi nchini kwa ruhusa maalum *(Residence Permit)* na kutunza taarifa zilizokusanywa kwa ajili hiyo katika database ya Serikali
- Kukamilisha marekebisho ya Sheria ya usajili Nam. 7 ya mwaka 2005.
- Kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi bora na sahihi ya vitambulisho vya Mzanzibari kwa kutoa vipindi 50 katika Redio.
- Kuendelea kuwajengea uwezo wa kielimu watendaji wa Ofisi.
- Kufanya utafiti juu ya uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa vitambulisho na kukusanya maoni juu ya huduma zinazotolewa.
- Kununua vitendea kazi vikiwemo kompyuta sita, Printer moja na vifaa vya uandikishaji.

Mhe. Spika, ili Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 1,248 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 150 milioni kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA SHUGHULI ZA WAZANZIBARI WALIOPO NCHI ZA NJE *(DIASPORA)*

Mhe. Spika, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Shughuli za Wazanzibari waliopo Nchi za Nje ina majukumu ya kuimarisha mfungamano wa Kikanda ili kuweza kutumia fursa za kiuchumi zinazotokana na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Jumuiya nyengine za Kikanda. Aidha, Idara ina jukumu la kusimamia uimarishaji wa ushirikiano mwema na nchi marafiki na Taasisi za Kimataifa. Jukumu jengine iliyopewa Idara hii ni kuwashajihisha Wazanzibari wanaoishi nchi za nje kushiriki katika shughuli za maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mhe. Spika, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari waliopo Nje kwa mwaka wa fedha 2010/2011, iliidhinishiwa TZS 651 milioni. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2011, Idara imeingiziwa TZS 509 milioni sawa na asilimia 78 ya makadirio ya matumizi ya kawaida.

Mhe. Spika, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Shughuli za Wazanzibari Waliopo Nchi za Nje iliendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya uratibu na uwezeshaji wa ushiriki wa Zanzibar katika mikutano ya ushirikiano wa Jumuiya za kikanda ambazo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama. Jumuiya hizo zinajumuisha Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC)*, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki *(EAC)*, Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi *(Indian Ocean Rim)* na Jumuiya nyengine za Kikanda.

Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*)

Mhe. Spika, katika mkutano wa kamati maalum ya Mawaziri wa Biashara wa Jumuiya ya *SADC* uliofanyika Windhoek, Namibia kuanzia tarehe 10 Februari, 2011 hadi tarehe 13 Februari, 2011. Mawaziri wa Biashara wa Jumuiya hii walipitia maamuzi yatokanayo na mkutano wao wa 21 kuhusu kuimarisha eneo huru la biashara la *SADC*. Katika mkutano huo lilizungumzwa suala la utayarishaji wa Sera na Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda kwa nchi za *SADC*. Kamati Maalum ya Mawaziri wa Biashara iliiagiza Sekretarieti ya *SADC* kuendelea kutafuta fedha na ushauri wa kitaalamu wa kuimaliza kazi hiyo kwa kuzingatia makubaliano yaliyofikiwa kati ya Sekretarieti ya *SADC* na *UNIDO* katika uendelezaji wa viwanda.

Katika hatua nyengine Kamati maalumu ya Mawaziri wa Biashara ilipitia hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa uhalisi wa bidhaa *(Rules of Origin)* kwa nchi za *SADC* ambapo imeripotiwa kuwa Nchi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Botswana, Zambia, Swaziland, Mauritius na Afrika Kusini zinatekeleza kikamilifu. Katika mkutano huo Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania iliomba ruhusa ya kupandisha ushuru wa bidhaa za karatasi na sukari zinazoingizwa Nchini kutoka Nchi za *SADC* kutoka 0 hadi asilimia 25 ili kulinda viwanda vyake. Ombi hilo lilikubaliwa, lakini kutokana na uhaba wa sukari uliojitokeza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijalitekeleza.

Mhe. Spika, mkutano wa Kamati maalumu ya Mawaziri wa Fedha na Uwekezaji wa Nchi za Jumuiya ya *SADC* ulifanyika katika tarehe 11 Februari, 2011 mjini Windhoek, Namibia. Miongoni mwa mambo yaliyozungumzwa ni pamoja na kupitia hatua zilizochukuliwa katika kuridhia Itifaki ya Biashara na Uwekezaji.

Katika mkutano huo iliripotiwa kuwa Itifaki hiyo tayari imekwishaanza kutekelezwa baada ya kuridhiwa na Nchi zaidi ya theluthi mbili za *SADC*. Nchi zilizokuwa hazijaridhia mpaka sasa ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Swaziland, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Zimbabwe na Sychelles. Mkutano huo pia ulizungumzia kuhusu mabadiliko ya utaratibu wa kuchangia katika bajeti ya *SADC*.

Mhe. Spika, mkutano Maalumu wa Wakuu wa Nchi wa *SADC* wa Ushirikiano wa Siasa, Ulinzi na Amani ulifanyika tarehe 31 Machi, 2011. Mkutano huo ulizungumzia kuhusu hali ya kisiasa Zimbabwe na Madagascar. Wakuu wa nchi walisisitiza kuwa hali ya Zimbabwe lazima ibadilike ili amani irejee na walimtaka Msuluhishi Rais wa Afrika ya Kusini Mheshimiwa Jacob Zuma kuendelea na usuluhishi wake.

Aidha, wakuu wa Nchi walimpongeza Rais wa zamani wa Msumbiji Mhe. Joaquim Chissano kwa juhudi anazozichukua katika kutafuta amani ya kudumu nchini Madagascar. Katika kikao cha dharura cha Wakuu wa Nchi za SADC kilichofanyika mjini Johanesburg, Afrika Kusini kuanzia tarehe 11 Juni, 2011 na tarehe 12 Juni, 2011 zilitolewa ripoti za kubadilika kwa hali ya kisiasa katika nchi ya Zimbabwe. Wakuu wa nchi hizo walipongeza hatua hizo na kutaka mageuzi yaendelee ili hatimae uchaguzi uweze kufanyika.

Kuanzisha Eneo Huru la Biashara la UTATU *(COMESA, EAC na SADC)*
Mhe. Spika, mkutano wa pili wa wakuu wa Nchi za *COMESA, EAC* na *SADC* ulifanyika tarehe 12 Juni, 2011 Johannesburg, Afrika Kusini. Ajenda za mkutano huo zilikuwa ni kupokea taarifa ya utekelezaji wa maamuzi ya mkutano wa kwanza wa UTATU uliofanyika Oktoba, 2008 Kampala, Uganda pamoja na kuzindua rasmi majadiliano ya kuanzisha eneo huru la biashara la UTATU. Katika mkutano huo, iliripotiwa kuwa hatua nzuri zimefikiwa katika kutekeleza maamuzi ya viongozi hao ya kuanzisha eneo huru la biashara hasa katika muhimili wa kwanza wa mfungamano wa masoko. Aidha, Wakuu wa Nchi waliagiza kuwa mihimili mengine ambayo ni maendeleo ya viwanda na

uendelezaji miundombinu uharakishwe ili Nchi wanachama ziweze kunufaika na soko la UTATU.

Mhe. Spika, katika mkutano huo, Wakuu wa Nchi wanachama walitia saini mkataba wa kuanzisha rasmi majadiliano ya eneo huru la biashara. Kipindi cha majadiliano hayo, kilitakiwa kiwe kati ya mwaka mmoja na mitatu. Aidha, Wakuu wa Nchi walikubali majadiliano hayo kufanywe baina ya Nchi na Nchi au baina ya kanda *(Blocs).* Pia, Nchi wanachama zilikubaliana kuharakisha utayarishaji wa taratibu, kanuni na mfumo wa kitaasisi wa kuongoza majadiliano ya UTATU.

Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba makubaliano hayo ni muhimu sana kwa manufaa ya Zanzibar. Wataalum wa Zanzibar watashiriki kikamilifu katika majadiliano hayo ili kuhakikisha kuwa Zanzibar inafaidika na mpango huu. Soko hili ni kubwa ambalo linajumuisha nchi 26 lenye idadi ya watu takriban 600 milioni na wastani wa pato la Taifa linalofikia Dola za Kimarekani Trilioni moja. Uanzishaji wa soko huru la UTATU utakuza biashara, kuongeza uwekezaji katika viwanda na kukuza miundombinu katika Nchi wanachama. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imo katika jitihada za kuzitaka Jumuiya za UTATU kukiingiza Kiswahili kuwa moja ya lugha za majadiliano.

Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)*

Mhe. Spika, katika kipindi hichi Jamhuri ya Burundi ilichukua rasmi Uenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2011/2012 baada ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumaliza muda wake 2010/2011. Mkutano wa Wakuu wa Nchi wanachama uliofanyika tarehe 19 Aprili, 2011 ulimteua Balozi Dk. Richard Sezibera kutoka Jamhuri ya Rwanda kuwa Katibu Mkuu mpya wa Jumuiya hiyo baada ya Balozi Juma Volter Mwapachu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumaliza muda wake. Aidha, Dk. Enosh Bukuku aliyekuwa Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo.

Mhe. Spika, kabla ya mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(Summit),* palifanyika kongamano la Biashara na Uwekezaji lililohudhuriwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Kenya Mhe. Mwai Kibaki, Rais wa Jamhuri ya Burundi Mhe. Pierre Nkurunziza, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein na Waziri Mkuu wa Rwanda Bernard Makuza. Mkutano huo ulifunguliwa na Mhe. Dk. Jakaya Mrisho Kikwete na viongozi hao walizungumzia mambo ya Biashara na Uwekezaji. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipata heshimaya kuufunga mkutano huo.

Mhe. Spika, Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki imeanza kazi rasmi tokea mwezi Julai, 2010 baada ya kuridhiwa na nchi wanachama. Hata hivyo, kuna baadhi ya viambatisho ambavyo majadiliano yake yalikuwa hayajamalizika. Viambatisho hivyo ni:-

- Utambuzi wa taaluma na ujuzi.
- Mafao ya Hifadhi ya Jamii.
- Jadweli la uregezaji wa masharti ya biashara katika sekta ya huduma.
- Jadweli la kufungua ajira.

Mhe. Spika, majadiliano yaliendelea katika viambatisho hivyo katika ngazi ya watalaamu, Makatibu Wakuu, Mawaziri wa Sekta mbali mbali na matokeo yake ni kama ifuatavyo:-

- Kiambatisho cha utambuzi wa taaluma na ujuzi, kanuni zake zimekamilika na nchi wanachama walikubaliana kuingia mikataba ya utambuzi ya taaluma na ujuzi miongoni mwao.
- Kiambatisho cha mafao ya Hifadhi ya Jamii majadiliano hayajakamilika. Hali hii inatokana na Nchi wanachama kubaini kuwa Itifaki ya Soko la Pamoja haitoi muongozo wa Kisera na Kisheria kuwezesha maandalizi ya kanuni za uratibu wa mafao ya Hifadhi ya Jamii. Hivyo, Nchi wanachama wamekubaliana ufanyike uchambuzi wa kina kuhusu suala hili.
- Kiambatisho cha maeneo ya nyongeza katika uregezaji wa masharti ya kibiashara ya huduma majadiliano yamekamilika. Nchi wanachama zimekubaliana kuongeza sekta nne katika jadweli. Sekta hizo ni ujenzi na huduma za kiufundi, huduma za mazingira, afya na huduma za jamii na burudani, utamaduni na michezo. Nchi zote wanachama zimewasilisha maeneo ya nyongeza ya kuregeza masharti ya biashara ya huduma.
- Kiambatisho cha maeneo ya nyongeza jadweli la kufungua ajira majadiliano yamekamilika na hakuna Nchi mwanachama iliyokubali kufungua maeneo zaidi ya ajira.

Mhe. Spika, Umoja wa Sarafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni moja kati ya mambo ya msingi yaliyoainishwa katika Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya hii. Majadiliano yanaendelea katika ngazi ya wataalamu kuhusu Itifaki ya kuanzishwa kwa Umoja wa Sarafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)* imeunda Kamati Maalum kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Wajumbe kutoka Tanzania Bara ni Wizara ya Fedha na Uchumi, Tume ya Mipango na Benki Kuu, wajumbe kutoka Zanzibar ni Ofisi ya Rais

Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Tume ya Mipango Zanzibar. Kamati hiyo itapitia tena mapendekezo ya Itifaki ya uanzishaji wa Umoja wa Sarafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kutoa ushauri wake kwa Serikali.

Mhe. Spika, uundwaji wa Shirikisho la Kisiasa la Jumuiya ya Afrika Mashariki bado ni tete ambapo baadhi ya Nchi wanachama wanaunga mkono hatua za uharakishaji wake. Wakuu wa Nchi katika mkutano wao wa dharura wa tisa walipokea taarifa ya mkutano wa 20 wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika kuhusiana na Kamati ya wataalamu iliyoundwa ya kuainisha hofu, kero na changamoto za kuanzishwa Shirikisho la Kisiasa la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wakuu wa Nchi walibainisha kuwa taarifa ya watalaamu haikuainisha mikakati ya kukabiliana na hofu, kero na changamoto hizo. Hivyo waliagiza Baraza la Mawaziri kuunda Kamati mpya itakayotoa mapendekezo thabiti ya kukabiliana na hayo. Katika Kamati hiyo Zanzibar itawakilishwa na Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria.

Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Pwani za Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Rim Association for Regional Co-operation)*

Mhe. Spika, mkutano wa Makatibu Wakuu wa Nchi za Jumuiya za Ukanda wa Pwani za Bahari ya Hindi ulifanyika Canberra, Australia kuanzia tarehe 30 Machi, 2011 hadi tarehe 31 Machi, 2011. Miongoni mwa mambo muhimu yaliyozungumzwa katika mkutano ni suala la kupambana na uharamia katika Bahari ya Hindi. Nchi ya Yemen ilipendekeza kujenga kituo cha kubadilishana taarifa kuhusu uharamia. Hata hivyo, baadhi ya nchi wanachama zilikuwa na wasi wasi kuwa hatua hiyo inaweza ikaingiliana na juhudi za Kimataifa za kupambana na uharamia. Kwa kutambua athari za uharamia katika ukanda huu, nchi wanachama zilipendekeza suala hili lipelekwe katika mkutano wa Mawaziri wa nchi wanachama wa Jumuiya hiyo utakaofanyika New Delhi, India mwezi wa Septemba, 2011.

Mhe. Spika, mkutano huo vile vile ulitawaliwa na ajenda ya utekelezaji wa miradi ya Jumuiya hiyo na namna Nchi wanachama watakavyoweza kuutumia Mfuko maalum wa fedha wa Jumuiya hiyo katika uendelezaji wa miradi. Nchi wanachama ziliipongeza Nchi ya Singapore kwa kutekeleza ahadi walioitoa katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri uliofanyika Sanaa, Yemen kwa kuanzisha kituo cha mafunzo maalumu (Tailor Made) kwa ajili ya Nchi wanachama.

Diaspora

Mhe. Spika, mkutano wa tatu wa Watanzania waliopo Nchi za nje ulifanyika mjini London, Uingereza kuanzia tarehe 6 Mei, 2011 hadi tarehe 7 Mei, 2011. Mkutano huo uliandaliwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa

Kimataifa kwa kushirikiana na Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza na Jumuiya ya Watanzania wanaoishi Nchini humo. Mkutano huo ulitoa dira ya namna ambavyo Watanzania ikiwa pamoja na Wazanzibari wanavyoweza kuhusishwa katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi Nchini.

Mkutano huo ulipata baraka ya kufunguliwa na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mheshimiwa Bernard Membe. Katika mkutano huo, Zanzibar iliwakilishwa na Mkurugenzi Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi Nchi za Nje, Mkurugenzi Mtendaji kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar, Mkurugenzi wa Uenezi na Huduma kwa Wawekezaji kutoka Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) na Afisa Masoko Muandamizi kutoka Kamisheni ya Utalii. Kwa upande wake, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imewaahidi Wazanzibari wanaoishi Uingereza walioshiriki katika mkutano huo kuhusu utayari wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kushirikiana nao na itawashirikisha katika kuandaa Mpango Mkakati wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi (*DIASPORA*).

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi za Nje imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuratibu na kufuatilia shughuli za ushirikiano wa Jumuiya mbali mbali za kikanda kwa lengo la kuifanya Zanzibar ishiriki kikamilifu na kufaidika na ushiriki huo.
- Kuendelea na kuimarisha juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukuza uhusiano mwema na Nchi marafiki na Taasisi za kimataifa.
- Kuendeleza juhudi na kukuza mashirikiano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa ajili ya maandalizi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki katika mikutano ya kimataifa.
- Kutayarisha Mpango Mkakati utakaowawezesha Wazanzibari wanaoishi nchi za nje kushiriki katika kuiletea Zanzibar maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
- Kufanya utafiti ili kuwatambua Wazanzibari wanaoishi nchi za nje, utaalamu wao na michango yao katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa Zanzibar
- Kuitangaza dhana ya Diaspora kwa wadau mbali mbali ndani na nje ya Nchi.

Mhe. Spika, ili kutekeleza malengo yake, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nchi

za Nje naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS.671 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ina jukumu la kuongoza, kufuatilia na kuratibu uendeshaji wa shughuli za Mamlaka ya Tawala za Mikoa, Wilaya na Serikali za Mitaa zikiwemo Halmashauri za Wilaya, Baraza la Manispaa na Mabaraza ya Miji kwa Pemba.

Mhe. Spika, Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2010/2011, iliidhinishiwa TZS 161.9 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Idara imeingiziwa TZS 61.5 milioni sawa na asilimia 38 ya makadirio ya matumizi na imefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

- Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa na Serikali za Mikoa kwa kushirikiana na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
- Kuandaa semina tano za mafunzo kwa masheha wote 332 na madiwani wote 141 wa Unguja na Pemba kuhusiana na dhana ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na pia wajibu na majukumu ya Sheha na Diwani.
- Kuwapatia mafunzo Watendaji 18 juu ya kutumia mbinu shirikishi jamii kwa kuangalia fursa na vikwazo vya maendeleo ya Mama na Mtoto.
- Watendaji 82 wamepatiwa elimu juu ya kujikinga na maambukizi ya UKIMWI na VVU.
- Kukagua na kuifanyia tathmimi ya utekelezaji Miradi 140 iliyoanzishwa na kuibuliwa na wananchi kupitia Halmashauri zao, *MACEMP* na TASAF.
- Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wawili katika ngazi ya Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Rasilimali watu.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendelea kusimamia Mpango wa Mageuzi ya Serikali za Mitaa na Serikali za Mikoa kwa kuweka mambo ya msingi kama vile miundo, taratibu za mapato na matumizi ili utekelezaji wa mpango huo uanze kwa majaribio mwaka 2012/2013.
- Kuhakikisha kwamba Mikoa kwa kushirikiana na Wizara husika zinawaelimisha wananchi katika suala zima la utunzaji

wa mazingira na kuepuka uharibifu kama ilivyojitokeza huko Kangagani, Mwambe na Micheweni.

- Kuendelea kuziimarisha Serikali za Mitaa kwa kuzipatia ruzuku, wataalamu wa fani mbalimbali ikiwemo taaluma ya ubunifu wa miradi endelevu na kudumisha usafi wa mazingira.
- Kuzijengea uwezo Serikali za Mitaa 13 katika kujiongoza kwa ajili ya kuweza kujiendesha wenyewe ikiwa ni pamoja na kukuza kiwango cha kukusanya mapato zaidi, matumizi bora ya mapato na mbinu ya kukuza uwajibikaji wa watendaji.
- Kuandaa semina 10 za mafunzo zenye lengo la kuimarisha mahusiano ya kiutendaji kati ya wananchi, Madiwani na watendaji wa Halmashauri.
- Kuratibu ukamilishaji wa sheria ndogo ndogo za Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, kama ilivyoelezwa katika bajeti ya Serikali, mpango wa kuimarisha huduma za miji Zanzibar (*Zanzibar Urban Service Program – ZUSP*) unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2011. Mpango huu utagharimu US$ 38 milioni ambao ni mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Matarajio ya mpango huu utakapokamilika mwaka 2016 ni kuiwezesha na kuipa haiba nzuri miji yetu na kujenga uwezo wa Baraza la Manispaa na Mabaraza ya Miji ya Wete, Chake-Chake na Mkoani. Hatua za kukamilisha hadudi rejea za wataalamu pamoja nyaraka za tenda zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwezi wa Julai, 2011. Idara hii itaratibu kikamilifu utekelezaji wa mpango huu. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Mradi huu umekusudia kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Ujenzi wa msingi wa maji ya mvua unaoanzia Magomeni, kwa Binti Hamrani, Jang'ombe hadi Kilimani wenye urefu wa mita 4,628.
- Ukarabati wa jengo la Ofisi Kuu Darajani pamoja na Karakana Kuu ya Manispaa iliopo Saateni.
- Kuanza ujenzi wa msingi wa maji ya mvua kutoka Magogoni hadi Mianzini Skuli ya Lumumba wenye urefu wa mita 9,147.
- Kujenga msingi wa maji ya mvua kutoka Sogea hadi Kidongo Chekundu wenye urefu wa mita 767.
- Kuanza ujenzi wa msingi wa maji ya mvua kutoka Uwanja wa Mnazi mmoja hadi pwani ya Kizingo wenye urefu wa mita 810.
- Kuanza ujenzi wa msingi wa maji ya mvua kutoka Darajabovu kwa Mzushi hadi Mtopepo wenye urefu wa mita 1,490.
- Kuweka taa za barabarani katika maeneo ya Mji Mkongwe yakiwemo Shangani na Kiponda.

- Kuanza ukarabati na ujenzi wa vituo 75 vya kuhifadhia taka kati ya vituo 193 katika maeneo ya Mji Mkongwe na Nga'mbo.
- Ununuzi wa vifaa vya kutendea kazi vikiwemo gari kumi na tatu (13) za kuzolea taka, gari mawili (2) ya maji machafu, gari moja la kuzibulia mitaro, gari tisa (9) kwa matumizi ya Ofisi, Vespa 25 pamoja na vikapu 203 vya kuzolea taka, mikokoteni (Push Cart) 75, ndoo 1,000 za kuzolea taka (dust bin), gari moja la kutengenezea taa na gari moja la kuvutia gari (Break down).

Mhe. Spika, kufuatia ziara zilizofanywa na Mheshimiwa Rais katika Mikoa mbali mbali ambazo zilikuwa za mafanikio makubwa na zenye kufanikisha utendaji. Maagizo aliyoyatowa katika ziara hizo yameanza kufanyiwa kazi na watendaji. Kwa upande wa migogoro ya ardhi na utoaji viwanja, Wakuu wa Mikoa na Wizara husika wametakiwa kuyatatua haraka iwezekanavyo. Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaratibu kwa kufanya utafiti (KAP) juu ya Tatizo la kuongezeka maambukizi ya UKIMWI na ubakaji katika Wilaya ya Kaskazini 'B'. Maagizo mengine yaliyotolewa ni kuepuka ukataji wa miti, kudhibiti uvuvi haramu na kuondosha mimba za utotoni

Mhe. Spika, ili Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iweze kutekeleza malengo yake, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe TZS 200 milioni kwa kazi za kawaida na ruzuku ya TZS 1,041 milioni kwa Baraza la Manispaa.

SERIKALI ZA MIKOA

Mhe. Spika, Serikali za Mikoa ni mwakilishi wa Serikali Kuu katika Mikoa na zina jukumu la kusimamia na kusaidia utekelezaji wa kazi za Serikali katika Mikoa pamoja na kuimarisha ulinzi na usalama. Kuhakikisha Sera, Mipango na kanuni za Serikali zinatekelezwa. Aidha, zinahakikisha kwamba maliasili pamoja na nguvu kazi zinatumika kwa maendeleo ya jamii na Taifa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Mikoa mitano ya Zanzibar imetekeleza yafuatayo:-

MKOA WA MJINI/MAGHARIBI

Mhe. Spika, Mkoa wa Mjini Magharibi, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 uliidhinishiwa TZS 661 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2011, Mkoa huu umeingiziwa TZS 509.7 milioni sawa na asilimia 77 ya makadirio ya matumizi.

Mhe. Spika, Mkoa wa Mjini.Magharibi uliweza kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kwa mashirikiano na Sekta husika Mkoa umehamasisha wakulima kulima mpunga Ekari 2,042, kuvuna mwani tani 65.5, mazao ya matunda na biashara Ekari 2279.5. Aidha, miche 33,500 ya mikarafuu, 225,400 ya misitu na 41,000 ya mazao ya matunda na biashara imeatikwa katika vitalu vya Selem, Mwera na Mwanyanya. Watoto 12,684 wameandikishwa darasa la kwanza,visima vitano vya maji safi vimechimbwa na ujenzi wa matangi mawili umefanywa.
- Kuwapatia mafunzo watendaji 11 katika fani ya uhasibu, utawala wa umma, kompyuta, utunzaji wa kumbukumbu na rasilimali watu.
- Elimu ya UKIMWI na jinsia ilitolewa kwa wafanyakazi 25 na wananchi 104 katika shehia tatu za Mwanyanya, Welezo na Shakani.
- Kwa kushirikiana na Sekta husika imewapatia mafunzo ya Uhifadhi wa Mazingira ya Bahari watendaji 60 wa kamati za maendeleo katika Shehia ya Bububu na Nyamanzi.
- Kuwapatia mafunzo juu ya utumiaji wa mbinu bora za kisasa wavuvi 90, wafugaji 80 wa ngo'mbe na mbuzi na wafugaji wa kuku 200.
- Kuzipatia mafunzo Kamati 20 za afya za Shehia juu ya mazingira, kujiepusha na maradhi ya mripuko na malaria. Aidha, Kamati 9 zimepatiwa mafunzo ya uandaaji wa siku ya afya za vijiji.
- Kuratibu Miradi minne ya maendeleo ya ujenzi wa barabara za ndani katika Shehia ya Chumbuni, ujenzi Skuli ya maandalizi Meya, Mradi wa Hospitali ya Mpendae na ujenzi wa madarasa matatu katika Skuli ya Mtoni. Miradi mengine ni kama inavyoonekana katika kiambatanisho namba 5.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Mkoa wa Mjini Magharibi unatarajia kutekeleza mambo saba kama ifuatavyo:-

- Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa malengo ya Sekta mbali mbali ikiwemo sekta ya elimu, afya, maji safi na salama, miundombinu, utawala bora, umeme, ustawi wa jamii, maendeleo ya vijana, wanawake na watoto, uvuvi, ufugaji, maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
- Kuratibu na kusimamia shughuli za ulinzi na usalama.
- Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi wake 15.
- Kutoa mafunzo kwa kamati za maendeleo za shehia na kuandaa semina kwa masheha 84.
- Kusimamia na kuratibu ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni.

- Kuratibu shughuli Mtambuka zikiwemo UKIMWI, mazingira na Jinsia kwa shehia 25 na wafanyakazi 97.
- Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi.

Mhe. Spika, ili Mkoa wa Mjini Magharibi uweze kutekeleza malengo iliyojipangia, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe TZS 744 milioni kwa kazi za kawaida.

MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Mkoa wa Kaskazini Unguja uliidhinishiwa TZS 616 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 150 milioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, uliingiziwa TZS 429.8 milioni sawa na asilimia 69 ya makadirio ya matumizi kwa kazi za kawaida na TZS 140 milioni kwa kazi za maendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 93 ya makadirio.

Mhe. Spika, Mkoa wa Kaskazini Unguja umeweza kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kwa mashirikiano na Sekta husika kushajihisha wakulima kulima Ekari 6,180 za mpunga, Ekari 6,180 za kilimo cha juu, Ekari 2,983 za Kilimo cha maweni na kuatika miche 60,230 ya miti matunda na misitu. Madarasa saba ya skuli kwa nguvu za wananchi yamekamilika.
- Kwa kushirikiana na sekta nyengine Miradi 13 ya maendeleo imeratibiwa. (Angalia kiambatanisho Nam. 6)
- Uendelezaji wa kazi za ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kupiga plasta, kutia dari, kuunga umeme na kutia sakafu.
- Kuwaendeleza wafanyakazi watano katika fani ya kompyuta, mipango na utawala.
- Kutia sakafu, kuweka vifaa vya umeme na kuezeka paa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Mkoa wa Kaskazini Unguja unatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa malengo ya Sekta mbali mbali ikiwemo sekta ya elimu, afya, maji safi na salama, miundombinu, utawala bora, umeme, ustawi wa jamii, maendeleo ya vijana, wanawake na watoto, uvuvi, ufugaji, maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
- Kuratibu na kusimamia shughuli za ulinzi na usalama.
- Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini ‘A’.

- Kufanya ukarabati nyumba ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Unguja.
- Kuwajengea uwezo wafanyakazi kumi kwa kuwapeleka masomoni katika fani za utawala, kompyuta.
- Kusimamia na kuratibu utekelezaji ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni.
- Kuratibu shughuli Mtambuka zikiwemo UKIMWI na Jinsia kwa Kamati 18 za shehia na wafanyakazi 63.
- kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi.
- Kwa kushirikiana na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kufanya utafiti juu ya kero ya unyanyasaji wa kijinsia na ubakaji.
- Kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kutia milango madirisha na ujenzi wa vyoo.

Mhe. Spika, ili Mkoa wa Kaskazini Unguja uweze kutekeleza malengo uliyojipangia, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe TZS 714 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 60 milioni kwa kazi za maendeleo.

MKOA WA KUSINI UNGUJA

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Mkoa wa Kusini Unguja uliidhinishiwa TZS 657 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 60 milioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Mkoa wa Kusini Unguja uliingiziwa TZS 480 milioni sawa na asilimia 73 ya makadirio ya matumizi kwa kazi za kawaida na TZS 60 milioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya matumizi kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, Mkoa wa Kusini Unguja umefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kwa kushirikiana na sekta husika Mkoa umeshajihisha wananchi kulima Ekari 2,987 za mpunga, Ekari 14,250 za mazao ya kilimo mchanganyiko, Ekari 17,894 za mazao ya matunda na upandaji wa miche 2,870 ya mikarafuu. Aidha, madarasa matano yamejengwa na watoto 3,513 wameandikishwa darasa la kwanza. Vituo vya afya vitano vimefanyiwa matengenezo na hospitali moja imepanuliwa. Serikali ya Mkoa vile vile, imesimamia mradi wa maji wa Kizimkazi Mkunguni na Dimbani na kuchimba visima vinne vya maji pamoja na kuweka miundo mbinu yake.

- Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wake 6 na wanne mafunzo ya muda mfupi pamoja na kuwapatia taaluma ya UKIMWI wafanyakazi 181.
- Ununuzi wa vifaa vya kutendea kazi pamoja na ununuzi wa Vespa moja.
- Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kutia plasta, sakafu, madirisha na milango pamoja na kuunga umeme, maji na upakaji wa rangi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Mkoa wa Kusini Unguja umepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa malengo ya Sekta mbali mbali ikiwemo sekta ya elimu, afya, maji safi na salama, miundombinu, utawala bora, umeme, ustawi wa jamii, maendeleo ya vijana, wanawake na watoto, uvuvi, ufugaji, maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
- Kuratibu na kusimamia shughuli za ulinzi na usalama.
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya kumalizia Ofisi ya Makao Makuu ya Wilaya ya Kusini.
- Kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Wilaya ya Kati.
- Kuwajengea uwezo wafanyakazi wake wanane kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi.
- Kuzijengea uwezo kamati 61 za maendeleo za Shehia
- Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni.
- Kuratibu shughuli Mtambuka zikiwemo UKIMWI na Jinsia.
- Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Miradi 11 ya maendeleo ya wananchi.
- Kutia rangi, shata za milango na madirisha, vioo vya madirisha, feni, mageti mawili makubwa, umalizaji wa ukuta wa mbele na kutia plasta.

Mhe. Spika, ili Mkoa wa Kusini Unguja uweze kutekeleza malengo uliyojipangia kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe TZS 741 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 20 milioni kwa kazi za maendeleo.

MKOA WA KASKAZINI – PEMBA

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Mkoa wa Kaskazini Pemba uliidhinishiwa TZS 834 milioni kwa kazi za kawaida, TZS 40 milioni kwa kazi

za maendeleo na TZS 233 milioni ikiwa ni ruzuku kwa Baraza la Mji la Wete. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Mkoa uliingiziwa TZS 429.8 milioni kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 52 ya makadirio ya matumizi, TZS 32 milioni sawa na asilimia 80 na ruzuku ya TZS 212 milioni sawa na asilimia 91 ya makadirio ya matumizi.

Mhe. Spika, Mkoa wa Kaskazini Pemba umetekeleza yafuatayo:-

- Kwa kushirikiana na sekta husika umehamasisha wakulima kulima Ekari 39,617 za mpunga na kuatika miche 316,950 ya matunda, mikarafuu, minazi, viungo na misitu.
- Kuratibu ujenzi wa barabara ya kilomita 30 kutoka Wete – Konde na Wete – Gando.
- Kusimamia upatikanaji wa huduma mbali mbali za Afya, ikiwemo upigaji wa dawa majumbani, chanjo dhidi ya magonjwa ya watoto na kampeni dhidi ya maambukizi mapya ya UKIMWI pamoja na ukamilishaji wa huduma za Afya katika kijiji cha Uondwe, Bwagamoyo, Shangafu na Kivumoni.
- Kuratibu maendeleo ya Elimu kwa Skuli za Msingi na Sekondari ambapo watoto 5,606 wa darasa la kwanza wameandikishwa.
- Kuwaendeleza wafanyakazi kitaaluma katika ngazi ya cheti na stashahada, katika fani za uhasibu, utawala na ukarani.
- Kulifanyia ukarabati jengo la Afisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kuligonga na kulitia plasta, kutia milango pamoja na kulipaka rangi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Mkoa wa Kaskazini Pemba umepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendelea kusimamia amani, umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi pamoja na kudumisha utulivu, ulinzi na usalama wa Raia na Mali zao.
- Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa malengo ya Sekta mbali mbali ikiwemo sekta ya elimu, afya, maji safi na salama, miundombinu, utawala bora, umeme, ustawi wa jamii, maendeleo ya vijana, wanawake na watoto, uvuvi, ufugaji, maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
- Kuratibu utekelezaji wa sekta Mtambuka zikiwemo UKIMWI na Jinsia.
- Kumaliza Ukarabati wa Jengo la Mkuu wa Mkoa pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi vikiwemo kompyuta, fotokopi na Fax.
- Kufanya ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Wete na nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Micheweni.

- Kusimamia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni.
- Kusimamia utekelezaji wa Miradi mbali mbali ya maendeleo ya jamii.

Mhe. Spika, ili Mkoa wa Kaskazini Pemba uweze kutekeleza malengo uliyojipangia, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 700 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 250 milioni ruzuku kwa Baraza la Mji Wete.

MKOA WA KUSINI PEMBA

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Mkoa wa Kusini Pemba uliidhinishiwa TZS 1,050 milioni kwa kazi za kawaida, TZS 60 milioni kwa kazi za maendeleo na TZS 523 milioni ikiwa ni ruzuku kwa Mabaraza ya Miji ya Chake-Chake na Mkoani. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Mkoa huu uliingiziwa TZS 480 milioni sawa na asilimia 46 ya makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida, TZS 60 milioni ya makadirio ya matumizi ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 100 na TZS 411 milioni sawa na asilimia 79 kwa ajili ya ruzuku.

Mhe. Spika, Mkoa wa Kusini umefanikiwa kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kwa kushirikiana na sekta husika umeratibu ulimaji wa Ekari 5,210 za muhogo, Ekari 942 za migomba, Ekari 2,170 za kunde, Ekari 1,306 za mahindi, Ekari 470 za viazi vitamu, Ekari 270 za njugu nyasa, Ekari 115 za mboga mboga, Ekari 48 za mtama, Ekari 40 za majimbi na Ekari 336 za minanasi.
- Umeratibu shughuli za kisekta zikiwemo elimu, afya, maji safi na salama, miundombinu, utawala bora, maendeleo ya kijamii na kiuchumi.
- Umeandaa vikao 9 vya ulinzi na usalama vya Mkoa na Wilaya.
- Umeendeleza wafanyakazi wake katika ngazi ya cheti, stashahada, kwa fani ya uhasibu, utawala na ukarani.
- Umeandaa semina kwa wafanyakazi juu ya umuhimu wa kupima afya zao na kupunguza unyanyapaa ili kujiepusha na maambukizi mapya ya UKIMWI.
- Ujenzi wa jengo la ziada la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba na ukarabati wa Ofisi alizohamia Mkuu wa Wilaya ya Chake-Chake.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Mkoa wa Kusini Pemba umepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kutoa Mafunzo kwa wafanyakazi wa fani mbalimbali.

- Kukamilisha ujenzi wa jengo dogo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na ujenzi wa uzio wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkoani.
- Kuratibu utekelezaji wa sekta Mtambuka zikiwemo UKIMWI na Jinsia.
- Kuratibu na kusimamia miradi mbali mbali ya maendeleo ya wananchi.
- Kusimamia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa kampeni.
- Kuendelea kusimamia amani, umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi pamoja na kudumisha utulivu, ulinzi na usalama wa raia na mali zao.
- Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa malengo ya Sekta mbali mbali ikiwemo sekta ya elimu, afya, maji safi na salama, miundombinu, utawala bora, umeme, ustawi wa jamii, maendeleo ya vijana, wanawake na watoto, uvuvi, ufugaji, maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mhe. Spika, ili Mkoa wa Kusini Pemba uweze kutekeleza malengo yake, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS.644 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 520 milioni kwa ajili ya ruzuku ya Mabaraza ya Miji ya Chake Chake na Mkoani.

BARAZA LA MANISPAA

Mhe. Spika, Baraza la Manispaa limeundwa kwa Sheria Nam. 3 ya 1995 kwa ajili ya kufanikisha majukumu ya kusimamia kazi mbali mbali za maendeleo katika mji wa Zanzibar pamoja na utoaji wa huduma za uzoaji taka, usafi wa michirizi ya maji machafu na mvua, usafi wa barabara, ukarabati wa taa za barabarani, utunzaji wa bustani na maeneo yaliyo wazi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza la Manispaa lilikadiria kukusanya TZS 1,004 milioni kutoka vyanzo vya mapato ikiwemo malipo ya leseni za maduka, maegesho ya gari na malipo ya uzoaji taka. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Baraza lilikusanya TZS 815 milioni sawa na asilimia 82 ya makadirio ya makusanyo. Aidha, Baraza liliidhinishiwa TZS 1,208 milioni ikiwa ni ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya mishahara na maposho ya wafanyakazi. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Baraza liliingiziwa TZS 906 milioni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya ruzuku.

Mhe. Spika, Baraza la Manispaa limeweza kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuwaendeleza wafanyakazi 15, kati yao 10 wamepata mafunzo ya muda mrefu na watano wamepata mafunzo ya muda mfupi

- Kuzibua na kuusafisha msingi mkubwa wa Haile - Selassie hadi Funguni wenye urefu wa kilomita 1.3 na pia kusafisha mitaro yote ya mjini yenye urefu wa kilomita 14.7.
- Kuzoa taka mita za ujazo 72,617 (cm x 3).
- Madiwani 21, masheha 45 na watendaji 15 wamepatiwa mafunzo juu ya kazi na wajibu wa Madiwani na Masheha.
- Ununuzi wa gari mbili ambazo ni gari ya mizigo na Basi la wafanyakazi.
- Ununuzi wa vifaa vya Ofisini vikiwemo vipoza hewa vinne, kompyuta nne, printa nne, fotokopi moja na samani za Ofisi.
- Kujenga vyoo na Ofisi ndani ya jengo la Manispaa
- Kutengeneza Barabara za ndani kuanzia Benki ya watu wa Zanzibar hadi Wizara ya Kilimo na Maliasili na uwekaji wa rangi za alama za kuvukia kwa miguu (*Zebra Cross*) pamoja na kuweka kifusi eneo la biashara Saateni.

Mhe. Spika, itakumbukwa kuwa katika majumuisho ya Ziara yake kwa Mkoa wa Mjini Magharibi, Mheshimiwa Rais alitoa agizo kwa Baraza la Manispaa kuimarisha usafi na kuondoa wanyama wote wakiwemo ng'ombe, mbuzi na punda wanaozurura ovyo barabarani na katika mitaa ndani ya Manispaa. Katika kutekeleza agizo hilo, Baraza la Manispaa limeanzisha mpango unaoitwa 'Manispaa Shirikishi' wenye lengo la kuwashirikisha wananchi katika kudumisha usafi. Vikundi mbali mbali vimeanzishwa kupitia Wadi ili viweze kufanya usafi katika maeneo yao.

Aidha, Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na Serikali ya Wilaya ya Mjini imewaita wafugaji wote ndani ya Manispaa na kuwataka kujisajili. Hatua hii imeanzisha mashirikiano kati ya Baraza la Manispaa na wafugaji yanayolenga katika kuwaondoa wanyama wanaozurura ovyo. Vile vile Baraza la Manispaa limeandaa mpango wa kuzisajili gari zote zinazokokotwa na wanyama kwa lengo la kuzipa vibali vitakavyowaruhusu kutoa huduma katika maeneo yaliyotengwa.

Mhe. Spika, Baraza la Manispaa kwa mwaka wa fedha 2011/2012, limekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendelea na ukarabati wa Soko la Mwanakwerekwe kwa kuziba paa na kutengeneza kuta. Soko la Mombasa, Soko la Mikunguni pamoja na kuendeleza ujenzi wa jengo la Ofisi ya mapato Darajani kwa kujenga ghorofa moja.
- Kujenga mitaro ya maji ya mvua, uwekaji wa mabomba ya maji safi na kuweka umeme na taa katika kituo cha biashara cha Manispaa kiliopo Saateni.

- Kuchangia miradi midogo midogo ya maendeleo ya Wadi 20 zilizomo ndani ya Manispaa ya Zanzibar.
- Kuimarisha na kuitunza michirizi ya maji machafu na ya mvua katika Manispaa ya Mji wa Zanzibar.
- Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi wake 13 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na wawili mafunzo ya muda mfupi katika fani za uchumi, takwimu, uhasibu, ufundi, mazingira, ukaguzi wa afya, kompyuta na utafiti.
- Kutekeleza mkakati mpya wa uzoaji taka na uondoaji mifugo ndani ya eneo la Manispaa ya Zanzibar na vitongoji vyake.

Mhe. Spika, Baraza la Manispaa limeanza mazungumzo na Makampuni ya simu ya *ZANTEL* na *TIGO* ili kujadili utata uliojitokeza katika Mikataba iliyofungwa baina ya Baraza la Manispaa na Kampuni za matangazo ya biashara ambazo zinaifanyia kazi kampuni hizo pamoja na mabadiliko ya sera za utekelezaji wa mradi wa ZUSP katika utengenezaji na uwekaji taa za barabarani.

Baraza la Manispaa linakusudia kufanya mikataba moja kwa moja na Kampuni hizo mama za simu badala ya kupitia Kampuni za Matangazo. Hatua hii itajenga uhusiano mzuri wa kibiashara na Kampuni hizo. Hivi sasa uwekaji wa mabango ya biashara utajadiliwa kupitia Kamati husika za Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo hayo, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza la Manispaa limekadiria kukusanya TZS 1,094.9 milioni kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGHARIBI

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi kwa mwaka wa fedha 2010/11, ilijipangia kukusanya TZS 367 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato na kutumia TZS 237 milioni kwa Miradi ya maendeleo sawa na asilimia 65 na TZS 130 milioni sawa na asilimia 35 kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Halmashauri imekusanya TZS 214 milioni. Kati ya hizo, TZS 169 milioni sawa na asilimia 78.9 zimetumika kwa kazi za maendeleo na TZS 45 milioni sawa na asilimia 21 zimetumika kwa matumizi mengineyo.

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi imetekeleza yafuatayo:-

- Kuendelea na ujenzi Ofisi yake ya Mombasa.
- Imesaidia ujenzi wa Skuli za Dole, Kiembesamaki, Kibweni, Sharifu Msa, Mfenesini, Kinuni, Mbuzini, Mtoni Kidatu na Magogoni.

- Imeendelea na ujenzi wa kituo cha Afya Mbuzini na Soko la Samaki Mwanakwerekwe.
- Ilichangia ujenzi wa madaraja madogo madogo na utiaji wa kifusi njia za ndani za Welezo na Mwanakwerekwe.
- Ilisaidia usambazaji wa maji safi na salama katika maeneo ya Kijito Upele, Fumba na Fuoni Kibondeni
- Imechangia vikundi vya Ushirika kupitia Waheshimiwa Madiwani wa Viti Maalumu
- Ukusanyaji wa taka katika Shehia zote pamoja ununuzi wa gari la kuzolea taka.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2011/12 Halmashauri imelenga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendeleza ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya hapo Mombasa na jengo la Hospitali ya Mbuzini.
- Ujenzi wa Silabi za kuhifadhia taka.
- Ujenzi wa nyumba za kulala wageni Bwefum.
- Ununuzi wa gari ya ukaguzi na gari ya kubebea taka pamoja na tela la kubebea wanyama.
- Kuimarisha mradi wa uzoaji taka na usafi wa mazingira.
- Ununuzi wa mashine ya kutengenezea matofali.
- Itasaidia utekelezaji wa miradi kumi na sita (16) ya maendeleo ya wananchi ambayo imeoneshwa katika kiambatanisho Nam. 7.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi imejipangia kukusanya TZS 400 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato na kutumia TZS 245.5 milioni kwa kazi za maendeleo katika Wadi 15 na kutumia TZS 154.5 milioni kwa kazi za kawaida

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI 'A'

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya Kaskazini 'A', kwa mwaka wa fedha 2010/11, ililenga kukusanya TZS 50 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato.

Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Halmashauri imekusanya TZS 62.7 milioni ikiwa ni sawa na asilimia 124 ya makadirio ya makusanyo. Kati ya hizo, TZS 28 milioni zimetumika kwa kazi za maendeleo na TZS 24.6 milioni zimetumika kwa matumizi ya kazi ya kawaida.

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'A' imeweza kutekeleza miradi ya ziada ya Ujenzi wa barabara ndogo ya Pita na Zako hadi Kizimbani,

Hospitali ya Kivunge na Skuli ya Chutama ambapo TZS 10 milioni zimetumika baada ya kikao cha Baraza la Madiwani kuidhinisha matumizi hayo. Viambatanisho Nam. 8A na 8B vinaeleza kwa kina miradi iliyotekelezwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri imelenga kutekeleza yafuatayo:-

- Ukarabati wa jengo la Makao Makuu ya Ofisi ya Halmashauri hapo Mkokotoni.
- Kusaidia ukarabati wa majengo ya Skuli za Kinyasini na Chaani Masingini.
- Kusaidia uchimbaji wa visima vitatu vya Tumbatu Gomani.
- Ukarabati wa masoko ya Kinyasini na Mkwajuni.
- Ujenzi wa Skuli za Matemwe Kizimiani, Moga, Kidago na Chaani Mnarani.
- Ujenzi wa vyoo katika Chuo cha Mafunzo ya Ualimu Mkwajuni.
- Ujenzi wa kituo cha Halmashauri Nungwi.
- Kusaidia gharama za mafunzo kwa wanafunzi, usambazaji wa maji katika wadi ya Muwange, uwekaji wa kifusi katika njia ndogo za ndani, Chaani Mtakuja, Kinyasini Ziwani, Pita na zako pamoja na ununuzi wa mipira ya maji Chaani Kubwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Kaskazini 'A' imelenga kukusanya TZS 189.7 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato na kutumia TZS 94 Milioni kwa kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na TZS 95.7 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KASKAZINI 'B'

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya Kaskazini 'B' kwa mwaka wa fedha 2010/11, ililenga kukusanya TZS 60 milioni kutokana na vyanzo vyake vya mapato. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Halmashauri imekusanya TZS 77.7 milioni ikiwa ni sawa na asilimia 129.5 ya makadirio ya makusanyo. Kati ya hizo TZS 48.9 milioni zilitumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 63 ya makusanyo na TZS 28.8 milioni sawa na asilimia 37 zimetumika kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' imelenga kutekeleza yafuatayo:-

- Ujenzi wa Skuli mbali mbali, usambazaji maji safi na salama, ujenzi wa visima vipya vya maji, usambazaji umeme katika Skuli mbali mbali, ujenzi wa kituo cha Afya Bumbwini

Kiongwe na uendelezaji wa jengo la Ukumbi wa Mkutano na Ofisi za Halmashauri.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' imelenga kukusanya TZS 214 milioni kutokana na makusanyo yanayotokana na vianzio vyake vya mapato na kutumia TZS 100 milioni kwa kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na TZS 114 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, ililenga kukusanya shilingi 56.2 milioni kutokana na vyanzo vyake vya mapato na kutumia shilingi 23.3 milioni kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi na shilingi 32.9 milioni kwa kazi za kawaida**.** Hadi kufikia mwezi Machi 2011 ilikusanya shilingi 64 milioni kati ya hizo shilingi 20 milioni zilitumika kwa kazi za maendeleo na shilingi 44 milioni ikiwa ni sawa na asilimia 46.6 zimetumika kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini imefanya shughuli zifuatazo:-

- Kusaidia miradi minne ya wananchi ikiwemo Kituo cha Afya Bwejuu, ukarabati wa Skuli ya Kiongoni Mtegani, Ukamilishaji wa vyoo Skuli ya Paje na ujenzi wa wodi ya kituo cha afya Mtende.
- Ukusanyaji wa taka katika Hoteli za Kitalii ili kuzuwia utupaji taka ovyo pamoja na uchafuzi wa mazingira. Mradi huu kwa sasa unasimamiwa na watu binafsi kupitia ubia na Halmashauri ya Wilaya.
- Kutekeleza miradi ya maendeleo katika kila Wadi na Kuendelea kutayarisha miji ya kisasa kwa kuzingatia ujenzi utakaofuata sheria na kanuni.
- Kununua vifaa vya ofisi ikiwa ni pamoja na gari moja, kompyuta na vifaa vya kuandikia.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja imepanga kukusanya shilingi 94.6 milioni kutokana na vyanzo vyake vya mapato na kutumia shilingi 50.5 milioni kwa miradi 13ya maendeleo ya wananchi na shilingi 40.1 milioni kwa kazi za kawaida.

HALMASHAURI YA WILAYA YA KATI

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kati, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, ililenga kukusanya shilingi 154.9 milioni. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Halmashauri ilikusanya shilingi 131 milioni sawa na asilimia 84.6 ya lengo

ililojipangia. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Kati ilitumia shilingi 34 milioni kwa kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shilingi 97 milioni kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kati imetekeleza mambo yafuatayo:-

- Imesaidia usambazaji wa umeme Uroa, ujenzi wa Ofisi ya Mazingira Cheju, Madrasat Ndijani Muembe Punda, Pagali na Ng'ambwa, Skuli ya Msingi Mwera-Pongwe, Tunguu, Jumbi, Kikungwi, Michamvi, Kiboje, Miwani, Bungi, Dunga Kiembeni na Skuli ya Maandalizi Umbuji.
- Imesaidia uchimbaji na ujenzi wa Kisima Uzi, Banda la Kuku Tunduni.
- Ujenzi wa maduka Kipilipilini Chwaka, Soko Ukongoroni, utiaji wa kifusi njia kuu Mchangani, uendelezaji wa ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri na usafishaji wa njia katika mji mpya Tunguu.
- Kusaidia ujenzi wa Kituo cha Polisi Uzi, Ujenzi wa vyoo katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kati.
- Ununuzi wa majoho kwa Waheshimiwa Madiwani na vifaa vya Ofisi ikiwa ni pamoja na vifaa vya kuandikia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Kati inatarajia kukusanya shilingi 174.5 milioni kutokana na vianzio vyake vya mapato na kutumia shilingi 87 milioni kwa utekelezaji wa miradi 14 ya wananchi na shilingi 87.5 milioni kwa kazi za kawaida.

BARAZA LA MJI WETE PEMBA

Mhe. Spika, Baraza la Mji Wete kwa mwaka wa fedha 2010/2011, lilijipangia kukusanya shilingi 40 milioni kupitia vyanzo vyake vya mapato na kutumia shilingi 20 milioni kwa kazi za maendeleo na shilingi 20 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Baraza limekusanya shilingi 42 milioni sawa na asilimia 105 ya malengo iliyojipangia na kutumia shilingi 22 milioni kwa kazi za maendeleo na shilingi 20 milioni kwa kazi za kawaida. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Baraza la Mji Wete limeweza kutekeleza yafuatayo:-

- Ukarabati wa ukumbi wa mkutano, soko la samaki Mtemani na soko la Kitutia.
- Uwekaji wa kifusi kituo cha magari cha Kitutia.
- Kuwahamasisha wananchi 178 kujua afya zao kwa kuwapatia elimu ya afya na kudumisha usafi wa mazingira na kujilinda na maradhi ya mripuko na Malaria.

- Kuwajengea uwezo watendaji 18 kwa kuwapatia mafunzo mafupi.
- Kufanya usafi wa mji wa Wete kwa kusafisha barabara, kuzoa taka na kuitunza mitaro ya maji ya mvua na maji machafu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza la Mji Wete limejipangia kufanya yafuatayo:-

- Matengenezo ya ukumbi wa mikutano wa Jamhuri *Hall*
- Kuendelea kuimarisha miradi ya jamii, Wete Mjini na kuweka kifusi Kituo cha Magari na ujenzi wa vyoo Wete Mjini.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza la Mji la Wete limelenga kukusanya shilingi 45.6 milioni na kutumia shilingi 20.6 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 25 milioni kwa miradi minne ya maendeleo.

HALMASHAURI YA WILAYA YA WETE – PEMBA

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Halmashauri ya Wilaya ya Wete ilipanga kukusanya shilingi 24 milioni kupitia vyanzo vyake vya mapato. Kati ya fedha hizo shilingi 11 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 13 milioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Halmashauri imekusanya shilingi 25 milioni sawa na asilimia 104 ya makadirio.

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Wete imetekeleza yafuatayo:-

- Imesaidia ujenzi wa madarasa Skuli za Uondwe, Kisiwani, Daya, Gando, Jojo, Kokota na Mkote.
- Uwekaji kifusi barabara ya Makaani hadi Ole.
- Imenunua Pikipiki na vifaa vya kuandikia.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Wete imejipangia kutekeleza yafuatayo:-

- Ujenzi wa msingi wa Ofisi ya Halmashauri.
- Kusaidia miradi ya wananchi pamoja na huduma za afya katika maeneo ya Halmashauri.

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Wete imejipangia kukusanya shilingi 40 milioni kutokana na vyanzo vyake vya mapato na kutumia shilingi 20 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 20 milioni kwa kazi za maendeleo.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ilijipangia kukusanya shilingi 20 milioni kupitia vyanzo vyake vya mapato na kutumia shilingi 9 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 11 milioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imekusanya shilingi 30 milioni ikiwa ni sawa na asilimia 150 ya makadirio.

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imetekeleza yafuatayo:-

- Kulifanyia matengenezo jengo la Ofisi ya Halmashauri pamoja na kuendelea na hatua ya upatikanaji wa hati miliki za majengo ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.
- Kusaidia ujenzi wa kituo cha afya Chimba.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imepanga kutekeleza yafuatayo:-

- Kusaidia miradi midogo midogo ya wananchi ya ujenzi wa Chinjio la Mziwanda, ujenzi wa choo Konde Mjini, Skuli ya Sekondari Micheweni na Skuli ya Msingi Mawe Matatu Makangale.
- Kununua vitendea kazi zikiwemo vespa mbili (2).

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, imepanga kukusanya shilingi 30 milioni. Kati ya hizo, shilingi 12 milioni zitatumika kwa kazi za kawaida na shilingi 18 milioni zitatumika kwa kazi za maendeleo.

BARAZA LA MJI CHAKE-CHAKE

Mhe. Spika, Baraza la Mji Chake Chake, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, lilijipangia kukusanya shilingi 50 milioni na kupanga kutumia shilingi 20 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 30 milioni kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Baraza limekusanya shilingi 60.4 milioni na kutumia shilingi 40.9 milioni sawa na asilimia 67.7 kwa kazi kawaida na shilingi 19.5 milioni sawa na asilimia 32.3 kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, Baraza la Mji Chake Chake limetekeleza yafuatayo:-

- Limesaidia ujenzi wa soko la Machomane pamoja na banda katika eneo la soko la samaki Chake Chake.
- Ujenzi wa vidaraja Tenga na uwekaji wa kifusi njia ya Kisiwani-Michakaeni.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza la Mji Chake Chake limekusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Ujenzi wa soko la Machomane na matengenezo ya Ofisi ya Baraza
- Misaada kwa jamii, uwekaji wa kifusi njia ya Machomane na ujazaji kifusi eneo la wafanyabiashara wadogo wadogo eneo la bahari.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza la Mji Chake Chake limejipangia kukusanya shilingi 64 milioni na kutumia shilingi 32 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 32 milioni kwa kazi za maendeleo.

HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAKE-CHAKE

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake ilijipangia kukusanya shilingi 24.6 milioni. Hadi kufikia mwezi Machi 2011 Halmashauri ilikusanya shilingi 23.6 milioni sawa na asilimia 96 ya makadirio ya makusanyo. Kati ya hizo shilingi 12.6 milioni zilitumika kwa kazi za maendeleo na shilingi 11 milioni zilitumika kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake ilitekeleza mambo yafuatayo:-

- Imesaidia ujenzi wa Skuli ya Chekechea Mavungwa, Skuli ya Kwale, Skuli ya Kilindi, Skuli ya Chanjamjawiri, Skuli ya Shungi, Skuli ya Uwandani, Skuli ya Pujini, Skuli ya Ndagoni, Skuli ya Furaha na Kituo cha Afya cha Kibokoni.
- Ujenzi wa soko la Wesha na kufanya ukarabati Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Chake-Chake.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Chake Chake imepanga kukusanya shilingi 35 milioni. Kati ya hizo shilingi 11.9 milioni zitatumika kwa mradi wa ujenzi wa utanuzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Chake-Chake na umalizaji wa ujenzi wa kituo cha afya cha Kibokoni - Vitongoji na shilingi 23 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida.

BARAZA LA MJI MKOANI

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza la Mji Mkoani, limejipangia kukusanya shilingi 17 milioni na kutumia shilingi 7.5 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 9.5 milioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Baraza limekusanya shilingi 20 milioni sawa na asilimia 118 ya makadirio.

Mhe. Spika, Baraza la Mji Mkoani, limetekeleza mambo yafuatayo:-

- Ukarabati wa ukumbi wa mkutano wa Umoja ni Nguvu Ng'ombeni.
- Ujenzi wa Soko la Samaki na Matunda Mbuyuni
- Ujenzi wa Ofisi ya Baraza la Mji Makadara.
- Ujenzi wa slabi mbili za kuhifadhia taka.
- Kusaidia miradi ya jamii Wadi za Makombeni na Mbuguwani.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza la Mji la Mkoani limekusudia kutekeleza yafuatayo:-

- Ukarabati wa paa pamoja na upakaji rangi soko la samaki na matunda Mbuyuni Mkoani.
- Ujenzi wa slabi tano za kuhifadhia taka Kinyasini, Makadara, Kanisani, Ng'ombeni na Kipitacho.
- Uwekaji wa kifusi barabara ya Makadara.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Baraza la Mji Mkoani linalenga kukusanya shilingi 19 milioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato na kutumia shilingi 9 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 10 milioni kwa kazi za maendeleo.

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKOANI

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani ilijipangia kukusanya shilingi 19 milioni na kutumia shilingi 9 milioni kwa kazi za maendeleo na shilingi 10 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani imekusanya shilingi 19.9 milioni sawa na asilimia 105 ya makadirio ya makusanyo. Kati ya hizo shilingi 12 milioni zimetumika kwa kazi za maendeleo na shilingi 7.6 milioni kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani imetekeleza yafuatayo:-

- Imeendeleza ujenzi wa Soko la Mkanyageni na Kangani.
- Imesaidia ujenzi wa skuli za Ukutini, Michenzani, Mkanyageni, Kisima Msengele, Kisiwapanza, Bandarini – Wambaa.
- Ujenzi wa Madrasa Chumbageni, Matele Chambani na Ngezi.
- Ujenzi wa vyoo vya Msikiti Kigope na nyumba ya watoto yatima Ngwachani.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendelea na ujenzi wa Soko la Samaki na Matunda Mkanyageni.
- Kusaidia ujenzi wa Msikiti Michezani, Madrasa Chumbageni, Skuli ya Sekondari Kengeja, Skuli ya Msingi Mahduthi, daraja la Mto Mkuu Kengeja, madrasa Kengeja na Mwambe.
- Kusaidia gharama za Mitihani ya Majaribio ya Wilaya ya Mkoani.
- Kuweka kifusi barabara ya Likoni Kengeja na msikiti Maambani, Chambani.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani imepanga kukusanya shilingi 30 milioni. Kati ya hizo, shilingi 14 milioni kusaidia kazi za maendeleo ya miradi ya wananchi na shilingi 16 milioni zitatumika kwa kazi za kawaida.

IDARA YA URATIBU IDARA MAALUM ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Mhe. Spika, idara hii ina wajibu wa kusimamia na kuratibu kazi zote za Idara Maalumu za SMZ ikiwemo usimamizi wa utekelezaji wa Sheria, Sera na Kanuni za Utumishi za Idara Maalum. Majukumu mengine ni pamoja na kuratibu na kusimamia vikao vya Tume ya Utumishi ya Idara Maalumu za SMZ na vikao vya Mahkama ya Rufaa ya Idara Maalumu za SMZ.

Aidha, inasimamia majukumu ya kisera ya kuoainisha miundo ya utumishi, maslahi ya maafisa na wapiganaji, kuwajengea uwezo kitaaluma na kuratibu masuala ya michezo.

Idara Maalumu za SMZ inajumuisha Vikosi vifuatavyo:-

- Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM)
- Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)
- Chuo cha Mafunzo (MFZ)
- Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU)
- Kikosi cha Valantia (KVZ)

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Idara ya Uratibu wa Idara Maalumu imefanya kazi zifuatazo:-

- Imeratibu shughuli zote za Idara Maalumu za SMZ.

- Imesimamia vikao vitano vya Tume ya Utumishi ya Idara Maalumu za SMZ.
- Imesimamia uanzishaji rasmi wa Mahkama ya Rufaa ya Idara Maalumu za SMZ.
- Imeratibu shughuli za michezo ya Idara Maalumu za SMZ.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Uratibu Idara Maalumu za SMZ inatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendelea kusimamia na kuratibu kazi za Idara Maalumu za SMZ.
- Kufanikisha vikao vitano vya Tume ya Utumishi ya Idara Maalumu za SMZ.
- Kufanikisha vikao vitano vya Mahakama ya Rufaa ya Idara Maalumu za SMZ.
- Kusimamia kusitishwa, kukatwa kwa posho la chakula kwa maafisa na wapiganaji wanapokuwa mafunzoni.

Mhe. Spika, ili idara hii iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 145 milioni kwa kazi za kawaida.

KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

Mhe. Spika, Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo kimeanzishwa kwa Sheria Nam. 1 ya 2003 na kina majukumu ya kulinda usalama wa bahari ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Kuzuia njia zote zinazoweza kutumika kupitishia magendo, kusaidia usalama wa vyombo vya baharini vya abiria na mizigo na kufanya uokoaji baharini.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo kiliidhinishiwa shilingi 6,109 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 250 milioni kwa kazi za maendeleo. Hadi mwezi Machi 2011, kikosi kimeingiziwa shilingi 4,574 milioni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na shilingi 250 milioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya matumizi kwa kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kikosi kimepatiwa vipuri, mafuta ya vyombo, pamoja na kufanya matengenezo kwa vyombo vikubwa na vidogo. Aidha, Mawasiliano ya Redio yameimarika ambapo Kambi zote zinauwezo wa kuwasiliana kwa wakati mmoja.

Pia, kimefanikiwa kudhibiti matukio ya magendo 15, Unguja na Pemba, ambapo matukio hayo ni ya utoroshaji wa karafuu kavu, jumla ya magunia 227

sawa na kilo 9,695, utoroshaji wa Sukari Paketi 389, betri katuni 200, uingizaji wa ng'ombe 41, mafuta ya Petroli pipa 10 na mifuko ya plastic vifurushi 570. Matukio yote hayo yalifikishwa katika vyombo husika kwa hatua za kisheria. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kikosi kimewapatia mafunzo ya kazi katika fani mbali mbali wapiganaji wake pamoja na kuwapatia sare kamili za kufanyia kazi. Aidha, Kikosi kimeendelea na kazi za ukarabati wa nyumba ya kukaa maafisa pamoja na vyoo kwa wapiganaji waliopo mafunzoni katika Kambi ya Kama.

Mhe. Spika, Mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Kibweni umekamilisha ujenzi wa jengo la Huduma za Mama na Mtoto (MCH). Hatua inayoendelea ni ujenzi wa ghorofa ya kwanza ya jengo la Hospitali. Hivi sasa huduma za mama na mtoto pamoja na huduma nyengine za afya zimeanza kutolewa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Kikosi kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendeleza kuwapatia sare na vifaa vya kulalia wapiganaji.
- Kuendeleza kufanya ukarabati majengo ya kikosi.
- Kuvipeleka vyombo vikubwa chelezoni kimatengenezo.
- Kuimarisha sehemu ya uzamiaji (*diver*) kikosini.
- Kuendeleza kuimarisha nguvu za ulinzi na doria baharini.
- Kuwaongezea uwezo wa kiutendaji kwa kuwapatia elimu ya kazi wapiganaji ndani na nje ya kikosi.
- Kununua vifaa kwa ajili ya kuendesha Hospitali ya Kibweni, kujenga fulio (*laundry*) na jiko la kuchomea taka za Hospitali (*incinerator*).

Mhe. Spika, ili Kikosi cha KMKM kiweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 6,687 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 200 milioni kwa kazi za maendeleo.

JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU)

Mhe. Spika, Jeshi la Kujenga Uchumi limeanzishwa kwa Sheria Nam. 6 ya mwaka 2003 na lina jukumu kubwa la kuwafunza vijana katika nyanja za uchumi, kilimo, viwanda vidogo vidogo, uvuvi na mafunzo ya amali pamoja na kutoa ulinzi kwa Taasisi za Serikali. Vijana hao hufunzwa kwa kufuata mfumo wa ujenzi wa taifa, ili waweze kujiari wenyewe wakati wanapomaliza mafunzo yao.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Jeshi la Kujenga Uchumi liliidhinishiwa shilingi 4,535 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 650

milioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Jeshi la Kujenga Uchumi limeingiziwa shilingi 3,530 milioni sawa na asilimia 78 ya matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 560 milioni sawa na asilimia 86 ya makadirio ya matumizi ya kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Jeshi la Kujenga Uchumi limewapatia elimu wapiganaji wake katika fani, viwango na vyuo tofauti. Aidha, Jeshi la Kujenga Uchumi lilinunua kuku 2,000 machotara kwa ajili ya uzalishaji wa mayai ili kuchukua nafasi ya kuku waliokwisha kuzeeka na waliokufa kutokana na maradhi. Jumla ya kuku 4,500 katika awamu tofauti walifugwa katika Makambi tofauti ya Jeshi hili. JKU limelima Ekari 135 za mpunga, Ekari 140 za mahindi, Ekari 29 za mtama, Ekari 78 za muhogo, Ekari 33 za kunde, Ekari 15 za viazi vitamu na Ekari 5 za bustani ya miti ya matunda.

Mhe. Spika, Jeshi la Kujenga Uchumi limetoa huduma za matibabu katika vituo vyake vya afya kwa wapiganaji wake na raia walio karibu na maeneo ya vituo hivyo. Jumla ya wagonjwa 25,987 walipatiwa huduma mbali mbali katika vituo hivyo. *(Makofi)*

Aidha, JKU inaendelea kutoa mafunzo ya ufundi kwa vijana ili waweze kujiajiri na jumla ya vijana 225 walihitimu mafunzo hayo katika Skuli yake ya Ufundi iliopo Mtoni. Sambamba na mafunzo ya uzalishaji na ufundi, Jeshi la Kujenga Uchumi limeanzisha Skuli ya Sekondari kwa ajili ya kuwaendeleza wapiganaji wake na raia kielimu. Kwa sasa, Skuli ya Sekondari ya Jeshi la Kujenga Uchumi lina jumla ya wanafunzi 101, idadi ambayo inajumuisha wanafunzi kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Mradi wa Shamba la Mfano la Mboga Mboga umeezeka nyumba mbili kati ya nyumba tatu za Wataalamu kutoka Misri. Aidha, ujenzi wa banda la mwanzo lenye vyumba vinne na Ofisi, ujenzi wa hodhi la maji lenye uwezo wa ujazo wa lita 2,500,000 umekamilika. Kukamilika kwa hodhi hilo kutasaidia kazi ya umwagiliaji. JKU kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Mali ya Asili, imelima Ekari 20 za mahindi aina ya Situka kwa ajili ya mbegu.

Mhe. Spika, JKU kwa mwaka 2011/2012, imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendelea na ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya JKU Mtoni kwa kuweka msingi wa jengo la pili la ghorofa.
- Kuwaendeleza kielimu wapiganaji katika fani na ngazi mbali mbali kwa lengo la kuongeza ufanisi.

- Kulima mazao ya aina mbali mbali ikijumuisha Ekari 135 za mpunga, Ekari 170 za mahindi, Ekari 30 za mtama, Ekari 78 za muhogo, Ekari 33 za kunde na Ekari 4 za bustani na miti ya matunda.
- Kuendeleza mradi wa ufugaji kuku ikiwemo ununuzi wa *incubator*, ili kurahisisha upatikanaji wa vifaranga
- Uunganishaji wa maji na umeme kwa ajili ya Skuli za Ufundi na Sekondari zilizoko Mtoni.
- Kununua zana kwa ajili ya kuimarisha vitengo mbali mbali katika Skuli ya Ufundi JKU Mtoni.
- Kuendeleza Shamba la mfano la Mboga Mboga Bambi kwa kujenga madarasa ya Kilimo, kulima Ekari 20 za mahindi aina ya Situka na Ekari 100 za mpunga aina ya Nerica kwa ajili ya mbegu, kujenga nyumba mbili kwa ajili ya wataalamu kutoka Misri na ukarabati wa ghala la kuhifadhia vifaa, chakula na mazao na uchimbaji wa visima vitatu, ununuzi wa mabomba ya umwagiliaji.
- Kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mradi wa Shamba la Mboga Mboga, ili uweze kuleta tija iliyokusudiwa.
- Kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Mali Asili kuendeleza utafiti wa mbegu mbali mbali za nafaka na mboga.

Mhe. Spika, ili JKU iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe shilingi 4,668 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 450 milioni kwa kazi za maendeleo. *(Makofi)*

CHUO CHA MAFUNZO

Mhe. Spika, Chuo cha Mafunzo kimeanzishwa kwa Sheria Nam. 1 ya mwaka 1980 na kina jukumu la kurekebisha, kudhibiti na kulinda wanafunzi na mahabusu wanaopelekwa chuoni kwa mujibu wa sheria. Pia, inashirikiana na vikosi vyengine vya SMZ na SMT katika kuimarisha ulinzi wa nchi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Chuo cha Mafunzo kiliidhinishiwa shilingi 3,766 milioni kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Chuo kimeingiziwa shilingi 2,800 milioni sawa na asilimia 74 ya matumizi yaliyoidhinishwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Chuo cha Mafunzo kimepokea jumla ya wanafunzi 474. Kati ya hao wanafunzi 462 ni wanaume na wanafunzi 12 ni wanawake. Idadi hii inaonesha kupungua kwa wanafunzi 73 waliopokelewa Chuoni hapo ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2009/2010 kama inavyoonekana katika kiambatanisho Nam 10.

Aidha, Chuo cha Mafunzo kimelima Ekari 74 za mpunga, Ekari 100 za muhogo, Ekari 15 za viazi vitamu na Ekari 5 za kilimo cha mboga mboga. Vile vile, jengo la Chuo cha Mafunzo Ubago pamoja na kujenga Bweni la kulala wanafunzi Kinu Moshi yamekarabatiwa. Ujenzi wa nyumba ya familia mbili Kangagani Pemba umefikia hatua ya kuezeka.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo cha Mafunzo kinatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kupima na kuyapatia hatimiliki mashamba ya Chuo cha Mafunzo yakiwemo Kinumoshi na Langoni.
- Kuendelea na Ukarabati wa Chuo cha Mafunzo Ubago.
- Kuendelea na ujenzi wa bweni la kulala Wanafunzi liliopo Kinumoshi.
- Kuendelea na ujenzi wa nyumba ya familia mbili Kangagani-Pemba.
- Kuanza ujenzi wa nyumba ya familia mbili Ubago-Unguja.
- Kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Kanda ya mashamba – Langoni.
- Kubadilisha kivazi cha wanafunzi kutoka kitambaa cha maradufu nyeupe na kuwa kitambaa cha rangi ya machungwa.
- Kurejesha mlo wa tatu wa jioni kwa wanafunzi.
- Kulima Ekari 50 za mpunga, Ekari 110 za muhogo, Ekari 7 za viazi vitamu na Ekari 10 za mahindi.
- Kufanya mapitio ya Sera na kutayarisha Mpango Mkakati wa Chuo cha Mafunzo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika kuimarisha huduma za wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo, Serikali imekusudia kujenga Kituo Kipya cha Mafunzo cha kisasa katika mwaka wa fedha 2011/2012. Kituo hicho cha kisasa kinatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2015/2016. Lengo kuu la Mradi huu ni kuondosha msongamano uliopo katika Chuo cha Mafunzo Kilimani. Hatua hii pia itaanzisha Kituo kipya cha Mafunzo kwa wanafunzi watoto. Kazi zitazofanywa katika kipindi hichi ni upimaji wa kiwanja, utafutaji wa hati ya usajili wa ardhi, utayarishaji wa michoro ya Kituo kipya cha Mafunzo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ili Chuo cha Mafunzo kiweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe shilingi 3,938 milioni kwa kazi za kawaida na shilingi 400 milioni kwa matumizi ya maendeleo.

KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Mhe. Spika, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimeanzishwa kwa Sheria Nam. 7 ya 1999 na kina jukumu la kusimamia shughuli zote za uzimaji moto na uokozi wa maisha na mali za watu. Vile vile Kikosi kina jukumu la kusimamia na kuhakikisha kuwa huduma za zimamoto kwenye Viwanja vya Ndege vya Unguja na Pemba zinaenda kulingana na masharti ya kitaifa na kimataifa. Aidha, Kikosi kinasimamia kutoa huduma za kibinaadamu na ushauri wa mafunzo ya kujikinga na moto kwa wananchi, taasisi za serikali na za watu binafsi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kiliidhinishiwa shilingi 1,789 milioni kwa matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2011, Kikosi kiliingiziwa shilingi 1,254 milioni sawa na asilimia 70 ya matumizi yaliyoidhinishwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kikosi kimeripotiwa jumla ya matukio 258. Matukio 129 ni ya moto wa majumbani na mahoteli ya kitalii, matokeo 55 ni ya moto wa misitu na mashamba, matukio 30 ni ya moto wa *transformer* za umeme, matukio 12 ni ya moto wa gari, matukio matatu ni ya moto wa uongo pamoja na matukio 29 iliyohusisha uokozi wa watu na wanyama walioingi katika visima na mashimo. Matukio yote hayo kwa pamoja yamesababisha hasara ya jumla shilingi 961.9 milioni pamoja na vifo vya watu 11. Aidha, shilingi 6,462 milioni zimeokolewa wakati wa kuyakabili matukio ya ajali hizo na kuokoa maisha ya watu wanane na wanyama wawili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Kikosi cha Zimamoto kimeimarisha huduma zake za tahadhari ya moto katika Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba na kuhakikisha usalama wakati ndege zikitua, kuruka na kujaza mafuta. Aidha, Kikosi kimeimarisha mawasiliano katika vituo vya Chanjaani, Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba na Kigunda kwa kununua 10 Redio ndogo za mawasiliano *Antenna* nne, Redio mbili kubwa za mawasiliano, vifaa 10 vya kujikinga, Kofia 25 za kujikinga na ajali na nguo 35 za kujikinga na moto.

Mhe. Spika, kikosi kimefanya mazungumzo na Idara ya Usafiri na Leseni kuhusu utaratibu wa kuweka vifaa vya kuzimia moto katika kila gari kwa tahadhari ya moto. Aidha, Kikosi kwa mara ya kwanza kilishiriki katika gwaride la kusherehekea miaka 47 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na gwaride rasmi la kumuaga Rais wa Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Kikosi kinakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuendelea kutafuta vifaa na gari za kisasa vya kuzimia moto na kusambazwa kwenye maeneo mapya na yale ambayo huduma zake bado hazijakamilika hasa kwa upande wa Pemba.
- Kuimarisha mawasiliano ya uhakika ndani ya Kikosi.
- Kuendelea kufanya ukarabati wa majengo pamoja na kujenga vituo vipya vya Zimamoto katika maeneo ya Uroa na ujenzi wa nyumba za mapumziko za Kikosi, Pemba.
- Kuwapatia sare na vifaa wapiganaji wa Kikosi.
- Kuwapatia mafunzo mbali mbali Maafisa na wapinganaji 100 ndani ya nchi na sita nje ya nchi.
- Kutoa elimu zaidi kwa jamii ya kujikinga na majanga ya moto, pamoja na uchimbaji visima vya maji vyenye usalama.
- Kutafuta eneo jipya la kuegesha gari za Zimamoto katika Wilaya ya Mjini Unguja (*Standby Station*). Eneo liwe ndani ya Manispaa ya Zanzibar pia liwe karibu na barabara kuu.
- Kutayarisha Mpango Mkakati wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi.

Mhe. Spika, ili Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kiweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe shilingi 1,883 milioni kwa kazi za kawaida.

KIKOSI CHA VALANTIA

Mhe. Spika, Kikosi cha Valantia kimeanzishwa kwa Sheria Nam. 5 ya mwaka 2004 na kina majukumu ya kutoa ulinzi kwa kushirikiana na vikosi vya ulinzi na usalama vya SMT na vya SMZ. Kusaidia kulinda raia na mali zao. Kutekeleza shughuli za kijeshi kwa wakati wa dharura kwa ajili ya kulinda na kuweka usalama wa nchi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Kikosi cha Valantia kiliidhinishiwa TZS 2,182 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 100 milioni kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, kikosi kiliingiziwa TZS 1,626 milioni sawa na asilimia 75 ya matumizi kwa za kazi za kawaida na TZS 100 milioni sawa na asilimia 100 ya makadirio ya matumizi ya kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, Kikosi cha Valantia kimewajengea uwezo wapiganaji wake kwa kuwapatia mafunzo katika fani mbali mbali, ndani na nje ya Zanzibar. Aidha, Kikosi kimefanya ukarabati wa majengo katika baadhi ya Kambi zilizopo Unguja na Pemba. Mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Valantia umeendelea vizuri hapo Mtoni. Hatua iliyofikiwa ni kukamilisha uwekaji wa vigae vya sakafuni *(tiles)* katika baadhi ya Ofisi, uwekaji wa vipoza hewa na upakaji

rangi. Vile vile, imejengwa sehemu ya mapokezi. Kikosi cha Valantia kimehamia rasmi katika Makao Makuu yake ya Mtoni.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Kikosi cha Valantia kitatekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuimarisha nguvu za ulinzi na usalama.
- Kuwaendeleza na kuwapatia elimu wapiganaji wa Kikosi katika fani mbali mbali.
- Kuendelea kuwapatia sare na vifaa vya ulinzi wapiganaji wote wa Kikosi.
- Kuendelea kuyafanyia ukarabati majengo ya Kikosi.
- Kuyapatia hati miliki maeneo ya vikosi Unguja na Pemba.
- Kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa kununua kompyuta nne (4) na printa nne (4).
- Kukamilisha ujenzi wa jengo la makao makuu yakiwemo ghala la kuhifadhia vifaa mbali mbali vya kikosi na ujenzi wa mesi.

Mhe. Spika, ili Kikosi cha Valantia kiweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe TZS 2,453 milioni kwa kazi za kawaida na TZS 100 milioni kwa kazi za maendeleo.

OFISI YA AFISA MDHAMINI PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za utawala, huduma za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zinazofanyika Pemba. Aidha, Ofisi hii inaratibu ziara za Viongozi wakuu wa kitaifa na kimataifa wanapotembelea Pemba. Majukumu mengine ni pamoja na kuratibu usimamizi wa nyumba za Ikulu, Idara Maalum za SMZ na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, iliidhinishiwa TZS 293 milioni kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi 2011, Ofisi imepatiwa TZS 187 milioni sawa na asilimia 64 ya makadirio ya matumizi na kutekeleza yafuatayo:-

- Imeratibu ziara sita za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, mbili kati ya hizo zilifanywa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar wa awamu ya sita na nne zimefanywa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar wa awamu ya saba. Ziara moja ilifanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nne za Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, katika

kipindi hicho Ofisi imeratibu ziara moja ya mke wa Rais wa Zanzibar na moja ya mke wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

- Imewapatia nafasi za mafunzo wafanyakazi saba ndani ya nchi, watano katika ngazi ya stashahada na wawili katika ngazi ya cheti.
- Imesimamia ukarabati wa majengo ya Ikulu ya Chake Chake na Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.
- Imenunua vitendea kazi vikiwemo vespa mbili, Kompyuta mbili na samani za Ofisi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- Kuratibu na kusimamia shughuli zote za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba ikiwemo ziara za Viongozi wakuu.
- Kuwajengea mazingira mazuri wafanyakazi pamoja na kuwapatia taaluma ya kujikinga na maambukizi mapya ya UKIMWI.
- Kufanya ukarabati wa jengo la Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba na kununua vitendea kazi na samani.

Mhe. Spika, ili Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba iweze kutekeleza malengo yake kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 365.5 milioni kwa kazi za kawaida.

JUMLA YA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Spika, baada ya kutoa maelezo juu ya utekelezaji wa malengo ya Idara na Taasisi zote zilizo chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, sasa naomba ruhusa yako kutoa maelezo ya muhutasari wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na maombi ya fedha kwa mwaka 20011/2012.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2010/2011, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ilikadiriwa kutumia ya TZS 32,559 milioni. Kati ya hizo TZS 26,511 milioni kwa ajili ya kazi za kawaida, TZS 3,610 milioni kwa ajili ya kazi za maendeleo na TZS 2,438 milioni kwa ajili ya ruzuku.

Mhe. Spika, ili Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iweze kutekeleza malengo na majukumu yake, kwa mwaka wa fedha 2011/2012,

naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe TZS 33,127.2 milioni. Kati ya hizo, TZS 29,386.2 milioni kwa kazi za kawaida, TZS 1,930.0 milioni kwa kazi za maendeleo na TZS 1,811.0 milioni kwa ajili ya ruzuku.

Mhe. Spika, uchambuzi wa fedha zilizoombwa kwa mwaka wa fedha 2010/2011, zilizopatikana na kutumika hadi mwezi Machi 2011 pamoja na fedha zinazoombwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 zimeoneshwa kwenye viambatanisho namba 11 na 12.

MWISHO

Mhe. Spika, kwa kumalizia hotuba hii naomba kuchukua fursa nyengine kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Ali Mohamed Shein kwa namna alivyoweza kutekeleza shughuli za Serikali kwa uadilifu na utaratibu aliouanzisha kwa kufuatilia kwa vitendo shughuli hizo katika kipindi kifupi cha uongozi wake. Hali hii imetupa changamoto sisi viongozi na kuona haja ya kubadilika na namna bora ya kuwatumikia wananchi. Namuomba Mwenyezi Mungu ampe nguvu Mheshimiwa Rais wetu aweze kuiongoza vyema nchi yetu na kufikia maendeleo tuliyokusudia.

Mhe. Spika**,** mwisho naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa wananchi wote wa Zanzibar kwa kuendeleza umoja, amani na utulivu. Nawashukuru sana Marafiki zetu waliopo ndani na nje ya Nchi yetu. Daima tupo tayari kufanya kazi nao bega kwa bega kuleta maendeleo Zanzibar. Pia nawapongeza wafanyakazi wote wa Serikali, wafanyakazi wa Sekta binafsi pamoja na Taasisi za Kiraia kwa kujituma na kufanya kazi kwa bidii ingawa kuna changamoto nyingi zinazotukabili. Naomba kutoa ujumbe kwao kwamba ari hiyo ya kufanya kazi kwa pamoja iendelee kwani wahenga wamesema *"UMOJA NI NGUVU".*

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba kutoka shukrani zangu za pekee kwa viongozi, watendaji wakuu na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushirikiano wao walionipa na katika kufanikisha kuandaa hotuba hii ambayo nimeiwasilisha kwenu.

Mhe. Spika, Nawashukuru wote kwa kunisikiliza kwa makini wakati wote na natanguliza shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa michango yenu mtakayoitoa katika kuijadili hotuba ya bajeti hii.

Mhe. Spika, Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. waziri kwa kuwasilisha hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapindu, umetumia muda wa saa mbili na dakika kumi, ni dhahiiri kutumia muda huo kwa sababu kitabu hiki ni kikubwa kinakaribia na kile cha waziri wa masuala ya Fedha wakati wa bajeti ya serikali, hoja imeungwa mkono na kuashirika sasa ianze kuchangiwa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi (Makamo Mwenyekiti Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa: Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kusimama tena mbele ya Baraza lako tukufu ili kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa juu ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na Makadirio ya mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, Pia napenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Mwinyihaji Makame na watendaji wake wa Ofisi hii kwa kuwasilisha kwa umakini mbele ya kamati taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2010/2011 na mwelekeo wa bajeti ya Ofisi kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, napenda pia kuwashukuru waheshimiwa Wajumbe wa Kamatiya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa ushirikiano na umakini wao wakati wa kuchambua na kutathmini kwa kina Bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza laMapinduzi. Naomba niwatambulishe kwa kuwataja wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
3. Mhe. Ali Salum Haji
4. Mhe. Mgeni Hassan Juma
5. Mhe. Mohammed Haji Khalid
6. Mhe. Salma Mohammed Ali
7. Mhe. Ussi Jecha Simai
8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni
9. Ndg. Ramadhan Kh. Masoud

Mhe. Spika, mhe waziri katika hotuba yake ameelezea muundo wa wizara yake kama hivi ifuatavyo;-

- ❖ Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.
- ❖ Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

- ❖ Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
- ❖ Ofisi ya Faragha.
- ❖ Kitengo cha Usalama wa Serikali *(G.S.O)*
- ❖ Idara ya Mawasiliano Ikulu
- ❖ Idara ya Usajili wa Kadi za Utambulisho.
- ❖ Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.
- ❖ Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- ❖ Idara ya Uhusiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Ughaibuni.
- ❖ Ofisi ya Afisa mdhamini Pemba.

Maoni na ushauri wa kamati kuhusiana na utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2010/2012 na mwelekeo wa bajeti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi 2011/2012

Idara ya mipango Sera na Utafiti

Mhe. Spika, kamati inapongeza jitihada zilizochukuliwa na ofisi hii, kwa kuyafanyia matengenezo majengo ya Ikulu na nyumba za serikali Unguja na Pemba. Hata hivyo, kamati inasisitiza yafuatayo katika suala la matengenezo na ujenzi wa majengo hayo:-

Majengo ya Ikulu ya Mkoani yanahitaji kujengwa upya kutokana na hali mbaya iliyonayo pamoja na kuzungushiwa uzio wa ukuta. Tumefurahi kuona kwamba suala hili kamati baada ya kutembelea na kutoa ushauri basi tayari suala hili limeanza kuchukuliwa hatua mara moja.

Mhe Spika, kamati yangu ilishauri kuchimbwa kisima kwenye Ikulu ya Wete lakini tumepata maelezo ya kwamba kutawekwa laini ya maji ambayo itaondoa tatizo la maji katika Ikulu hiyo kwa hiyo tunaomba suala hili kukamilishwa mara moja ili kuwe na maji ya kutosha na ile bustani ipate kuimarishwa. Vile vile kamati inaikumbusha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuitengeneza upya sakafu iliyomo katika maeneo ya Ikulu ya Chake Chake kwani sakafu iliyopo imechakaa na hairidhishi.Vile vile Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni vyema iendelee kuzungumza na Wizara ya Miundombinu ili kuifanyia matengenezo barabara iendayo Ikulu ya Chake Chake.

Mhe Spika**,** Kamati pia inatilia mkazo kwa Serikali kufikiria kutafuta eneo kwa ajili ya ujenzi wa makaazi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwani makaazi ya sasa ya Mheshimiwa Rais hapo Migombani yapo karibu sana na barabara kuu inayotumika muda wote. Hali ambayo inaweza kuhatarisha usalama wa eneo hilo, vile vile Kuwekewa uzio kwa majengo ya Serikali ya Bwefum na Mkokotoni. Aidha, jengo la Serikali la Mkokotoni ni vyema likapatiwa walinzi na vile vile likatenganishwa na nyumba ya Mkuu wa Mkoa ili kulipa hadhi ya matumizi ya Rais. Mhe Spika, pia tunashauri tunshauri kuimarishwa bustani ya Ikulu ya kibweni.

Mhe Spika, tunashauri Ofisi ya Rais ishirikiane na Idara ya Mazingira kutathmini tatizo la uharibifu wa mazingira unaosababishwa na maji ya bahari yanayoendelea kuimaliza ardhi katika eneo la Ikulu ya Bwefum. Pia yunahsauri kwamba Viwanja na majengo yote ya Serikali yawe na hati miliki kuepusha mizozo ambayo kwa hivi sasa imekuwa ni tatizo sugu kwa taasisi zote za Serikali , hapa tunasisitiza Serikali kumaliza tatizo hili kwa haraka ili kuondoa mizozo. Pia Serikali iangalie uwezekano wa kuzijenga nyumba za viongozi mbali na eneol la fukwe kuepusha athari ya chumvi kwa nyumba hizo na mmong'onyoko wa ardhí.

Kitengo Cha Usalama wa Serikali (*G.S.O)*
Mhe. Spika, kamat**i** inatambua na kuzithamini kazi zinazotekelezwa na kitengo hiki.Hata hivyo, kamati imebaini kwamba baadhi ya taasisi za Serikali zinaajiri wafanyakazi bila kufuata sheria na utaratibu wa upekuzi *(Security Vetting)* hali inayopelekea kuajiriwa watu wasiokua na sifa na uaminifu.Hivyo, kamati inaishauri Ofisi ya Rais kupitia kitengo hiki kuzielimisha taasisi za Serikali kufuata sheria na taratibu za uajiri kwa lengo la kuepusha udanganyifu katika ajira. Ambapo kwa siku za hivi karibuni kumejitokeza vijana wengi kufoji vyeti au kutumia vyeti vya Skuli visivyokuwa vyao ili kupata ajira na baadae kupata watumishi wasiokuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa maeneo wanayopangiwa.

Idara ya Mawasiliano Ikulu
Mhe. Spika, kamati inapongeza utendaji wa kazi nzuri zinazofanywa na idara hii. Ingawa kwaa bajet ya mwaka huu fungu lake la matumizi limepunguzwa kwa kiasi kikubwa lakini Hata hivyo, kamati inaishauri idara hii kumshauri mara kwa mara Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi ili kurahisisha ufanisi katika utekelezaji wa ahadi zinazotolewa na Mhe Rais. Aidha kamati inaiomba Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kufuatilioa utekelezaji wa ahadi zinazotolewa na viongozi wastaafu, ambazo hazijatekelezwa ili zipate kutekelezwa.

Idara ya Usajili wa Kadi za Utambulisho
Mhe. Spika, kamati imefarajishwa na utekelezaji wa kazi unaofanywa na idara hii.Lakini pia kamati inaitaka Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuipatia idara hii posho nyeti kutokana na uhalisia wa kazi wanazozifanya. Kwa kuwa suala hili bado limo ndani ya uwezo wa wizara basi tunashauri litekelezwe ndani ya bajet ya mwaka huu. Aidha kuna umuhimu wakulifanyia matengenezo jengo lao lililopo migombani ili kuiwezesha ofisi kuondosha ufinyu wa eneo ilio nao hivi sasa. Kamati yangu inpongeza Idara hii hasa kwa kutoa vitambulisho bora na kupata tunzo ya ubora kila mwaka.

Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
Mhe. Spika, kamati inaipongeza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kuendelea na mchakato wa kukamilisha marekebisho ya Sheria ya Uanzishwaji wa Serikali za Mitaa. Hata hivyo, kamati imeagiza kuongezwa kwa kasi ya ukamilishaji wa marekebisho hayo kwa lengo la kuimarisha utawala bora na kuwapatia maendeleo wazanzibari.

Vile vile, kamati, inaona kwamba bado Serikali haijatenga fedha za kutosha katika eneo hili, shilingi 100,000,000 zilizotengwa kwa ajili ya kazi za kukamilisha zoezi hili kwa mwaka 2011/2012 hazitoshelezi hata kidogo , hapa Serikali yetu ni lazima ilitilie mkazo suala hili kwani kwa fedha zilizotengwa hatutegemei suala hili kukamilka kwa haraka kama tunavyotegemea, kuna haja kwa serikali kuu kuzipa umuhimu mkubwa serikali za mitaa kwa kuzitengea fedha wanazozihitaji. Lakini bila kukamilika kwa maboresho hayo basi hakuna utaratibu wa halmashauri kupata fedha za kutosha.

Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Mikoa, Halmashauri na Mabaraza)
Mhe. Spika, Kamati inathamini sana kazi zinazotekelezwa na ofisi za Wakuu wa Mikoa ya Zanzibar.Hata hivyo kamati yetu kwa upande wake haikuridhishwa na fedha zilizotengwa kwa shughuli za maendeleo kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja na ule wa Kusini Unguja. Hivyo kamati inaona kuna haja ya kuipa kipaumbele mikoa kwa kuitengea fedha za kutosha kwa miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, kamati yetu inaikumbusha Serikali kuwapatia majengo ya kisasa na yatayokidhi haja wakuu wa Mikoa hasa ukitilia maanani baadhi ya Wakuu wa Mikoa mfano Kusini Pemba na Mjini Magharibi Unguja wanafanya kazi katika majengo chakavu na yasiyoridhisha. Hapa pia tunaitaka ofisi ya mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi kuandaa program maalum ya kuendeleza

ujenzi wa ofisi yao ilyopo hapo Amani, vile vile kamati yangu inamuonya Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi kuacha tabia ya kudharau kamati yangu kwa kudharau kushiriki katika vikao vya kamati, kwani kamati zetu zinafanya kazi kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, Kamati inazipongeza kwa dhati Halmashauri zilizoanzisha na kutekeleza zoezi la uchukuaji wa taka katika hoteli na majumbani.Hali hii inaenda sambamba na kauli ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar wa kuitaka jamii ibadilike kwa kuiweka Zanzibar katika hali ya usafi.Hata hivyo,kamati imeagiza Halmashauri ya Magharibi kuongeza wigo wa kuchukua taka hizo ili lengo lililokusudiwa lifikiwe.

Aidha kamati inaziagiza Halmashauri nyenginezo kuiga mfano wa Halmashauri za Kusini, Unguja, Mjini/Magharibi kuchukua taka mahotelini na majumbani ili kuimarisha usafi. Hapa tunawaomba sana Halmashauri na mabaraza ya miji kuhakikisha usafi katika maeneo yetu kwani wageni wengi hasa watalii wanatoa kasoro utalii wetu hasa kushindwa kuweka safi miji yetu, hii ni kasoro kubwa. Mhe Spika, tunalitaka Baraza la *Municipal* kukaa pamoja na kamisheni ya Utalii pamoja na Bodi ya *ZAT* ili kuzungumzia suala la utupaji taka katika eneo la Maruhubi kwani kumejitokeza malalamiko kwamba eneo hilo kuna maeneo ya kihistoria na watalii wengi wameanza kulalamikia uchafu katika eneo hilo.

Mhe. Spika, kamati kwa upande mwengine inaiagiza Mikoa na Halmashauri kutekeleza sheria na agizo la Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kuhakikisha kwamba mifugo kama vile ng'ombe ,mbuzi na kondoo haizururi ovyo barabarani hasa mijini. Kamati imebaini kwamba agizo hilo bado halijafanyiwa kazi.
Mhe. Spika, kamati vile vile inaviagiza vitengo vya habari katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa kushirikiana na kitengo cha habari Ikulu ili kukiwezesha kitengo hicho kupata taarifa za maendeleo ya Mikoa na nchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine, kamati inazisisitiza taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa upande wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaaa kuwa makini na ufungaji wa mikataba pamoja na ukusanyaji wa mapato ili kuepusha malumbano ndani ya taasisi hizo.

Kwani kumenza kuwa na malalamiko kwamba Halmashauri na Mabaraza ya miji huwa hawafuati taratibu za kisheria hasa katika ufungaji wa mikataba na makampuni wanayoomba kazi za kuweka matangazo yao. Pia tunamba kuwekwa mipaka inayoeleweka kwa kutofautisha mipaka waziwazi inayotenganisha mipaka ya Halmashauri ili kuondoa mgongano hasa katika ukusanyaji wa mapato.

Idara ya Uhusiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Ughaibuni *(Diaspora)*

Mhe. Spika, kamati yetu inapongeza kwa dhati hatua zilizochukuliwa na Mhe Rais wa Zanzibar kwa kuanzisha kitengo maalum kinachoshughulikia uratibu wa wazanzibari wanaoishi nchi za nje *(diaspora).* Uanzishwaji wa kitengo hiki utaweza kuisaidia Zanzibar kiuchumi na kijamii.Kamati kwa ujumla inafarajishwa na hatua zinazochukuliwa na kitengo hiki katika kuandaa utaratibu wa kuhakikisha kwamba wazanzibari waliopo nje ya nchi wanachangia nguvu zao katika kuiendeleza Zanzibar.

Hata hivyo kamati inaendelea kuikumbusha Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia kitengo hiki, pia kuwasaidia wazanzibari wanaoishi nje, ambao wanahitaji kurudi Zanzibar lakini hawana uwezo wa kifedha kuweza kurudi kwao. Pia katika zoezi hilo kuangalia uwezekano wa kuwaandalia wazanzibari walioko nje kuweza kutuma pesa zao hapa kwetu kwa njia ya kibenki ambayo itawahakikishia usalama wa fedha zao na pia kuingiza mapato kwa nchi yetu. Pia kuangalia namna ya walivyozipata fedha hizo ili Zanzibar isije ikawa ni njia ya kusafirisha fedha kharam za zinazochumwa kwa magendo na uuzaji wa madawa ya kulevya.

Mhe. Spika**,** kwa upande wa mpango mpya unao zungumzwa hivi sasa kwa watalii wanakuja nchi za Afrika ya mashariki na kusini kuweza kutumi viza moja *(UNI VIZA)* ukweli ni kwamba utaratibu huu si mzuri hata kidogo kwa Zanzibar, kwa sababu kwa asilimia mia moja Zanzibar haitoweza kupata mapato kutoka kwa watalii au wawekezaji watakaotumia utaratibu huu.pia kutekelezwa kwa suala hili kutaiumiza sana Idara ya Uhamiaji hapa Zanzibar kwani kwa asilimia kubwa hupata mapato yao kutegemea mapato ya viza.

Hivyo basi kabla ya suala hili kufikishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kuridhiwa na wabunge wa pande mbili za Muungano, kuna haja kwa Serikali ya Zanzibar kukubaliana na serikali ya Muungano kuona namna gani Zanzibar itafaidika kimapato, vyenginevyo Uni Visa kwa kutumia balozi za Tanzania zilizoponje ya nchi zinaweza kufaidisha kiuchuni upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano na kuudumaza upande mwengine.

Kamati vile vile inaona kwamba kuna haja kwa Mawaziri wa Bara na wale wa Zanzibar, kama kuna masuala yanayohusu maslahi ya Tanzania Bara na Zanzibar, wakutane kabla ya kwenda kwenye vikao vya kanda, ili wakubaliane kwa pamoja kuhusu maslahi hayo kwa lengo la kuepusha malalamiko siku hadi siku. Aidha kwa upande mwengine, kamati inaona kwamba umefika wakati

Zanzibar iende katika vikao hivyo kama nchi na sio kuwakilishwa na Jamhuri ya Muungano, hasa ikitiliwa maanani kwamba masuala ya Zanzibar wanayoyajua ni wazanzibari wenyewe. Na pia kuna masuala mengi yanayozungumzwa huko sio masuala ya Muungano.

Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena kamati yetu inapongeza utendaji mzuri wa kazi inayofanywa na idara hii kupitia vikosi vyake zikiwemo kazi za ujenzi wa taifa,kazi za amali pamoja na ujenzi wa skuli na hospitali ambazo husaidia sana wanajamii. Mbali na utendaji mzuri wakujenga taifa na kulinda usalama wa mali za wananchi na usalama wa nchi, idara hii inakabiliwa na tatizo kubwa la ufinyu wa bajeti hali inayopelekea kuzorota kwa uwajibikaji kutokana na kazi nzito wanazozifanya. Aidha idara inakabiliwa na upungufu wa vitendea kazi pamoja na uchakavu wa mashine hali ambayo husababisha mapungufu makubwa katika utendaji wa kazi zao. Hivyo, kamati inashauri yafuatayo kwa Idara hii na Serikali kwa ujumla.

Jeshi la Kujenga Uchumi
Kamati inasisitiza yafuatayo kupitia kikosi hichi:-

Kamati inapongeza kikosi hichi Kwa ujenzi wa skuli ya sekondari katika kambi yao ya Mtoni pamoja na kazi nzuri wanazozifanya zikiwemo kazi za amali na ujenzi wa taifa. Hata hivyo kamati inaikumbusha Serikali kukiimarisha kikosi kwa kukipatia zana ili kiweze kufikia lengo lililokusudiwa la kuanzishwa kwake. Aidha, kamati inaikumbusha serikali kuimarisha maslahi ya wapiganaji na walimu wa skuli ya JKU Mtoni kwani bado maslahi yao ni madogo ukilinganisha na kazi wanazozifanya
Kamati inasisitiza kuanzishwa kwa akaunti ya pamoja kati ya JKU na Misri katika mradi wa shamba la pamoja la mboga mboga kuwezesha utekelezaji mzuri wa mashirikiano na utekelezaji wa mradi wa mboga mboga huko Bambi.

Mhe. Spika: Inavyoonekana Waheshimiwa Wajumbe muda uliobaki hautomtosha Makamo Mwenyekiti, kumaliza kusoma hotuba yake hii. Nafikiri haichukui muda mkubwa sana. Kwa hiyo nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi ili atuwekee utaratibu ili Makamo Mwenyekiti amalize kusoma hotuba yake.

KUONGEZWA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda uliopo mbele yetu hautoshi kwa Mhe. Mwenyekiti wa Kamti ya Viongozi wa Serikali kuwasilisha hotuba yake. Hivyo naliomba Baraza lako liridhie tuweze kumaliza hotuba yake kwa kufuata kanuni za muda.

Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi (Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Ahsante Mhe. Spika, aidha kamati inasisitiza uchimbaji wa visima katika mabonde ya JKU, kwa Pweza na Msaani huko Pemba kuimarisha shughuli za kilimo katika mabonde hayo na yale yaliyo jirani. Upatikanaji wa maji ya uhakika katika mabonde hayo kutaiwezesha JKU kufanya shughuli za kilimo kwa ufanisi kulikoni hivi sasa hutegemea mvua ambazo hunyesha kwa msimu lakini pia hazitabiriki. Sambamba na hilo, kuna haja kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Mali Asili kuangalia uwezekano wa kuisaidia JKU kuipatia matrekta kuimarisha shughuli za kilimo katika mabonde yake yaliyopo Unguja na Pemba.

Kamati inaishauri serikali kuitumia JKU katika shughuli za ulinzi katika taasisi za Serikali badala ya kutumia kampuni za ulinzi kutoka nje ya Zanzibar. Lengo ni kuimarisha shughuli za kikosi hiki.

Kamati pia inashauri kuanzishwa kwa shirika la JKU ambalo litatumika kwa ajili ya kazi za ulinzi, ufundi, ujenzi pamoja na kuendesha kikosi. Lengo kuliwezesha jeshi kubadilika na kujiongezea mapato.

Kamati inasisitiza ajira za vikosi vyengine vya ulinzi kama vile polisi, jeshi la wananchi na usalama zitokane na vijana kutoka JKU, ambao huwa tayari na mwelekeo wa kazi hizo na kuepukana na utaratibu wa kuajiri vijana ambao baadhi yao huwa hawana maadili na kazi za kiaskari.

Kamati pia inasisitiza kikosi kuchukua jitihada za kuchimba kisima katika maeneo yake ya Mtoni kuweza kupata maji. Mhe Spika tunaishauri Serikali kukitengea fungu maalu kikosi hichi ili kuwachukua vijana wengi na kuwalipa posho la sabuni vijana hawa ili kuweza kujenga taifa na kuwapatia ujuzi wa ufundi na kuweza kujitegemea baada ya kutoka wanaporejea mitaani.

Kikosi cha Zima Moto

Kamati inaagiza kuwekwa kituo cha zima moto Katika Bandari ya Malindi kurahisisha shughuli za uokozi zinapotokea ajali mbali mbali bandarini hapo.

Kamati vile vile inaishauri serikali kupitia mamlaka ya uwanja wa ndege kukipatia kikosi hiki jengo linaloratajia kuhamwa na wafanyakazi wa uwanja wa ndege ili waweze kutumia kwa kazi zao. Ukweli ni kwamba kwa hivi sasa kikosi hiki hakina ofisi inayotazamika katika uwanja wa ndege. Pia tunaitaka

mamlaka ya Uwanja wa ndege kufunga mkataba na kikosi cha Zimamoto ili kuweza kutoa huduma zenye ubora na kukidhi kukiweka kiwanja chetu kuwa chenye ubora zaidi kiusalama kimataifa.

Kamati vile vile inaishauri serikali kukamilisha ujenzi wa uzio wa ukuta katika uwanja wa ndege Kisauni ili kuzuia uingiaji wa wanyama ambao wanaweza kuja kusababisha hatari na hasara kubwa kwa taifa.

Kamati inaishauri Mamlaka ya Maji kushirikiana na zima moto kuhakikisha kwamba kikosi hiki kinapatiwa huduma za maji katika maeneo ambayo yalikusudiwa kwa matumizi ya Zimamoto kwa ajili ya kurahisisha kazi za uokozi katika maeneo ya mijini na vijijini. Hivi sasa kikosi hiki husumbuka kupata maji katika baadhi ya maeneo na kupelekea kazi za uokozi zitekelezwe katika mazingira magumu.Kamati pia inasisitiza upatikanaji wa vifaa kwa kikosi hichi kama vile nguo na madawa.

Kamati inashauri kuongezwa idadi ya askari katika kikosi hichi kutokana na uhaba wa askari waliopo hivi sasa.

Kamati pia inaishauri Zimamoto kushirikiana na Idara ya Ardhi katika upimaji wa maeneo ili kuepuka ujenzi holela ambao husababisha athari katika majanga yatokanayo na moto lakini pia ni busara kwa zima moto kushirikishwa katika ujenzi wa majengo ili kutoa maelekezo yanayohitajika. Hivi sasa Zimamoto inashirikishwa zaidi katika ujenzi wa mahoteli. Kamati vile vile inashauri Serikali kukipatia kikosi hiki maeneo ya Garagara na Mwanakwerekwe kwa ajili kuwekwa vituo vya zima moto kurahisisha kazi za uokozi katika maeneo mbali mbali.

Chuo Cha Mafunzo

Kamati inasisistiza ujenzi wa vyuo vya mafunzo vya kisasa na kuondokana na mazingira ya sasa kuwa na vyuo ambavyo kwa ujumla haviridhishi kimajengo na hata huduma. Hivyo, kuna umuhimu kwa Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuviimarisha vyuo hivi.

Kamati vile vile inasisitiza kujengwa Chuo cha Mafunzo cha watoto na kuondokana na mazingira ya sasa watoto hao kuwekwa pamoja na watu wazima kuwaharibu baadhi yao huwaharibu kisaikolojia watoto hao. Kamati yangu inashauri kwamba chuo cha mafunzo cha watoto kijengwe eneo tofauti kabisa mbali na na watu wazima lakini pia askari watakao wahudumia pia wasivae nguo za kiaskari ili kuwaondoa mawazo kwamba wako katika kifungo.

Kamati pia inaikumbusha serikali kuwapatia taaluma wana chuo juu ya elimu ya ukimwi pamoja na kuwapatia kazi za amali ili wanapomaliza vifungo vyao na kwenda katika jamii waweze kujitegemea. Hivi sasa vyuo vyetu vya mafunzo kwa ujumla havina kazi za Amali

Kamati inasisitiza uharakishwaji wa kesi ili kupunguza mahabusu ambao huitia hasara serikali.

Kamati vile vile inaishauri serikali juu ya urekebishaji wa baadhi ya sheria ambazo huwakosesha haki wana chuo.

Kamati mwisho kwa upande wa Chuo cha Mafunzo inaipongeza timu yake ya mpira wa miguu kwa kuweza kutwaa Kombe la Ubingwa wa Zanzibar. Kamati inawatakia maandalizi mazuri katika michuano yao ya Kimataifa.

Kikosi Cha Valantia.
Kamati inasisitiza kupatiwa vitanda kwa kikosi hiki kwa ajili ya kulaza askari katika mabweni yake yaliyopo Makao Makuu Mtoni.

Kamati pia inatoa pongezi kwa KVZ kwa kuwa na jengo lenye kuridhisha lakini inakikumbusha kikosi hiki kurekebisha paa la jengo hilo kudhibiti uvujaji wa maji ya mvua katika jengo hilo.

Kikosi maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)
Kamati inakipongeza kikosi cha KMKM kwa ujenzi wa hospitali ya kisasa. Lakini pia inaishauri serikali kukipatia kikosi hichi vifaa vya uokozi kutokana na kuwa viliopo havikidhi haja.

Kamati pia inaishauri serikali kuifanyia kazi write up yakufufua chelezo kilichopo Mtoni makao makuu KMKM kwa lengo la kuiongezea mapato serikali.

Kamati pia inawapongeza wanamichezo wa KMKM kwa kuwa miongoni mwa wanamichezo wa Zanzibar, walioiwezesha nchi yetu kupata medali zikiwemo za dhahabu katika Michezo ya Riadha ya Kanda ya Afrika Mashariki, yaliyomalizika hivi karibuni mjini Dar- es- salaam. Kamati inathamini jitihada za wanamichezo hawa kwa kuiletea heshima Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ijapokuwa hawakuwezeshwa kushiriki katika mashindano hayo. Hivyo, kamati inawaomba wadau wote kuwawezesha wanamichezo wetu kushiriki vizuri katika mashindano ya kimataifa kwani wakiwezeshwa wanaweza wakafanya maajabu makubwa ulimwenguni.

HITIMISHO

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii tena kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii mbele ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, aidha napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza kwa kunisikiliza. Kwa niaba ya Kamati na kwa niaba ya Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. Ahsante

Mhe. Spika: Pongezi zimemtosha sana. Waheshimiwa wajumbe nakushukuruni na sasa naahirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 29/06/2011 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:48 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 29/06/2011 saa 3:00 asubuhi)